

# IMANI NA DESTURI ZA WABATISTI




Na Sam Turner

# IMANI NA DESTURI ZA WABATISTI




Na Sam Turner

# IMANI NA DESTURI YA WABATISTI

By

Sam Turner

Published and Printed by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi, Kenya

© Copyright 1989
Baptist Publications House, Nairobi
All Rights Reserved

Translated From *Baptist Beliefs And Customs*
© International Publications Services,
1987 Second Edition, used by permission

# DIBAJI

Wabatisti ni nani? Wanaamini nini? Kwa nini wanafanya mambo yao vile wanavyofanya? Pengine umewahi kuuliza maswali kama haya. Kitabu hiki kitajaribu kujibu maswali haya na pia kueleza juu ya imani na desturi za Wabatisti. Vile imani na desturi zilivyoanzishwa ni jambo la muhimu sana. Wabatisti wanaamini ya kwamba imani na desturi zinatakiwa kuanzishwa katika mwongozo unaofuata:

## 1. BWANA YESU KRISTO

Wabatisti wanamtegemea Bwana Yesu. Yesu ni Mwana wa Mungu na Mwokozi wa wote wanaomwendea kwa imani.

## 2. MAANDIKO

Imani na desturi za Wabatisti ni kutoka katika Biblia. Kwa vile Agano Jipya hueleza juu ya Yesu kama kamilisho la sheria na manabii (Agano la Kale), Wabatisti hutegemea Agano Jipya katika imani yao.

## 3. MAFUNDISHO YA BIBLIA

Mafundisho au kanuni za kanisa huanzishwa baada ya kusoma na kujifunza Neno la Mungu (Biblia). Kanuni hutegemea maandiko yote ya Biblia. Wale hujifunza kanuni, hulinganisha mstari mmoja na mistari mingine. Mistari kadha wa kadha kutoka katika vitabu mbali mbali hutumiwa katika kutunga na kuandika kanuni za dhehebu fulani (Batisti).

## 4. IMANI YA WABATISTI

Mafundisho ya Biblia huwa yale anayoyaamini mtu mwenye kuhusika wakati anapoyakubali katika maisha yake. Wabatisti wanayakubali mafundisho ya Biblia kama imani yao. Mafundisho yote yanatakiwa kupimwa au kulinganishwa na Neno la Mungu. Kwa hivyo Wabatisti hawafanyi mambo mengine yanayofanywa na madhehebu mengine kwa sababu hawaoni thibitisho la mambo hayo katika Biblia.

## 5. MATENDO AU DESTURI ZA WABATISTI

Matendo ya mtu hutokana na yale anayoyaamini. Matendo haya ambayo mtu huyatenda kila mara, ndiyo desturi za mtu. Wabatisti wanaamini ya kwamba desturi lazima ziongozwe na neno la Mungu. Kwa hivyo, lengo la kitabu hiki ni kueleza imani na desturi za Wabatisti. Hiki si kitabu cha mwongozo kwa ajili ya Wakristo. Kinauliza maswali mengi. Na majibu ya maswali hayo ni maoni na kuelewa kwa mwandishi kwa wakati huu.

## YALIYOMO


| SURA | | UKURASA |
|---|---|---|
| 1. | WABATISTI KATIKA HISTORIA YA WAKRISTO | 6 |
| 2. | KANISA LA AGANO JIPYA | 14 |
| 3. | KUSUDI LA KANISA | 20 |
| 4. | MSINGI WA IMANI YA WABATISTI | 26 |
| 5. | MAAGIZO YA KANISA | 36 |
| 6. | USHIRIKA WA KANISA | 44 |
| 7. | UONGOZI WA KANISA | 53 |
| 8. | UTAWALA WA KANISA | 63 |
| 9. | UHUSIANO WA KANISA | 73 |
| 10. | MAPATANO YA KANISA, TAARIFA NA TARATIBU ZA MIPANGO | 84 |

## MUHTASARI
## SOMO LA KWANZA

1. Je, baadhi ya mafundisho na matendo muhimu katika makanisa ya Agano Jipya yalikuwa gani?
   A. Yesu Kristo ni Bwana.
   B. Wokovu ni kwa imani tu.
   C. Waamini wanatakiwa kubatizwa.
   D. Ushirika wa kanisa unaleta wajibu kwa kila mshirika.

2. Je, ni mafundisho gani yalioanzishwa baada ya Agano Jipya kuandikwa?
   A. Kuwa mshiriki wa kanisa kulikuwa na maana ya kuwa ndani ya ufalme wa Mungu.
   B. Kubatizwa kulikuwa kuwa Mkristo.
   C. Kuwa Kasisi (au mchungaji), mtu alikuwa mtawala wa washiriki.
   D. Kufuata uamuzi wa baraza au kamati ya kanisa kulikuwa sawa na kufuata mafundisho ya Agano Jipya.

3. Je, mwongozo wa mwamini katika imani na desturi ni nini?

4. Je, chanzo cha umoja wa kanisa ni mambo ya kiroho ama ni mambo ya kawaida?

5. Je, historia ya Wabatisti ni ipi?

6. Je, tumejifunza nini kuhusu Wabatisti katika historia ya Wakristo?

## SURA YA KWANZA

## WABATISTI KATIKA HISTORIA YA WAKRISTO

Wabatisti ni Wakristo wa Agano Jipya. Makanisa ya Kibatisti ni makanisa ya Agano Jipya. Wabatisti hutegemea hali ya kiroho katika makanisa kwa ajili ya umoja wao. Madhehebu mengine hutegemea utaratibu wao kwa ajili ya umoja wao. Ili tuweze kujua mambo haya, ni vyema kujifunza historia fupi ya Wakristo na pia Wabatisti.

1. Je, baadhi ya mafundisho na matendo muhimu katika makanisa ya Agano Jipya yalikuwa gani?

Tukisoma Agano Jipya, tunaona mafundisho na matendo muhimu mengi. Hapa tutajifunza mafundisho mawili muhimu na pia desturi mbili muhimu.

A. Yesu Kristo ni Bwana.

Yesu wa Nazareti, aliye Kristo, ni Bwana. Hili ni jambo la kuamini na fundisho la msingi katika Agano Jipya. Yesu ni Mwana wa Mungu aliyejitoa mwenyewe kwa wokovu wetu. Sasa tuna njia ya wokovu. Yesu hutusamehe dhambi zetu. Yesu hutoa bure maisha mapya kwa watu wote wanaomjia kwa imani. Ili Yesu awe Bwana wa maisha yako, ni lazima ayatawale. Jina Bwana lina maana ya mtawala. Yesu ni Bwana au mtawala wa maisha ya Mkristo. Sisi tu watumishi wake. Kwa hivyo Wakristo hufanya mapenzi ya Yesu.

B. Wokovu ni kwa imani tu.

Agano Jipya hufundisha ya kwamba watu wote ni wenye dhambi. Mtu ni mwenye dhambi kwa tabia ya asili. Sisi tu watumwa wa dhambi. Dhambi zimetufanya wanajisi. Dhambi zetu zimetushtaki. Dhambi pia zimetufanya kuwa maadui wa Mungu. Walakini, Mungu katika Yesu Kristo hutupa wokovu. Wokovu ni kuzaliwa mara ya pili na kuacha asili yetu ya zamani ya dhambi (Yohana 3:3). Wokovu ni kupewa uhuru kutokana na utumwa wa dhambi (Yohana 8:36). Wokovu ni kusafishwa dhambi (I Yohana 1:7). Wokovu ni kuwekwa huru kutokana na hatia ya dhambi (Warumi 3:24). Wokovu ni kupatanishwa na Mungu (2 Wakorintho 5:18). Wokovu huja tu kwa kugeuka kutoka kwa dhambi zetu na kumwamini Yesu. Hatuwezi kujiokoa. Yesu ni wokovu wetu. Ikiwa mtu ye yote atatubu dhambi zake na kumpokea Yesu kama Bwana kwa imani, ataokolewa. Wokovu haupatikani kwa matendo. Hatuwezi kuununua. Twaweza kuupokea tu kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa imani. Imani ndiyo iletayo wokovu, na si matendo yetu.

C. **Waamini wanatakiwa kubatizwa**

Kwa kuzamishwa ndani ya maji: Makanisa ya Agano Jipya yaliwabatiza waamini kwa kuwazamisha ndani ya maji. Maana ya kuzamisha ni kudidimiza ndani ya maji kabisa. Na kwa hivyo maana ya ubatizo ni kuzamisha. Wale waliozaliwa mara ya pili, ndio waliobatizwa katika Agano Jipya. Walibatizwa kwa kuzamishwa kwa sababu walikuwa wameokolewa. Hawakubatizwa ili wawe Wakristo. Makanisa ya Agano Jipya yaliwabatiza waamini wapya kwa ushuhuda wa wokovu wao. Ushuhuda huu wa ubatizo ulikuwa mfano wa kifo, mazishi na ufufuo wa Yesu Kristo.

D. **Ushirika wa kanisa unaleta wajibu kwa kila mshirika.**

Lengo moja la Agano Jipya lilikuwa kwa washiriki wote kuwa Wakristo waaminifu. Ni wale tu waliozaliwa mara ya pili waliweza kuwa washiriki wa kanisa. Kama washiriki wa kundi la kiroho, wote walikuwa sawa mbele za Mungu. Walikubali kuwa washiriki kwa hiari yao wenyewe. Walikuwa na uhuru katika Kristo. Walikubali wajibu wao pale kanisani. Pia waliendelea kutafuta mapenzi ya Mungu katika maisha yao kadiri walivyoendelea kuabudu pamoja. Kila mshiriki alikuwa sawa na mwingine mbele ya Mungu. Washiriki wanao wajibu kila mmoja kwa mwingine.

Kanisa ni kundi la watu ambao wamempokea Yesu Kristo kama Mwokozi na wamebatizwa. Watu hao humwabudu na humtumikia Mungu pamoja. Wakati kanisa linapotafuta nafasi ya kufanya kazi na kushirikiana na makanisa mengine, wao huanzisha jumuiya katika eneo lao. Jumuiya hutaka kufanya kazi na kushirikiana na jumuiya nyingine. Kwa kawaida matokeo ni jumuiya kuu kwa taifa lote.

2. **Je, ni mafundisho gani yalioanzishwa baada ya Agano Jipya kuandikwa?**

Makanisa mengi yaliacha mfano wa mafundisho ya Agano Jipya. Katika karne zilizofuata, kulikuwa na mafundisho na matendo manne ya makosa ambayo yalianzishwa. Tunapojifunza haya, tunaelewa juu ya mwanzo wa mafundisho yaliyopotoka au yaliyo makosa ambayo tunayaona siku hizi. Haya yote hayafuatwi na dhehebu moja, lakini kumbuka ni mafundisho yaliyopotoka.

A. **Kuwa mshiriki wa kanisa kulikuwa na maana ya kuwa ndani ya ufalme wa Mungu.**

Mtu aliye ndani ya ufalme wa Mungu ni Kristo. Wachache walifikiri kwamba kuwa mshiriki wa kanisa ni sawa na kuwa mkristo. Hili ni fundisho ambalo limepotoka. Ni lazima mtu awe

Mkristo kwa njia ya kutubu na kumwamini Yesu. Mtu anapofanya hivyo, ataweza kuwa mshiriki wa kanisa. Mathayo 16:19 ilitafsiriwa vibaya. Makanisa yalianza kufikiri ya kwamba jinsi ya kuingia katika ufalme wa Mungu eti ni sawa na kuingia kanisani. Walifikiri ya kwamba mtu ye yote aliyeruhusiwa kuingia katika ushirika wa kanisa, alikuwa ameingia katika ufalme wa Mungu pia. Makanisa yakaacha mafundisho ya Agano Jipya yalipoanza kufuata kosa hili. Wakristo wanashika injili ambayo ndio ufunguo wa ufalme wa Mungu. Hawawezi kupokea wokovu kwa ajili ya mtu mwingine; wanashika ufunguo tu. Ni lazima Wakristo kuwaambia wengine juu ya Yesu. Ni lazima mtu azaliwe mara ya pili ili aweze kuingia katika ufalme wa Mungu, kabla ya kuweza kuwa mshiriki wa kanisa.

B. Kubatizwa kulikuwa kuwa Mkristo.

Kosa la kwanza lilizaa kosa la pili. Kosa hili la pili lilikuwa na maana ya kuwa Mkristo. Kosa hili pia lilitokana na tafsiri mbaya ya Mathayo 16:19. Njia ya kuwa mshiriki wa kanisa imekuwa ni mtu kubatizwa. Ikiwa ubatizo ndio ulikuwa mlango wa kuingia kanisani, makanisa yalifikiri eti ndio ulikuwa "ufunguo." Kwa hivyo alidhani ya kwamba ye yote aliyebatizwa aliweza kuingia katika ufalme wa Mungu. Kwa sababu ya kosa hili, hata wengine walifikiri ubatizo ungeweza kumwokoa mtoto mchanga. Haya ni mawazo ya watu wengi siku hizi, lakini Agano Jipya halifundishi hivi. Agano Jipya linafundisha ya kwamba kila mtu anaokolewa kwa neema ya Mungu katika imani.

C. Kuwa Kasisi (au mchungaji), mtu alikuwa mtawala wa washiriki.

Kosa la tatu lilikuwa ya kwamba, kuwa kuhani, kasisi au mchungaji kulikuwa na maana ya kuwa mtawala wa washiriki. Mchungaji alikuwa na wajibu wa kuwabatiza wale walioingia kanisani. Washiriki walifikiri ya kwamba mchungaji alihitaji kuwa mtakatifu zaidi kuliko wao. Kumwekea mtu mikono, kama vile tunavyosoma katika Kitabu cha Matendo kulianzishwa katika fundisho hilo la makosa kuhusu kuweka wakfu. Fundisho hili, lilifundisha ya kwamba kuwekwa wakfu ilikuwa njia ambayo mchungaji alipata neema maalum kutoka kwa Mungu. Hii ilitenganisha mchungaji na washiriki. Na baada ya miaka fulani, hata wachungaji waliweza kugawanywa katika daraja mbali mbali za kiofisi na pia uwezo.

D. Kufuata uamuzi wa baraza au kamati ya kanisa kulikuwa sawa na kufuata mafundisho ya Agano Jipya.

Tunaweza kuona kosa la tatu linaloendelea katika mafu-

ndisho mengine. Kwa sababu viongozi wa makanisa walikuwa wamewekwa wakfu na walioelimishwa, washiriki walikubali mafundisho yao. Viongozi hawa walitumia uwezo wao juu ya makanisa. Mara kwa mara viongozi walikutana pamoja. Mikutano hii iliitwa baraza au kamati ya kanisa. Watu wengi waliamini ya kwamba kamati hizi au mikutano ilikuwa na uwezo kuhusu yale Wakristo wangeamini na kutenda. Hata wengine waliamini ya kwamba uamuzi wa kamati ulikuwa na uwezo sawa na mafundisho yaliomo katika Agano Jipya. Kamati iliamua mambo mengi ambayo yalikuwa mema. Lakini pia kulikuwa na mambo mengine ambayo hayakuwa mema. Haya yalipoendelea yalileta kile tunachokiita "kuanzishwa kwa madhehebu yasiyokubali mafundisho ya Kirumi." Viongozi waliokataa mafundisho yaliopotoka waliitwa watengenezaji. Walitaka kusahihisha makosa. Walitaka kurudisha mafundisho ya Agano Jipya. Lakini kwa sababu ya mila au desturi za wakati huo, hawakuweza kukamilisha kazi hii.

3. Je, mwongozo wa mwamini katika imani na desturi ni nini?

Ni lazima tuamue mwongozo wetu katika imani na matendo ni nini. Wengine huamini mafikara au mawazo ya watu. Serikali kwa kawaida huwa na msingi katika mawazo ya watu. Lakini kumbuka mawazo ya watu hubadilika na hapo serikali pia kubadilika. Kuna wengine pia ambao hufuata vile wanavyojisikia mioyoni mwao kama mwongozo wa imani yao. Hali ya kujisikia hubadilika mara kwa mara. Wachache watakubali uamuzi wa kamati au baraza la kanisa. Na tumeona vile wakati mwingine wanakamati wanavyoweza kuamua mambo ya kupotosha. Mambo haya yote ni mazuri katika imani yetu; lakini yasiwe ndiyo mwongozo au uamuzi wa mwisho katika imani yetu.

Wabatisti wanaamini ya kwamba Agano Jipya ndiyo mwongozo na msingi wa imani na desturi za Mkristo. Ni Biblia tu ambayo haibadiliki. Wengine wote wanafuata na kutegemea watu. Maandiko matakatifu tulipewa na Mungu. Roho wa Mungu aliongoza watu kuandika ujumbe wake kwetu. Na kwa hivyo Wabatisti wanaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu. Wakristo hutafsiri Agano la Kale wakijua ya kwamba Kristo ndiye aliyeikamilisha. Tunaamini ya kwamba kanisa likifuata mafundisho ya Agano Jipya, litaitwa kanisa la Agano Jipya. Na ikiwa halifuati si la Agano Jipya. Agano Jipya ndio mwongozo katika imani na desturi.

4. Je, chanzo cha umoja wa kanisa ni mambo ya kiroho ama ni mambo ya kawaida?

Umoja ni kitu cha maana sana katika Afrika. Umoja ulitokana na jamii. Wakati mtu alipooa katika jamii fulani, jamii hizo mbili ziliona ya kwamba zimekuwa kitu kimoja. Kulikuwako na mawazo ya kwamba uhusiano huu ulikuwa wa kimwili. Lakini uhusiano huu ulikuwa wa kiroho.

Hii ni kweli hata kwa makanisa. Umoja wa kanisa ni wa kiroho wala sio wa kimwili. Jamii nyingi ambazo zina uhusiano wa kimwili hazina umoja. Makanisa mengine yana washiriki ambao hawana uhusiano wa kimwili, lakini yana umoja ulio wa kweli. Umoja wao umo katika uhusiano wao na Kristo Yesu. Kumbuka hatuwezi kuwa na uhusiano au ukoo mmoja na Yesu kimwili ila ni kwa njia ya makanisa.

Makanisa yanahusiana na makanisa mengine kama vile washiriki wanavyohusiana wao kwa wao. Kama katika jamii, kila mshiriki ana uhuru wa kufanya vile aonavyo ni vyema. Lakini kwa sababu yeye ni mmojawapo wa jamii, yeye hutaka kutenda yale yaliyo mema kwa jamii yote. Washiriki wa kanisa wana uhuru wa kufanya mapenzi ya Bwana na yale yaliyo mema kwa kanisa. Kila kanisa lina uhuru wa kufanya yale wanayofikiria ndiyo mapenzi ya Mungu. Umoja wetu ni katika kufanya mapenzi ya Bwana pamoja.

5. Je, historia ya Wabatisti ni ipi?

Kumekuwa na makundi mengi ya Wakristo tangu wakati wa Agano Jipya. Baadhi ya makundi haya yanaamini na kufuata mafundisho ya Agano Jipya ambayo Wabatisti wanafundisha. Lakini kanisa la kwanza kutumia jina, "Batisti" lilikuwa huko Uholanzi (Holland) mwaka wa 1609. Washiriki wa kanisa hili walikuwa wakimbizi wa kidini kutoka Uingereza. Walienda Uholanzi kwa sababu huko kulikuwa na uhuru wa dini. Mwisho wa miaka ya 1500 na mwanzo wa 1600, kulikuwako na ufufuo huko Uingereza. Mfalme wa Uingereza alitenganisha kanisa la Kingereza na kanisa la Kikatoliki la Rumi. Baadhi ya washiriki walifikiri ya kwamba mabadiliko hayo hayakutosha. Walitaka kutumia Biblia peke yake kama mwongozo wao. Wengine hawakutaka kanisa na serikali kuwa kitu kimoja. Walitaka kusanyiko la kanisa lijitawale lenyewe. Wale ambao waliunda kanisa linaloitwa Batisti walitokana na makundi haya. Waliamini ya kwamba mwamini anaweza kuongozwa na Mungu. Neno la Mungu ndio mwongozo wa pekee, na wokovu ni kwa njia ya imani pekee. Walibatiza watu kwa njia ya kuwachovya au kuwazamisha majini. Kanisa liliongozwa na washiriki wenyewe. Waliamini kuhusu uhuru wa dini walikataa ubatizo wa watoto. Walimbatiza tena kila mwamini ambaye hakuwa amebatizwa kwa

kuzamishwa majini. Kwa sababu ya tendo hili, wale wengine wakawaita Wabatisti.

Askofu mkuu Lud wa kanisa la Uingereza alitaka kuwe na imani ya waamini katika nchi ya Uingereza. Alitaka kuwe na kanisa moja katika nchi hiyo, nalo ni kanisa la Uingereza. Alipinga uhuru wa kidini. Alitaka njia moja tu ya imani katika kanisa moja, yaani kanisa la Uingereza. Wabatisti na wengine waliotaka uhuru wa kidini walikimbilia Amerika.

Katika nchi ya Amerika, baada ya uhuru, asili ya uhuru wa kumwabudu Mungu ilianzishwa. Hati ya kanuni yenye haki na ya uwezo wa wananchi katika kuabudu ilipitishwa kuwa sehemu moja wapo ya katiba ya nchi ya Amerika. Wabatisti walisaidia kupitishwa kwa kanuni hii kwa sababu wao waliifundisha. Kanuni hii pamoja na sehemu yake yenye uhuru wa kumwabudu Mungu zilitia moyo katika kuanzishwa kwa mkataba wa mwungano wa mataifa (charter of the United Nations). Baadaye, katiba nyingi za nchi changa zilizoweza kujitawala ziliweza kufuata imani ya Wabatisti ya tangu hapo mwanzo.

Makanisa ya Kibatisti yaliyo katika eneo moja hufanya kazi pamoja katika jumuiya. Pia huweza kufanya kazi pamoja katika jumuiya ya taifa. Nazo jumuiya za kitaifa hufanya kazi na jumuiya za mataifa mengine ulimwenguni katika muungano wa Wabatisti katika ulimwengu (Baptist World Alliance or BWA). Hapo mwaka 1980 chama cha Wabatisti ulimwenguni kilikuwa na makundi ya Wabatisti kutoka nchi tofauti 115 kama wanachama. Kulikuwa na wabatisti zaidi ya milioni 30 katika makundi haya ulimwenguni. Kuna wabatisti zaidi ya milioni moja katika bara la Afrika. Hesabu ya wabatisti inaendelea kuongezeka kila wiki. Wabatisti wanapatikana karibu katika kila taifa la Afrika.

6. Je, tumejifunza nini kuhusu Wabatisti katika historia ya Wakristo?

1. Makanisa katika Agano Jipya yalifundisha ya kwamba Yesu ni Bwana na kwamba wokovu ni kwa imani tu. Walibatiza watu waliokuwa wameamini kwa kuwachovya ndani ya maji. Washiriki wa kanisa ni wale waliokuwa wamekomaa.

2. Baada ya Agano Jipya kuandikwa, mafundisho yafuatayo yenye kupotosha yalianzishwa:

Kuwa mshiriki wa kanisa kulikuwa na maana ya kuwa katika

ufalme wa Mungu.
Kubatizwa kulikuwa na maana ya kuwa Mkristo.
Kuwa kuhani (au mchungaji) kulikuwa na maana ya kuwa juu ya washiriki. Kufuata mashauri ya baraza la kanisa kulikuwa na maana ya kufuata mafundisho ya Agano Jipya.

3. Ni Agano Jipya tu linaloweza kuwa mwongozo wa Wakristo katika imani na matendo.

4. Wabatisti huamini ya kwamba umoja huja kwa uhusiano au ukoo mmoja wa kiroho katika Yesu Kristo na Wakristo wengine, wala siyo katika uhusiano au ukoo mmoja wa kimwili au utaratibu. Ni kwa hiari na sio kwa lazima.

5. Wabatisti tangu mwanzo wameendelea kuwa Wakristo wa Agano Jipya kwa kufuata mafundisho ya Agano Jipya.

## MSINGI WA IMANI YA JUMUIYA YA WABATISTI WA NEW ZEALAND

(1). Biblia ni kutokana na pumzi ya Mungu na mambo yote kuhusu imani na matendo yanapasa kuwa na msingi katika Biblia.

(2). Ubinadamu na Uungu wa kweli wa Bwana Yesu Kristo.

(3). Upatanisho wa Bwana msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote.

(4). Wokovu ni kwa imani katika Kristo pekee.

(5). Washiriki katika kanisa la Kikristo ni kwa wale waliozaliwa mara ya pili.

(6). Kuzamishwa majini kwa waamini ndio ubatizo wa kweli katika Biblia.

(7). Baada ya kukubaliana na masharti ya imani, kila kanisa ambalo limo katika jumuiya litakuwa na uhuru wa kutafsiri na kusimamia sheria za Kristo na kuongoza mambo yao wenyewe.

Huu ni mfano wa imani ya Wabatisti na shauku ya kutaka kufuata mafundisho ya Agano Jipya.

## MUHTASARI
## SOMO LA PILI

1. Mwanzo wa kanisa ni nini?
   A. Kanisa ni matokeo ya mapatano mapya.
   B. Kristo ndiye msingi wa kanisa.

2. Je, neno kanisa lina maana gani?
   A. Neno Kanisa, lilitumiwaje mara ya kwanza?
   B. Neno Kanisa limetumiwaje katika Agano Jipya?
   C. Neno Kanisa, lina maana gani kwa Wabatisti?

3. Yale Agano Jipya yanayozungumzia kuhusu Kanisa yanaonyesha Utatu Mtakatifu.
   A. Kanisa ni, "Watu wa Mungu."
   B. Kanisa ni, "Mwili wa Kristo."
   C. Kanisa ni, "ushirika wa Roho Mtakatifu."

4. Je, Kanisa ni mwili wa utaratibu na pia Mwili wa Kiroho?

5. Je, Kanisa limekua?

6. Je, tumejifunza nini kuhusu Kanisa la Agano Jipya?

# SURA YA PILI
# KANISA LA AGANO JIPYA

Wabatisti wanaamini ya kwamba kanisa la Agano Jipya ni lile ambalo huonyesha na kufuata mafundisho ya Agano Jipya. Mwanzo wa kanisa ulikuwa nini? Maana ya neno, kanisa, ni nini? Neno hili lilitumiwaje katika Agano Jipya? Wabatisti wanaamini nini juu ya neno hili? Asili ya matumizi ya neno hili yalionyeshwaje katika Agano Jipya? Kanisa huonyeshaje tabia ya Mungu? Tutajibu maswali haya katika sura hii.

Kanisa ni muhimu. Kristo alijitoa mwenyewe kulianzisha kanisa. Maana ya kanisa si jengo. Kanisa ni mwili wa waliokombolewa.

## 1. Mwanzo wa kanisa ni nini?

### A. Kanisa ni matokeo ya mapatano mapya.

Asili ya Ukristo inatokana na imani ya Waebrania. Waebrania waliishi chini ya Agano la Kale. Yeremia alizungumzia juu ya mapatano mapya ambayo Mungu angeandika ndani ya mioyo ya watu wake (Yeremia 31:31-34). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania aliandika juu ya Yesu akianzisha mapatano mapya. Kwa kutoa maisha yake pale msalabani, alimwaga damu yake ili iwe upatanisho mpya. "Na kwa sababu hii yeye ni mjumbe wa Agano Jipya, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya Agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele" (Waebrania 9:15).

### B. Kristo ndiye msingi wa kanisa.

Yesu alianzisha mapatano mapya. Kwa hivyo yeye ndiye msingi, jiwe la pembeni la kanisa. Paulo alisema, "maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo" (I Wakorintho 3:11). Petro anatwambia ya kwamba, "....Jiwe walilolikataa waashi, limekuwa jiwe kuu la pembeni" (I Petro 2:7). Yesu naye akizungumza na wanafunzi, aliwauliza kwamba yeye ni nani. Petro akamjibu ya kwamba, "Wewe ndiwe Kristo, mwana wa Mungu aliye hai" (Mathayo 16:16). Yesu akamjibu akasema, "....Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milangfo ya kuzimu haitalishinda" (Mathayo 16:18). Maneno haya Yesu aliyasema kuhusu yeye mwenyewe na kuhusu ukiri wa Petro. Kanisa limejengwa juu ya Yesu Kristo aliye mwamba imara.

## 2. JE, NENO KANISA LINA MAANA GANI?

### A. Neno Kanisa, lilitumiwaje mara ya kwanza?

Neno kanisa, katika lugha ya Kiyunani lina maana ya "watu walioitwa pamoja katika kusanyiko, kwa kufanya shughuli yao." Neno Kanisa limetumiwa katika kuelezea kusanyiko ama mkutano katika tafsiri ya Wayunani ya maandiko matakatifu ya Waebrania. Neno hili lilianza kutumiwa katika mji wa Athene. Ulikuwa mkutano wa watu au wananchi wa mji huo walio huru. Wale waliokuwa baraza kuu la mji huo. Kwetu sisi kanisa lina maana ya watu wanaoitwa pamoja katika kumwabudu na kumtumikia Mungu. Pia lina maana ya kwamba kanisa linahitaji kujitawala au kuwa na uhuru.

### B. Neno Kanisa limetumiwaje katika Agano Jipya?

Neno hili lina maana mbili katika Agano Jipya. Kwanza, lina maana ya mwili wa kiroho wa Wakristo wote. Hii ina maana Wakristo wa wakati wote na wa kila mahali. Watu wengine husema hii ina maana ya kusanyiko la Wakristo ulimwenguni kote. Kila mara ambapo neno hili kanisa huandikwa na herufi kubwa ya "K," lina maana hiyo. Lakini neno hili halitumiwi sana likiwa na maana hii. Pili, neno hili lina maana ya kanisa la mahali fulani. Makanisa haya ya mahali fulani yalikutanika katika nyumba za Wakristo. Sehemu tisini kwa mia (90%) na hata zaidi, neno hili kanisa lina maana ya kanisa la mahali fulani.

### C. Neno Kanisa, lina maana gani kwa Wabatisti?

Viongozi hamsini wa Kibatisti waliandika taarifa ya imani iliyoitwa Ujumbe na Imani ya Wabatisti. Nao walikuwa na haya ya kusema juu ya Kanisa:

> Kanisa la Agano Jipya la Bwana Yesu Kristo ni kusanyiko la waamini waliobatizwa na ni washiriki wa Kanisa la mahali fulani. Waamini hawa wanaunganishwa pamoja na Agano katika imani na ushirika wa injili. Kanisa hutunza maagano mawili yake Kristo, tena hufuata kamili mafundisho yake wakitumia vipawa vyao, haki na nafasi walizopewa na Neno lake Mungu. Tena hutafuta kueneza Habari Njema ulimwenguni kote.

Kanisa la mahali fulani liko huru katika mambo yake yote. Hufuata hatua za demokrasia chini ya ubwana wa Yesu Kristo. Hivyo basi, wote ambao ni washiriki wa Kanisa la mahali fulani, hujisimamia wenyewe katika mambo yao yote. Viongozi wake wa kiroho ni wachungaji na wazee wa Kanisa (mashemasi).

Agano Jipya linazungumzia juu ya Kanisa kama watu waliokombolewa zamani, sasa na hata siku zijazo.

## 3. YALE AGANO JIPYA YANAYOZUNGUMZIA KUHUSU KANISA YANAONYESHA UTATU MTAKATIFU.

Kuna maneno 35 kuhusu Kanisa katika Agano Jipya. Hapa tutazungumzia mambo matatu tu yanayoonyesha utatu mtakatifu. Haya yanaonyesha hali ya kiroho ya Kanisa. Na twaona hali hii ya kiroho katika Kanisa la mahali fulani.

### A. Kanisa ni, "Watu wa Mungu."

Petro alitaja maneno kutoka katika kitabu cha Kutoka 19 akionyesha ya kwamba Wakristo wa sasa ni watu wa Mungu. "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu" (I Petro 2:9). Hii inaonyesha Kanisa...watu walio na hali mpya na wenye madaraka makubwa. Pia inaonyesha hali ya Mungu anayepeana uhuru na madaraka kwa wale anaowaita kutoka gizani na kuingia nuruni.

### B. Kanisa ni, "Mwili wa Kristo."

Paulo aliandika katika Wakolosai 1:18, "Naye (Kristo) ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha Kanisa..." Kwa hivyo twazungumzia Kanisa kama mwili wa Kristo. Kanisa linaishi kwa sababu ya kazi ya Kristo Yesu aliyokwisha kuifanya. Kanisa ni mwili wa kiroho. Bila Kristo kama kichwa, Kanisa halingeweza kuishi wala kuwa na mwongozo. Kama mwili wa Kristo, Wakristo hutegemea Kristo na pia wenyewe kwa wenyewe.

### C. Kanisa ni, "ushirika wa Roho Mtakatifu."

Ushirika katika Agano Jipya una maana zaidi ya kunywa chai na wengine. Ushirika una maana ya mapatano ya watu wawili au zaidi kwa sababu ya kumfuata Yesu pamoja. Wakristo hutafuta kumtumikia na pia kumtukuza Mungu. Pia waamini hushirikiana na Roho Mtakatifu kwa sababu hii ni hamu yake kwao. Yesu alisema ya kwamba, "Yeye (Roho Mtakatifu) atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari" (Yohana 16:14). Kuwepo kwa Roho Mtakatifu ni lazima katika wokovu. Yeye hukaa na waamini na kuwapa uwezo wa utumishi na kutawala matendo yao. Yeye hufanya hivi ili kumtukuza Yesu kama Mwana wa Mungu.

## 4. JE, KANISA NI MWILI WA UTARATIBU NA PIA MWILI WA KIROHO?

Ndiyo, Kanisa linahitaji kufuata utaratibu. Katika Agano Jipya, utaratibu wa makanisa ulikuwa rahisi. Makanisa yalikuwa na utaratibu wa kutosha wa kufikia lengo la kuwa na wanafunzi. Walianza kuwatumia mashemasi ili kuratibisha kazi yao vyema. Pia katika utaratibu huo waliweza kutuma wamisheni walioitwa na Roho Mtakatifu. Hali ya kuwa na utaratibu ni nzuri sana. Na kumbuka ya kwamba huhitaij kuwa na utaratibu zaidi ya vile unahitaji kutimiza mapenzi ya Mungu. Mwili unahitaji kuwa na viungo.

Pia unahitaji uhai. Kwa mfano, ikiwa mwili hauna mifupa, huwezi kusimama au kutembea. Ikiwa mwili hauna kichwa, hauwezi kuishi. Ni lazima uwe na vyote. Ingawa hivyo, twahitaji kufikiria zaidi juu ya afya ya kiroho ya kanisa kuliko utaratibu wa kawaida wa kanisa.

## 5. JE, KANISA LIMEKUA?

Kanisa limekuwa kutokana na wanafunzi wachache hadi waamini milioni nyingi siku hizi. Hii ni kwa sababu ya uongozi wa Roho Mtakatifu na uwezo wake katika maisha ya waamini. Wakristo wanaporuhusu Roho Mtakatifu kutawala maisha yao, wanaweza kutumia maisha yao katika njia inayofaa na ya kufaulu. Lakini wanapojaribu kuongoza na kusimamia makanisa na Wakristo wengine, ushuhuda wao huwa hauna nguvu. Kuenea kwa injili katika kitabu cha Matendo kulikuwa kazi ya Roho Mtakatifu. Wale ambao walipokea injili siku ya Pentekoste walirudi nyumbani ili kushirikisha wengine kile walichopokea. Makanisa ya Antiokia na Rumi (Rome) yalianzishwa kwa njia hiyo. Waamini ni lazima wamruhusu Roho Mtakatifu awasaidie katika kupeleka injili kwa jamii zao.

## 6. JE, TUMEJIFUNZA NINI KUHUSU KANISA LA AGANO JIPYA?

1). Kanisa lilianzishwa na Mungu, linategemea Kristo na linapata uwezo kutoka kwa Roho Mtakatifu.

2). Kanisa ni kwa wote ambao kwa imani yao wamemtolea Mungu maisha yao ayatawale.

3). Kanisa lina nguvu zaidi kwa sababu lina umoja na viungo tofauti.

4). Ni wajibu wa kanisa kushirikisha injili ya Yesu Kristo kwa watu wengine.

5). Kanisa la mahali fulani ni ufunuo wa mwili wa Kristo katika jamii ambapo kila Mkristo ni vyema kuwa mshiriki.

## MUHTASARI
## SOMO LA TATU

1. Je, jamii inahitaji Kanisa la aina gani?
   A. Kanisa lililo na washiriki ambao wameokolewa.
   B. Kanisa lililo na huduma kama ile ya Yesu.
   C. Kanisa lililo na uwezo wa kiroho.

2. Je, kusudi la Kanisa ni nini?
   A. Kusudi la Yesu
   B. Amri ya Yesu: fanya mataifa kuwa wanafunzi wangu.
   C. Mitume: watu waliofuata amri ya Yesu.

3. Je, huduma ya Uinjilisti ni nini?
   A. Maana ya Uinjilisti.
   B. Hakikisho la Uinjilisti.
   C. Kanuni za Uinjilisti.

4. Je, huduma ya kukuza kiroho ni gani?
   A. Maana ya huduma ya kukuza kiroho.
   B. Njia ama ndimi za huduma ya kukuza kiroho.
   C. Kanuni za kukuza kiroho.

5. Je, ni vyema Kanisa kupima huduma yake?

6. Je, tumejifunza nini juu ya kusudi la Kanisa?

# SURA YA TATU

## KUSUDI LA KANISA

Jamii inahitaji Kanisa la aina gani? Kusudi la Kanisa la mahali fulani ni nini? Huduma ya kukuza kiroho au kuwatia nguvu wengine katika imani ni gani? Je, Kanisa laweza kupima huduma yake?

Kanisa la mahali fulani lina kusudi ambalo walipewa na Kristo, la kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wa Yesu. Jamii inahitaji Kanisa ambalo linaamini kusudi lake ni la muhimu.

### 1. JE, JAMII INAHITAJI KANISA LA AINA GANI?

A. Kanisa lililo na washiriki ambao wameokolewa.
Jamii ina watu wengi ambao hawajaamini. Kwa hivyo, kila jamii inahitaji Kanisa lililo na washiriki ambao wameokolewa. Kanisa, kama watu wa Mungu, linahitaji kuhimiza ya kwamba, mtu ni lazima aokolewe kwanza kabla ya kuwa mshiriki. Kanisa linahitaji kuwa mfano wa mabadiliko yanayofanyika wakati mtu amempokea Yesu kama mwokozi wake.

B. Kanisa lililo na huduma kama ile ya Yesu.
Kanisa, kama mwili wa Kristo, linahitaji kutumikia jamii kama Yesu alivyofanya. Kama mwili, Kanisa ni watu wa kutumika. Kanisa lahitaji kutafuta njia za kutumika katika jina la Yesu Kristo. Ikiwa Kanisa litasaidia jamii, sharti lisaidie na litende zaidi ya vile washiriki wangetenda kwa nguvu zao wenyewe. Ni lazima Kanisa likuballi uongozi na nguvu za Roho Mtakatifu katika utumishi wake.

C. Kanisa lililo na uwezo wa kiroho.
Kanisa ni ushirika ulio na uwezo wa Mungu. Kanisa lililo na uwezo wa kiroho, ni Kanisa ambalo linatawaliwa na Kristo kwa kupitia Roho wake Mtakatifu. Washiriki wa Kanisa ni wajumbe wa wokovu katika jamii. Kristo huwatumia ili kudhihirisha nguvu za Mungu katika maisha ya watu wengine.

### 2. JE, KUSUDI LA KANISA NI NINI?

Kusudi la Kanisa ni sawa na kusudi la Yesu. Maisha, huduma na amri zake, zinaonyesha kusudi lake. Mitume ni mfano bora wa watu waliofuata amri na maagizo yake Yesu.

A. Kusudi la Yesu.

Yesu ni Mwana wa Mungu. Alifanyika kuwa mwanadamu ili watu waweze kuwa na uzima wa milele. Alikuja ulimwenguni ili aanzishe Agano Jipya. Yesu ni ufunuo kamili wa Mungu aliye mbinguni. Mtu atakapouliza, Mungi ni kama nani, anahitaji kuangalia Yesu na matendo yake. Yesu hutuonyesha hali ya Baba wetu wa mbinguni. Filipo naye akitaka kujua akamuuliza Yesu, "Bwana, tuonyeshe Baba" Yesu akamjibu, "Aliyeniona mimi amemuona Baba...mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu..." (Yohana 14:8-11). Yesu ni njia ya ukombozi. Binadamu walikuwa watumwa wa dhambi na mauti. Kwa imani katika Yesu, waamini wamekuwa huru. Yesu alilipa deni ya dhambi ili mwanadamu aweze kuwa huru. Kwa hivyo Wakristo wanahitaji kuonyesha upendo wa Mungu kwa wengine kama vile alivyowafanyia.

B. Amri ya Yesu: fanya mataifa kuwa wanafunzi wangu.

Katika Mathayo 28:19-20, Yesu aliwaamuru Wakristo kufanya mataifa kuwa wanafunzi wake. Kazi hii hufanywa kwa njia mbili, uinjilisti na kukuza kiroho. Katika uinjilisti, Wakristo wanatoa ushuhuda wao, wa kazi iliyofanywa na Yesu katika maisha yao. Kukuza kiroho kuna maana ya "kutia nguvu au kujenga mtu katika imani." Katika kukuza kiroho, Wakristo wanafundisha au kumwongoza mwamini mpya. Wanamsaidia kukua na kukomaa katika imani. Uinjilisti unatangulia kukuza kiroho. Walakini, uinjilisti hauwezi kukamilika mpaka mwamini amekuwa mfuasi mwema. Mfuasi mwema anaweza kumwongoza mwingine kuwa Mkristo na kumfundisha jinsi ya kuwa mwanafunzi wa Yesu.

C. Mitume: watu waliofuata amri ya Yesu.

Kitabu cha Matendo ya Mitume ni kitabu ambacho hustaajabisha sana. Mitume walikuwa watu wa kawaida. Walikuwa na taabu. Walijaribiwa. Wakati Yesu alipokufa, walitawanyika. Walakini, katika kitabu cha Matendo, Roho Mtakatifu, hapo siku ya Pentekoste, aliwapa nguvu. Mitume walikuwa mashahidi wa kweli. Twasoma vile walianzisha makanisa na kuongoza watu wa Yesu. Vitabu vingi vilivyokifuata kitabu cha Matendo ya Mitume vina waraka (barua) kwa makanisa mengine. Makanisa haya yalitaka kufanya kazi ya Yesu.

3. JE, HUDUMA YA UINJILISTI NI NINI?

A. Maana ya Uinjilisti.

Uinjilisti una maana ya "kuwaambia wengine habari za Yesu Kristo." Uinjilisti unawasaidia wengine kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Uinjilisti ni kazi ya Wakristo wote. Mkristo

binafsi pamoja na kundi la Wakristo kama Kanisa wana wajibu huu. Wanahitaji kuwapa wasiojua Yesu habari za wokovu. Mkristo anaweza kushirikisha injili kwa njia nyingi. Anaweza kuzungumza na wengine kuhusu vile Yesu amemfanyia katika maisha yake. Pia anaweza kuhubiri. Anaweza kuzungumzana na watu kuhusu Yesu ni nani. Pia anaweza kuwa na majadiliano juu ya maana ya imani ya Kikristo.

B. Hakikisho la Uinjilisti.

Maisha ya shahidi yanahitaji kuonyesha ya kwamba amebadilishwa. Ikiwa hayaonyeshi mabadiliko, shahidi anaweza kuzuia wengine kumpokea Kristo. Mchungaji mmoja alikuwa na shida na mwanamke mmoja kanisani. Mwanamke huyu aliishi na zaidi ya mwanaume mmoja. Na yule aliyeishi naye wakati huo, hakuwa baba wa mtoto aliyekuwa naye. Tena hakukuwa na ndoa ya kiutamaduni (asili) wala ya kikristo. Na katikati ya mambo hayo, mwanamke huyu alitaka kutoa ushuhuda wake jinsi alivyookolewa, mbele ya kanisa. Mchungaji alikataa kumruhusu atoe ushuhuda wake. Naye mama huyo akakasirika sana. Je, ikiwa ulikuwa mchungaji wake, ungefanya nini?

Kila sehemu ya maisha ya Mkristo inahitaji kuonyesha ya kwamba imebadilishwa. Ni lazima kuonyesha katika shughuli ya biashara, jamaa, jamii na hata kanisani. Maisha ya Wakristo yanahitaji kuonyesha upendo, uaminifu, na umoja katika imani yao kwake Yesu Kristo.

C. Kanuni za Uinjilisti.

1). Kanisa lina wajibu wa kushirikisha injili katika jamii.

2). Matendo na moyo wa kanisa unaweza kusaidia au kuzuia ushuhuda wa mshiriki.

3). Kazi ya uinjilisti inahitaji kufanywa katika jamii kuliko kanisani.

4). Kanisa linahitaji kutambua wenye wito na vipawa vya kazi ya uinjilisti.

5). Waamini wapya wanahitaji kuingizwa katika shughuli za kanisa mara moja.

## 4. JE, HUDUMA YA KUKUZA KIROHO NI GANI?

A. Maana ya huduma ya kukuza kiroho.

Kukuza kiroho kuna maana ya "kufundisha, kuelimisha, kujenga na kutia nguvu." Huduma ni kwa wale ambao ni waamini. Huduma hii ina lengo kwa kanisa; lakini uinjilisti una lengo kwa wale wasio Wakristo. Makanisa, kama kila Mkristo, yanahitaji kukua katika imani.

B. Njia ama ndimi za huduma ya kukuza kiroho.

Kanisa linaweza kutumia njia nyingi kuwakuza washiriki katika imani. Ibada ni muhimu sana. Ibada inahitaji kupangwa na kufuata utaratibu. Ibada inahitaji iwe na kuimba, kuomba, kutoa sadaka, kushuhudia, kusoma na kulihubiri Neno la Mungu. Walakini, ushuhuda unahitaji kuwa juu ya mambo yale ambayo Kristo amefanya hivi karibuni katika maisha ya shahidi. Ingawa urefu wa ibada unahitaji kulindwa, mambo yote yanahitaji kufanywa. Kiongozi anahitaji kuzuia mtu mmoja au kundi fulani kutotumia wakati wote wa ibada. Kwa mfano, kwaya isiruhusiwe kuimba nyimbo nyingi hata kutumia nafasi ya mtu mwingine. Kiongozi wa ibada au mchungaji ana wajibu wa kuongoza ibada kwa njia ambayo watu hawatazuiliwa kumwabudu Mungu. Kiongozi anahitaji kufikiria juu ya kundi lote, na wala si mtu mmoja na mapenzi yake.

Ikiwa Kanisa litaendelea kukua katika imani, linahitaji kuwa na mpango wa mafundisho. Mpango huu si kwa watoto tu. Ikiwa Kanisa litafaulu katika kufundisha watu wazima, watoto wataweza kujifunza pia. Mchungaji anahitaji kufundisha wengine kufundisha. Pia anahitaji kuwa mtu mwenye kujifunza. Kanisa litaweza kukua kulingana na uwezo wa viongozi wake.

C. Kanuni za kukuza kiroho.

(1). Kila Mkristo anahitaji kujifunza Neno la Mungu na kulidhihirisha maishani mwake.

(2). Kila Mkristo anahitaji kutambua na kuendeleza karama yake au zake za kiroho.

(3). Kila kanisa linahitaji kutoa nafasi kwa washiriki kuwa na ibada ya maana.

(4). Kanisa linahitaji kutayarisha washiriki wake kwa kazi ya Mungu.

5. JE, NI VYEMA KANISA KUPIMA HUDUMA YAKE?

Huduma ya Kanisa inaweza kupimwa? Je, inahitaji kupimwa? Ndiyo, kanisa linahitaji kupima na kuchunguza huduma yake. Kufanya hivi kanisa linahitaji kujiuliza maswali mawili muhimu. Je, tunawavuta watu katika jamii kuja kwake Yesu? Je, tunawasaidia Wakristo wapya kukua katika imani? Ikiwa jibu moja au yote ni la, kanisa linahitaji kuomba na kutafuta uongozi wa Mungu na uwezo wake ili liwe kanisa linalotakiwa kuwa.

## 6. JE, TUMEJIFUNZA NINI JUU YA KUSUDI LA KANISA?

1). Kila jamii inahitaji kanisa lililo na washiriki waliookolewa, lililo na huduma kama ile ya Yesu, na lililo na uwezo wa kiroho.

2). Kusudi la kanisa, katika uongozi na uwezo wa Roho Mtakatifu, ni kutimiza amri ya Yesu kufanya mataifa kuwa wanafunzi wake.

3). Uinjilisti una maana ya kuwaambia wengine habari ya Yesu. Na kila Mkristo ana wajibu katika uinjilisti.

4). Kukuza kiroho kuna maana ya kusaidia Wakristo kukua katika imani. Huu ni wajibu wa kanisa na Wakristo waliokua kiroho.

5). Kanisa linahitaji kupima na kuchunguza huduma yake kila wakati.

## MUHTASARI
## SOMO LA NNE

1. Ni imani gani inayotofautisha ukristo na dini zingine?
   A. Mungu kufanyika mwili na upatanisho uliopatikana kwa kifo cha Yesu msalabani.
   B. Wokovu ni katika Yesu Kristo peke yake.
   C. Maandiko matakatifu.

2. Ni imani gani inayowatofautisha Wabatisti na Wakatoliki?
   A. Maandiko matakatifu ndiyo amri ya mwisho kwa mwamini (Biblia).
   B. Kuhesabiwa haki kwa njia ya imani.
   C. Ukuhani wa mwamini.


3. Ni imani gani inayowatofautisha Wabatisti na madhehebu mengine?
   A. Ubwana wa Yesu Kristo.
   B. Imani.
   C. Ubatizo.

4. Tumejifunza nini kuhusu msingi wa imani ya Wabatisti?

# SURA YA NNE

## MSINGI WA IMANI YA WABATISTI

Siku hizi kuna madhehebu mengi ya kikristo. Yale kundi fulani hutenda ndiyo huamini. Wabatisti huamini mambo mengi ambayo madhehebu mengine pia huamini. Ingawa hivyo, madhehebu hayo hawafuati na kutenda sawa kabisa kama jinsi tunavyofanya. Hapa tutaangalia imani na matendo yanayowafanya Wabatisti wawe tofauti na dini zingine kama Wakatoliki na madhehebu mengine yasiokubali baadhi ya mafundisho ya Kanisa la Kirumi (Protestanti).




1. Ni imani gani inayotofautisha ukristo na dini zingine?

A. Mungu kufanyika mwili na upatanisho uliopatikana kwa kifo cha Yesu msalabani

Utu wa Yesu na upatanisho wa kifo chake ni imani muhimu kwa Wakristo. Fundisho hili haliwezi kutenganishwa wala kugawanywa. Upatanisho wa mtu na Mungu uliweza kufanywa tu kwa njia ya kifo cha Yesu Kristo msalabani. Kwa sababu ya ubinadamu (utu) wa Yesu Kristo, dhabihu ile ya kufa kwake msalabani huleta maana kamili katika imani ya waamini. Bila upatanisho na ondoleo la dhambi, ubinadamu wa Yesu ungekuwa bila maana.

1) Utu maana yake ni kwamba, Mungu alifanyika kuwa mwanadamu.

Dini nyingi za ulimwengu kama dini ya Kiislamu, Kiyahudi, kihindu na kadhalika humheshimu Yesu. Wao husema ya kwamba Yesu alikuwa mwalimu mwema, mtu mtakatifu au nabii. Ingawa hivyo, Wakristo wanaamini ya kwamba Yesu alikuwa Mungu na pia mwanadamu. Mungu, kwa upendo wake, alichagua njia hii ili amlete

mwanadamu kwake kwa sababu mwanadamu alikuwa ametenganishwa na Mungu. Damu ya mbuzi na ng'ombe haikuwa na nguvu ya kutosha kumsafisha mwanadamu kutokana na dhambi zake. Kwa hivyo Mungu akafanyika kuwa mwili katika kuzaliwa kwa Yesu. Yesu akazaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hili ni fundisho ambalo watu wa dini zingine hawakubali. Ili mtu awe Mkristo, anapaswa kuamini fundisho hili la ubinadamu wa Yesu. Makanisa yote yanayoitwa ya kikristo yanaamini ukweli huu. Yohana anamwita Yesu Neno. "Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14).

2) Upatanisho ni kazi ambayo Yesu alifanya ili kumrejesha mwanadamu katika ushirika na Mungu.

Kila mtu ni mwenye dhambi. Dhambi zako zimekutenga mbali na Mungu. Mtu hawezi kufanya kitu cho chote ili aondoe dhambi zake. "Haiwezekani kamwe kwamba damu ya ng'ombe dume na mbuzi iweze kuondoa dhambi" (Waebrania 10:4). Kwa sababu ya Yesu kuwa mwili, dhabihu yake ilikuwa kamilifu na yenye nguvu." Damu ya Yesu Mwana wake yatusafisha dhambi zote (Yohana 1:7b). Hii ndiyo kazi ya upatanisho ambayo Kristo alifanya kwa mwenye dhambi. Mwamini humkubali Yesu kuwa Bwana wake. Nayo damu ya Yesu husafisha dhambi za mtu huyo. Yesu basi ni kuhani mkuu wa mtu huyo huko mbinguni. Yesu hujua na kutunza shida za watoto wake kwa sababu alikuwa Mungu na mwanadamu.

B. Wokovu ni katika Yesu Kristo peke yake.

Kufuatana na Biblia, kuna njia moja tu ya wokovu. Wokovu huja kwa imani katika Kristo Yesu. Kila mtu ni lazima atubu dhambi zake na kumwamini Yesu. Wakristo huamini yale Yesu aliyosema ya kwamba, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6). Katika Matendo 4:12, Petero alisema, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Wokovu ni katika Yesu Kristo pekee. Alifanya upatanisho wa dhambi kwa njia ya kifo na ufufuo wake. Watu wa dini zingine wanaamini ya kwamba wanaweza kuokolewa kwa njia nyingine. Wakristo nao wanaamini ya kwamba wokovu ni kwa njia ya imani katika Kristo Yesu peke yake.

C. Maandiko matakatifu.

Wakristo hupokea vitabu 66 vya Biblia kuwa Neno la Mungu. Maandiko hayo hutofautisha Wakristo na Wayahudi ambao

hawapokei Agano Jipya. Huwatofautisha pia na Waislamu ambao hufuata na kuamini Korani. Wahindi nao wana maandiko wanayoamini kuwa ni matakatifu. Dini za kienyeji nyingi hufuata desturi badala ya maandiko yo yote.

2. Ni imani gani inayowatofautisha Wabatisti na Wakatoliki?

Kuna mafundisho matatu ya imani yenye umuhimu katika Agano Jipya. Mafundisho hayo ya imani ni yale ambayo watu wale wa matengezo walitaka Kanisa la Kikatoliki kukubali. Walitaka kurudi katika kanuni za Agano Jipya.

A. Maandiko matakatifu ndiyo amri ya mwisho kwa mwamini (Biblia).

Kanisa wakati wa matengenezo lilikuwa na desturi zingine zisizokuwa za Biblia. Desturi hizi zikaleta shida, kwa sababu iliaminika ya kwamba baraza la kanisa lilikata mashauri ambayo yalifikiriwa kuwa na uwezo sawa na Biblia. Kama vile mashauri mema mengi ya kanisa yalivyokubaliwa, pia makosa yalikuwemo vile vile. Wabatisti pamoja na madhehebu mengine hukubali maandiko matakatifu pekee kuwa ndiyo amri ya mwisho.

Wabatisti hawaamini kwamba neno lo lote la mtu ye yote au kundi lo lote linaweza kuwa sawa na Biblia. Mashauri na maelezo yote au desturi lazima yakubaliane na Biblia. La sivyo, yasifuatwe wala kukubaliwa. Watu wengine wanataka kutumia maneno yao au vitabu vyao eti viwe sawa na maandiko matakatifu, Neno la Mungu. Wengine wanatumia nia zao na jinsi wanavyoweza kuwasaidia watu kulielewa Neno la Mungu, lakini hakuna kitabu kingine cho chote, ambacho kinaweza kuwa sawa na neno takatifu la Mungu. Amri ya mwisho lazima iwe Neno la Mungu.

Wakati ambapo mtu analifafanua Neno la Mungu, hufanya hivyo kama mwamini katika Yesu Kristo. Imani yake ndani ya Yesu na ufahamu wake katika Agano Jipya humsaidia kufafanua na kufahamu Agano la Kale. Maandiko matakatifu, ambayo ndiyo amri ya mwisho ya mwamini huwasaidia watu kufahamu ujuzi wao na jinsi wanavyojisikia ndani ya maisha yao.

B. Kuhesabiwa haki kwa njia ya imani.

Wakati wa matengezo, kanisa lilikuwa likifundisha kwamba wokovu hupatikana kwa kuyatenda mambo fulani. Hiyo ilikuwa shida ya Martin Luther na wahubiri wengine. Luther akawasaidia wengine kuelewa maelezo ya Paulo, ".....tunahesabiwa haki kwa imani...." (Warumi 5:1). Kuhesabiwa haki maana yake ni kufanywa haki. Wabatisti huamini ya kwamba mtu anaweza kufanywa haki

mbele ya Mungu kwa njia ya imani. Kwa sababu ya imani ya mwamini, Mungu humtangaza kuwa mwenye haki. Mtu ni mwenye dhambi kwa asili yake. Hawezi kujiokoa mwenyewe. Ni lazima abadilishwe. Mungu anaweza kumbadilisha mtu kwa sababu ya imani yake katika Yesu. Kwa hivyo, wokovu humtegemea Mungu, wala siyo mtu.

Mwamini huwa salama katika wokovu wake. Hii ni kwa sababu ya tabia na asili ya Mungu. Wokovu humtegemea Mungu kwa kuokoa na pia kumlinda mwamini. Mwanadamu hawezi kujiokoa na hana nguvu kama za Mungu. Wokovu daima ni kazi ya neema ya Mungu katika imani ya mwamini ndani ya Yesu Kristo.

C. Ukuhani wa mwamini.


Wakristo wote ni makuhani mbele ya Mungu. Wanaweza kuomba moja kwa moja kwa Mungu kwa ajili yao wenyewe na pia kwa ajili ya watu wengine. Tofauti kati ya viongozi na washiriki ilimalizika wakati Yesu alipokufa pale msalabani, na hapo fundisho hilo likapoteza maana katika Agano Jipya. Washiriki wa kanisa waliitwa watu wa kawaida au "Laity." Neno hili ni neno la Kiyunani lililo na maana ya "watu." Makuhani wakaitwa watu wenye cheo cha "Clergy." Maana ya neno hili la Kiyunani ni "mwito katika maisha." Hata hivyo maneno hayo mawili yana maana ya Wakristo WOTE katika Agano Jipya. Wakristo WOTE ni watu wa Mungu, na wameitwa katika utumishi wake. Katika mwili wa kiroho wa Kristo, hakuna migawanyiko. Mchungaji anaheshimiwa kwa sababu ya hekima yake na kukua kwake katika imani. Hata hivyo yeye si bora kuliko waamini wengine. Yeye si njia ya wenzake kumfikia Mungu. Yeye si mtu wa pekee tu ambaye Mungu husema naye na kumsikia. Wakristo WOTE wanaweza kuomba, kutumika, kukua katika imani, kujifunza, kushuhudia na kutoa mali zao. Mungu anawataka watu wake WOTE kumjua na kusema naye na kuyafanya mapenzi yake.

Wabatisti huamini fundisho hili kwa nguvu sana. Mtu anaweza, kwa kuongozwa na Mungu, kukata mashauri yake mazuri katika maisha yake ya kiroho. Kila Mkristo ni kuhani. Ukuhani ni wa Wakristo wote; kwa hivyo, Wakristo wote ni washiriki katika ukuhani. Ukuhani sio kwa kundi dogo la watu wachache tu maalum. Ila ni kwa Wakristo wote.

3) Ni imani gani inayowatofautisha Wabatisti na madhehebu mengine?

Huko Uingereza kuna chuo cha Wabatisti kinachoitwa Regents Park College. Katika chuo hicho, kuna mfano unaoeleza

kuhusu mambo makuu ya imani ya Wabatisti. Mfano wenyewe ulikuwa wa aina ya pekee. Mafundisho yake yameonyeshwa kwa mfano wa mkono.




A. Ubwana wa Yesu Kristo.

Agano Jipya hufundisha kuhusu ubwana wa Yesu Kristo (Warumi 10:9; Wafilipi 2:9-11). Huu ndio msingi wa imani na kanuni ya Wabatisti. Yesu ndiye anayeokoa. Roho wake huwapa watu uwezo. Kazi zote za mtu ni bure ikiwa Yesu si Bwana wake. Ni lazima Yesu awe Bwana katika sehemu zote za maisha. Ni lazima amwongoze mwamini. Roho wake huongoza katika ukweli wote na hekima yote. Kama mtu akitembea katika imani, Bwana humwezesha kujua mapenzi yake. Mwamini huwa na uwezo wa kutambua mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo haya yafuatayo kuhusu Yesu:

1) Yesu ni Mwana wa Mungu (Yohana 4:14-15).

2) Kujitolea kwa Yesu kunatosha kwa wokovu wa kila mwamini (Warumi 5).

3) Yesu ni njia pekee ya wokovu (Matendo 1:12).

4) Kanuni na imani zote ni lazima zifuate mafundisho yaliyoandikwa katika Agano Jipya (I Timotheo 6:3; I Wathesalonike 4:1-2; Ufunuo 1:2).

B. Imani

Agano Jipya hufundisha kuhusu ujuzi wa wokovu wa mtu binafsi katika neema kwa njia ya imani. Waefeso 2:8 hufundisha pia kuhusu kufanywa haki kwa njia ya imani. Tunafanywa kuwa wenye haki mbele za Mungu katika njia ya imani ndani ya Yesu kama Bwana. Hii ni imani ya mtu binafsi. Kila mtu ni lazima aungame hali yake ya dhambi na aseme waziwazi mbele ya watu wengine kwamba Yesu ni Bwana wake. Mtu hawi Mkristo kwa bahati tu au kwa ajali. Ni lazima afanye hivyo kwa kupenda kwake na kwa

uchaguzi wake mwenyewe mbele ya watu. Huwa Mkristo tu kwa njia ya imani. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo haya yafuatayo kuhusu wokovu kwa imani.

1) Mtu huwa mwamini na kuokolewa tu kwa imani (Warumi 3:22-28; 5:1).

2) Mtu huokolewa kwa neema ya Mungu (Waefeso 1:7; 2:8).

(a) Wokovu huanza kwa Mungu siyo mwanadamu (Yohana 6:65; Mathayo 16:17).

(b) Wokovu ni salama kwa sababu humtegemea Mungu daima (Waefeso 1:13-14; Tito 3:7; I Petero 1:5).

3) Mwamini hupokea Roho Mtakatifu anapookoka (Waefeso 1:3; Warumi 8:9).

4) Ni mtu aliyeokoka pekee anayestahili kuwa mshiriki wa kanisa (Matendo 2:41-47).

C. Ubatizo.

Makanisa ya Agano Jipya yaliwabatiza waamini kwa njia ya kuchovya ndani ya maji (Matendo 2:41; 8:38; 10:47). Wabatisti hufuata sana mikazo ya maandiko hayo kuhusu ubatizo. Wabatisti huwabatiza wote waliofanya ukiri wao waziwazi kuwa Yesu ni Bwana. Huwabatiza kwa kuwazamisha au kuwachovya ndani ya maji. Tumesoma habari ya ubatizo katika sura ya kwanza, na tutapata zaidi katika sura ya tano. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo haya yafuatayo kuhusu ubatizo.

1) Ubatizo wa Agano Jipya ni kwa kuzamisha au kuchovya (Matendo 8:38; Warumi 6:3-4).

(a) Kubatiza ni kumdidimiza mtu kabisa ndani ya maji mengi yaani kuchovya au kuzamisha.

(b) Ni kuzamisha tu kunakoonyesha kufa, kuzikwa na kufufuka kwa mtu ndani ya Yesu.

2) Ubatizo wa Agano Jipya ni kwa mwamini tu (Matendo 10:47).

(a) Ubatizo ni kitendo cha utii wa mwamini kwa Bwana Yesu.

(b) Ubatizo si tendo la wokovu (Waefeso 2:8-9).

3) Ubatizo wa Agano Jipya wa mwamini kwa Bwana Yesu ni muhimu kwa ushirika wa kanisa (Mathayo 28:19; Matendo 2:41).

4) Mamlaka ya kubatiza ni ya kanisa, si ya mchungaji (Tazama sura ya saba).

D. Ushirika

Agano Jipya hufundisha ya kwamba kanisa ni ushirika wa kiroho. Kanisa la Kibatisti ni kundi au kusanyiko la waamini waliobatizwa (Matendo 2:41; Warumi 16:5; I Wakorintho 1:2). Tulizungumza kuhusu Kanisa la Agano Jipya katika sura ya pili na kusudi la kanisa katika sura ya tatu. Kanisa ni ushirika wa watu wa Mungu. Kanisa ni mwili wa Yesu ukifanya kazi kwa kusudi lake. Kanisa ni ushirika wa Roho Mtakatifu ukimtukuza Mungu. Ushirika ni tokeo la kumfuata Yesu. Washiriki wa Kibatisti lazima wawe wamemkiri Yesu kama Bwana wao na kubatizwa. Mkristo ni afadhali ajiunge na kundi ambalo linaamini kama vile anavyoamini. Sio ukristo kuingia kanisa ili kulibadilisha kutoka kwa dhehebu lake na kulifanya liwe lingine. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo yafuatayo kuhusu kanisa:

1) Kanisa ni kundi la watu wa mahali fulani waliobatizwa baada ya kuamini na ni washiriki wa kundi hilo (Matendo 2:41, 47; 20:17).

2) Kama mwili wa kiroho, kanisa ni ushirika wa Wakristo walio na usawa mbele ya Mungu (I Wakorintho 12:14-20; Warumi 12:3-6).

3) Kanisa linapaswa kumtukuza Kristo katika ibada zake na mikutano yake (Yohana 16:14; Matendo 2:42-47).

4) Ushirika wa waamini huhitaji vipawa vya kiroho vya kila mshiriki (I Wakorintho 12:7).

5) Ushirika chini ya Bwana huwa na wajibu kwa wanachama wake (I Wakorintho 5:5; 2 Wathesalonike 3:6).

E. Uhuru.

Agano Jipya hufundisha ya kwamba kuna uhuru ulio na wajibu katika Yesu Kristo (Yohana 8:36; Luka 12:47-48; Warumi 6:17-18). Uhuru huleta wajibu kila mara. Mtu hawi na uhuru wa kufanya kama apendavyo tu. Kama wangefanya hivyo, basi hapangekuwa na utaratibu na utulivu kanisani. Wabatisti huamini ya kwamba mtu ana uhuru wa kumkubali au kumkataa Yesu. Mungu amempa mtu uhuru wa kuchagua. Ni lazima atumie uhuru huo kwa hekima. Kanuni ya ukuhani wa waamini hufundisha ukweli huu. Makanisa ya Kibatisti hufuata fundisho hili. Washiriki chini ya uongozi wa Kristo wako huru kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu kwa kanisa lao. Makanisa ya Kibatisti hufanya kazi pamoja kwa njia za jumuiya ndogo (yaani eneo la makanisa ya sehemu

ndogo kama wilaya), jumuiya kuu (yaani eneo la makanisa ya sehemu kubwa kama nchi) na vyama vingine. Washiriki wa makundi hayo pia wamo katika uongozi wa Yesu Kristo. Wana uhuru wa kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu kwa kundi lao. Ingawa ni hivyo, kundi moja halina uhuru wa kukatia kundi lingine shauri kuhusu mapenzi ya Mungu kwa kundi hilo. Wanaweza kuomba ama kuuliza kundi fulani kufanya kitu fulani. Lakini haliwezi kulazimisha kundi fulani kufanya kitu ambacho hawataki kufanya. Wabatisti wanaheshimu uhuru wa wengine. Huamini ya kwamba, wengine ni lazima wapokee wajibu wa matendo yao. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo yafuatayo kuhusu uhuru:

1) Mungu amempa kila mtu uhuru wa kuchagua (Yoshua 24:15).
2) Uhuru daima huhitaji wajibu (Warumi 6:22-23; I Petro 2:16; Luka 12:47-48).
3) Uhusiano wote wa kanisa uchaguliwe kwa hiari (I Wakorintho 16:16; Waefeso 5:12; I Petro 2:13).
4) Roho Mtakatifu anaweza kumwongoza kila Mkristo katika imani (Warumi 8:14-17).

F. Uinjilisti.

Agano Jipya hufundisha hitaji la kuwashirikisha wasio Wakristo injili (Matendo 1:8). Wabatisti wanawafikiria wale ambao hawajamjua Kristo kama mwokozi wao. Wanaamini ya kwamba kila Mkristo ana wajibu wa kuwa mwinjilisti. Roho Mtakatifu huwapa waamini uwezo na ushujaa wa kuwa mashahidi wa Yesu.

Wabatisti wanaamini katika umisheni. Umisheni maana yake ni kwenda au kumtuma mtu kuwapelekea injili wale watu ambao hawajaokolewa. Wabatisti huanzisha vituo vipya na ushirika ili watu waweze kumjua Yesu. Wanataka kushirikiana baraka, furaha na upendo waliopata katika Yesu. Wakristo wana wajibu wa kuwatuma wamisheni. Wanaweza kufanya mpango wa kushirikiana katika makanisa, jumuiya ndogo na jumuiya kuu kwa kufanya kazi hiyo ya uinjilisti. Kila kanisa linaweza kushiriki katika kazi hii kwa kutoa fedha zao kwa jumuiya dogo na jumuiya kuu. Makundi haya yanaweza kuwatuma wamisheni katika sehemu ambazo hakuna makanisa. Wabatisti huhubiri na kufundisha mambo yafuatayo kuhusu uinjilisti.

1) Kila mwamini ni mwinjilisti na shahidi wa Yesu (Matendo 1:8; Yohana 5:10-12).

2) Roho Mtakatifu hutupa ushujaa katika kushuhudia (Matendo 4:3, 31).

3) Kanisa lina wajibu wa kuwaambia watu wa jamii yake kuhusu Yesu (Matendo 19:10).

4) Kanisa lina wajibu wa umisheni katika jamii nyingine (Matendo 13:1-4; 3 Yohana 6-8).

4. Tumejifunza nini kuhusu msingi wa imani ya Wabatisti?

1) Yesu alikuwa Mungu na wokovu ni kwa njia ya imani
2) Biblia ni kiongozi katika imani na matendo ya mwamini.
3) Ubatizo wa waamini kwa kuchovya ndio wa kibiblia.
4) Washiriki wa Kanisa ni lazima wawe na usawa na udugu.
5) Mungu humpa kila mtu uhuru na wajibu.
6) Wakristo wote wana wajibu wa umisheni na uinjilisti.

## MUHTASARI
## SOMO LA TANO

1. Tutumie Neno gani, sakramenti au maagizo?
   A. Neno sakramenti lina maana gani?
   B. Neno maagizo lina maana gani?
   C. Wabatisti hukubali ubatizo na meza ya Bwana kuwa ni maagizo.

2. Wabatisti wanaamini nini kuhusu ubatizo?
   A. Je, kulikuwako na ubatizo kabla ya ubatizo wa Kristo?
   B. Ubatizo wa kikristo ni upi?
      1) Ubatizo wa Agano Jipya ni wa waamini tu.
      2) Ubatizo wa Agano Jipya ni wa kuchovya.
      3) Ubatizo wa Agano Jipya ni ushuhuda wa maisha mapya katika Kristo.

3. Wabatisti wanaamini nini kuhusu meza ya Bwana?
   A. Meza ya Bwana huonyesha maana mapya wakati wa Pasaka.
   B. Wabatisti hufundisha nini kuhusu meza ya Bwana
      1) Meza ya Bwana ni kwa Wakristo pekee.
      2) Meza ya Bwana ni mfano wa ukweli mkuu.
      3) Meza ya Bwana ni chakula cha ukumbusho.
      4) Meza ya Bwana ni wakati wa ibada.

4. Ni nani aliye na amri juu ya maagizo hayo?
   A. Amri ya mwisho juu ya maagizo ya kanisa ni Kristo.
   B. Maagizo yanapaswa kusimamiwa na kanisa.

5. Ni maagizo gani yanayohitajiwa kufuatwa na kanisa?
   A. Haya ni mapendekezo ya mwongozo kuhusu ubatizo.
      1) Lazima kanisa liwabatize wote wanaopaswa kuwa Wakristo.
      2) Lazima kanisa liwabatize wale tu wamemkiri Kristo.
      3) Kanisa liwabatize waamini wote ambao hawakubatizwa kibiblia.

   B. Haya ni mashauri kuhusu mwongozo wa meza ya Bwana.
      1) Kanisa liwakubalie Wakristo tu kushiriki katika meza ya Bwana.
      2) Kanisa likate shauri kuhusu anayealikwa kushiriki katika meza ya Bwana.
      3) Kanisa linapaswa kuweka mpango wa kila mara kuhusu matendo ya meza ya Bwana.

6. Tumejifunza nini kuhusu maagizo ya kanisa?

## SURA YA TANO

## MAAGIZO YA KANISA

Kwa nini watu wengine huita ubatizo na chakula cha Bwana sakramenti? Kwa nini wengine huviita maagizo? Je, kuna maagizo mangapi? Ni yapi ambayo yanapasa kufanywa? Kuna historia gani inayohusu ubatizo na meza ya Bwana? Ni nani aliye na uwezo wa kufanya mambo haya, ni mchungaji au ni Kanisa? Ubatizo na meza ya Bwana ni desturi ya kikristo inayofundisha ukweli wa kibiblia.

1. Tutumie Neno gani, sakramenti au maagizo?

A. Neno sakramenti lina maana gani?

Madhehebu fulani hutumia neno hili sakramenti. Sakramenti ina maana ya "alama, ahadi au muhuri." Neno hili lilitumiwa kwa kiapo cha ahadi ya utii. Askari wa Kirumi alipojiunga na uaskari alipaswa kula kiapo cha utii, au sakramenti katika nyakati za Wakristo wa kwanza, ubatizo na meza ya Bwana vikawa viapo vya kuonyesha uaminifu au utii kwa Yesu. Kwa hivyo, wengi wakaviita sakramenti. Hata hivyo, jinsi sakramenti inavyotumiwa na Kanisa la Katoliki siku hizi ina maana tofauti. Sakramenti inaaminika kuwa ni njia ya kupata baraka za Mungu. Wengine hufikiri zaidi. Kanisa Katoliki lina sakramenti saba.

B. Neno maagizo, lina maana gani?

Neno maagizo, lina maana ya "hitaji, kanuni, agano, amri." Kanisa la kwanza lilijua ya kwamba limeamriwa kuendelea kufanya matendo hayo. Wakristo waliamini ya kwamba Mungu alitenga ubatizo na kushiriki katika meza ya Bwana kuwa tendo la Kanisa. Kwa hivyo yanaitwa maagizo kwa sababu Mungu aliamuru yafanywe. Mambo haya hufundisha ukweli mkuu wa kibiblia. Matendo haya kama mafundisho hayampi mtu baraka yo yote maalum. Bali yanashuhudia juu ya baraka ambayo imekwisha pokewa. Maagizo haya ni mfano wa ukweli mkuu.

C. Wabatisti hukubali ubatizo na meza ya Bwana kuwa ni maagizo.

Wabatisti hutumia neno hili, maagizo wakiwa na maana mbili. Ya kwanza ni, Kristo amekwisha kupokea neema na baraka za Mungu. Hivyo anataka kushuhudia ya kwamba neema na baraka za Mungu zimo. Sasa, anataka kushuhudia ya kwamba neema na baraka za Mungu ni kuu. Mtu hawezi kwa njia yo yote kuchuma neema ya Mungu. Wakati alipostahili hukumu, Mungu alimsamehe. Alipostahili adhabu, Mungu akampa neema hii, "...ambayo tunasi-

mama ndani yake..." (Warumi 5:2). Neema hii na msamaha huu ni vipawa vya bure kutoka kwa Mungu. Sababu ya pili ni kwamba Mungu amewaamuru Wakristo kuwa na ubatizo na meza ya Bwana. Kazi hiyo siyo desturi ya mwanadamu. Kila wakati Wakristo wanapofanya hivyo katika ibada ya kanisa, huwa wanatoa ushuhuda. Huwa wanaonyesha wengine vile Mungu alivyowatendea. Wanakumbuka baraka zao katika Kristo.

Makanisa ya kwanza yalikuwa tu na ubatizo na meza ya Bwana. Na baraza za makanisa tofauti wakaongeza maagizo mengine matano zaidi katika miaka iliyofuata. Makundi fulani husafisha miguu. Bila shaka kuna dhehebu moja ambalo halifuati agizo lolote kwa sasa. Wabatisti hukubali tu ubatizo na meza ya Bwana. Kwa nini wao hukubali hayo mawili tu? Ni kwa sababu hayo mawili hushuhudia ukweli maalum wa msingi wa injili. Hayo mawili huwakumbusha Wakristo kuhusu kifo, mazishi na ufufuo wa Yesu Kristo. Hii ndiyo habari njema ambayo Yesu alitufanyia sisi. Yeye ndiye njia ya wokovu.

2. Wabatisti wanaamini nini kuhusu ubatizo?
   (Mathayo 28:19-20; Yohana 3:22-23; Matendo 2:42; 10:47; Warumi 6:1-11).

A. Je, kulikuwako na ubatizo kabla ya ubatizo wa Kristo?

Wayahudi waliwabatiza watu wa mataifa waliokata shauri kufuata dini ya Kiyahudi. Ubatizo wao ulikuwa na shabaha mbili. Shabaha ya kwanza ilikuwa kulinda na kutetea dini ya Kiyahudi. Ya pili ilikuwa kumfundisha mwamini umuhimu wa shauri lake alilokata. Walimsomea maagano. Halafu mtu huyo mwenyewe alijichovya kabisa ndani ya maji. Mpango huo wa ubatizo ulijulikana kuwa ubatizo wa kibinafsi. Kutokana na tendo hili tunayo mafundisho makuu matatu. Kwanza, wale waliobatizwa ni wale tu waliojua umuhimu wa shauri walilokata. Pili, uhakika wa imani ukawa wa kwanza kabla ya ubatizo. Tatu, kuchovya mtu ndani ya maji, kukaonyesha ukamilifu wa kujitolea kwake katika imani yake mpya.

Ubatizo wa Yohana Mbatizaji ulikuwa sawa na ubatizo wa Kiyahudi katika njia mbili. Kwanza, wale tu waliosikia ujumbe wa Mungu waliweza kubatizwa. Pili, ubatizo wake ulikuwa wa kuchovya ndani ya maji. Hata hivyo, ubatizo huu ulikuwa tofauti katika njia tatu. Kwanza, Yohana aliwabatiza Wayahudi. Yohana hakuamini ya kwamba mtu akizaliwa Myahudi, eti yeye ni mfuasi kamili wa Mungu. Pili, Yohana mwenyewe alibatiza watu. Mtu hakujibatiza mwenyewe. Tatu, ubatizo wa Yohana ulikuwa mfano au alama ya toba na ondoleo la dhambi.

B. Ubatizo wa kikristo ni upi?

1) Ubatizo wa Agano Jipya ni wa waamini tu.

Ubatizo ni alama inayoonyesha jambo lililotendeka. Ubatizo haumwokoi mtu. Agano Jipya hufundisha ya kwamba waamini tu ndio wanaoweza kubatizwa. na hivyo ndivyo kanisa la Agano Jipya lilivyofanya. Wabatisti wanafuata mfano huu wa ubatizo wa mwamini.

2) Ubatizo wa Agano Jipya ni wa kuchovya.

Neno la Kiyunani "ubatizo" ambalo lina maana ya kuchovya, lilikuja katika lugha ya Kiingereza kwa njia ya ajabu. Mfalme wa Uingereza aliyeitwa James (Yakobo) alitaka Biblia itafsiriwe katika lugha ya kiingereza. Yeye mwenyewe alikuwa kiongozi mkuu wa kanisa la Uingereza. Ubatizo wao ni wa kunyunyizia maji. Na badala ya kulitafsiri neno jinsi lilivyo, mtafsiri alikata shauri kuliandika moja kwa moja kutoka lugha ya Kiyunani. Kwa hivyo tuna neno batizo badala ya chovya. Katika imani ya Kiyahudi na pia katika makanisa ya Agano Jipya, ubatizo ulikuwa wa kuchovya.

3) Ubatizo wa Agano Jipya ni ushuhuda wa maisha mapya katika Kristo.

Kwa kawaida mtu hubatizwa mbele ya mashahidi. Wao hushuhudia kuhusu maisha ya mtu huyo anayebatizwa ndani ya Yesu. Kwa kubatizwa kwake anaonyesha imani yake. Ubatizo wa kuchovya huonyesha picha ya kifo, mazishi na ufufuo wa Yesu. Ubatizo huonyesha ya kwamba mtu amekuwa mfu kwa njia ya dhambi zake, amezika maisha yake ya kale na amefufuka katika maisha mapya. Mkristo huyo mpya huonyesha katika ubatizo utii, kujitolea na umoja wake na Kristo. Wabatisti huwabatiza tu wale ambao wamepata maisha katika Kristo.

3. Wabatisti wanaamini nini kuhusu meza ya Bwana?
(Mathayo 26:26-30; I Wakorintho 10:16-22; 11:23-32).

A. Meza ya Bwana huonyesha maana mapya wakati wa Pasaka.

Pasaka imekuwa siku muhimu sana kwa Waebrania. Katika siku hiyo, hukumbuka usiku ule walipotoka katika utumwa huko Misri. Kila jamaa hula chakula cha ukumbusho. Usiku ule Yesu aliposalitiwa alikula chakula cha mwisho pamoja na wanafunzi wake. Hata hivyo, alitoa maana mpya kwa mfano wa zamani. Alitumia mkate kuonyesha mfano wa mwili wake. Akatumia maji ya matunda kwa kuonyesha mfano wa damu yake. Waebrania waliokolewa kwa njia ya damu na nyama ya kondoo. Yesu Mwana kondoo

wa Mungu hutuokoa kutoka katika utumwa wa dhambi na mauti. Damu ya kondoo iliwalinda Waebrania kutokana na hasira ya malaika wa kifo. Damu ya Yesu huwalinda waamini kutoka katika mauti ya kiroho. Kondoo alichukua mahali pa wazaliwa wa kwanza wa kiume wa Waisraeli. Yesu alichukua mahali pa waamini. Chakula kile kilikuwa kwa Waebrania peke yao. Meza ya Bwana ni kwa waamini tu. Wakati wa kula pamoja, waamini hukumbuka mambo makuu ambayo Mungu amewafanyia.

B. Wabatisti hufundisha nini kuhusu meza ya Bwana?

1) Meza ya Bwana ni kwa Wakristo pekee.

Paulo anawaambia Wakristo ya kwamba meza ya Bwana inafaa kuwa kwa waamini peke yao. Wale ambao si Wakristo haifai washiriki katika meza ya Bwana. Hawajakubali dhabihu ya Yesu. Kwa hivyo hawastahili kukaa katika meza yake. Meza ya Bwana ni kwa wale tu waliomkubali Yesu kuwa Bwana wao. Wamesamehewa dhambi na kupokea baraka za Mungu za uzima wa milele. Wamekuwa washiriki katika jamaa ya Mungu ndani ya Kristo. Ni hao tu wanaoweza kukaribishwa katika meza ya Bwana.

2) Meza ya Bwana ni mfano wa ukweli mkuu.

Meza ya Bwana ni onyesho la toleo alilofanya Yesu Kristo kwa ajili yetu. Hili ni somo muhimu sana la Biblia. Yesu alitoa mwili wake na damu yake kwa kuisafisha dhambi. Maji ya matunda na mkate ni mfano. Hakukuwa miujiza ndani ya mkate na maji ya matunda. Hii huwakumbusha tu waamini kuhusu mwili na damu ya Yesu.

Wakatoliki huamini ya kwamba mkate na maji ya matunda hufanyika mwili hasa na damu kamili ya Yesu. Martin Luther alisema ya kwamba mkate na maji ya matunda havifanyiki kuwa mwili na damu hasa ya Kristo. Lakini mwili wa Yesu na damu yake hushiriki ndani ya mkate na maji ya matunda. Wabatisti huamini ya kwamba mkate na matunda ni mfano wa mwili na damu ya Kristo. Kwa hivyo, vitu hivyo viwili havimpatii mtu baraka maalum. Ni mfano wa baraka ambavyo mwamini amekwisha kupokea tayari.

3) Meza ya Bwana ni chakula cha ukumbusho.

Maisha, kifo na ufufuo wa Yesu ni ujumbe wa injili. Meza ya Bwana ni chakula cha ukumbusho. Wakati wote ambapo Wakristo huwa na meza ya Bwana, hukumbuka mambo ambayo Yesu aliwafanyia. Wakristo hukumbuka maisha yake, kifo chake na ufufuo wake. Huyakumbuka matendo yote kwa sababu ya wokovu wao. Hukumbuka ushindi wake juu ya dhambi na mauti. Wakristo hukumbuka ile ahadi yake aliposema ya kwamba hatawaacha peke

yao hapa duniani. Roho Mtakatifu yuko tayari kuwasaidia wale wanaoamini kushinda dhambi na majaribu. Hukumbuka pia ahadi yake ya kurudi na kuwachukua watu wake. Kwa hivyo, Wakristo wanaposhiriki katika meza ya Bwana, huyakumbuka mafundisho makuu ya Biblia.

4) Meza ya Bwana ni wakati wa ibada.

Wakati wo wote ambapo kanisa huwa na meza ya Bwana, lazima uwe ni wakati wa ibada. Mtume Paulo katika I Wakorintho 11:20-28 alilazimika kusahihisha matendo ya Wakorintho. Walikuwa wakitumia meza ya Bwana katika njia zingine zisizo za maana. Haikuwa saa yao ya ibada. Katika ibada Mkristo hujichunguza maisha yake na matendo yake. Hii hufanyika wakati wa meza ya Bwana kwa sababu ni wakati wa ibada.

4. Ni nani aliye na amri juu ya maagizo hayo (Meza ya Bwana na ubatizo).
(I Wakorintho 11:23-26; Mathayo 28:19-20).

A. Amri ya mwisho juu ya maagizo ya kanisa ni Kristo.

Amri ya mwisho juu ya ubatizo na meza ya Bwana ni Yesu Kristo mwenyewe. Alisema ya kwamba amri yote ni yake. Aliwaamuru Wakristo wote kama mwili wa waamini kufanya maagizo yake. Wanapaswa kufanya hivyo huku wakiendelea kuwafanya watu kuwa wanafunzi wake. Hata hivyo, ni nani anayesimamia maagizo haya hapa duniani, ni mchungaji au ni kanisa?

B. Maagizo yanapaswa kusimamiwa na kanisa.

Wengine hufikiri ya kwamba maagizo husimamiwa na mchungaji. Wanafikiri ya kwamba mchungaji amepewa amri hiyo kwa kuwekewa mikono. Hata hivyo Wabatisti wanaamini katika ukuhani wa waamini wote. Kanisa pamoja na washiriki wake wote wako chini ya uongozi wa Kristo. Roho wa Mungu huwaongoza na Biblia ikiwa amri yao ya mwisho. Kwa hivyo Wabatisti huamini ya kwamba maagizo ya Yesu kwa kanisa yako chini ya amri ya Kanisa lenyewe.

Kanisa likiongozwa na Yesu Kristo hukata shauri kuhusu uongozi wa maagizo. Kanisa hukata shauri juu ya nani anayekubaliwa katika ushirika, na sio mchungaji. Mchungaji ni kiongozi wa kiroho, siye mtawala. Kwa kawaida kundi hukubaliana naye juu ya yule anayepaswa kubatizwa. Ingawa hivyo, hana amri ya kumbatiza mtu ye yote pasipo na kibali cha kanisa.

5. Ni maagizo gani yanayohitajiwa kufuatwa na kanisa?

A. Haya ni mapendekezo ya mwongozo kuhusu ubatizo.

1) Lazima kanisa liwabatize wote wanaopaswa kuwa Wakristo.

Ubatizo ni muhimu. Ni tendo muhimu ambalo mwili wa Kristo umeamriwa kufanya. Tumeamriwa kuwabatiza waamini. Kwa hivyo watu wote wanaopata kuwa Wakristo lazima wabatizwe.

2) Lazima kanisa liwabatize wale tu wamemkiri Kristo.

Kanisa lina wajibu wa kusimamia ubatizo. Ubatizo siyo njia ya wokovu. Ni ushuhuda wa yule aliyekwisha okolewa. Ikiwa maisha ya mtu hayaonyeshi ya kwamba ameokolewa, kanisa lisimbatize. Ikiwa kanisa litachunguza vizuri wale wanaobatizwa, litapunguza shida ya wakati ujao.

3) Kanisa liwabatize waamini wote ambao hawakubatizwa kibiblia.

Waamini wote ambao hawakuzamishwa ndani ya maji kibiblia, yafaa wabatizwe. Wale wanaokuja kutoka makanisa mengine ya Kibatisti yafaa waulizwe kuhusu ubatizo wao. Kanisa moja lilikuwa likitaka kumweka wakfu shemasi. Na katika mahojiano wakagundua ya kwamba hakuwa amebatizwa kama waamini kwa njia ya uzamisho Kanisa liwaulize waamini wote kubatizwa.

B. Haya ni mashauri kuhusu mwongozo wa meza ya Bwana.

1) Kanisa liwakubalie Wakristo tu kushiriki katika meza ya Bwana.

Hili ni hitaji la kibiblia. Meza ya Bwana ni wakati wa ukumbusho. Ni jinsi gani mtu asiye Mkristo anaweza kukumbuka wokovu wake? Meza ya Bwana, sawa na ubatizo, haina miujiza. Haimpi mtu damu na mwili Yesu. Wanaopaswa kukaribishwa katika meza ya Bwana ni waliookoka pekee.

2) Kanisa likate shauri kuhusu anayealikwa kushiriki katika meza ya Bwana.

Wabatisti hutumia njia tatu tofauti kuhusu jambo hili. Kanisa likate shauri juu ya njia ya kufuata.

a. Ushirika wa kanisa pekee "Closed Communion." Ushirika huu huwapa washiriki wa kanisa lile pekee kushiriki katika meza ya Bwana. Hao huamini ya kwamba wana amri juu ya matendo ya washiriki wao pekee. Kwa hivyo wana uwezo wa kuhukumu mambo ya kiroho juu ya washiriki hao peke yao. Ubatizo wa kibiblia na amri ya kanisa la mahali fulani ni mambo muhimu sana kuhusu desturi hii.

b. Ushirika wa karibu "Closed Communion." Ushiriki huu huwakubalia Wabatisti wa makanisa mengine kushiriki katika meza ya Bwana. Huamini ya kwamba kanisa lingine la Kibatisti huamini sawa na vile wanavyoamini. Mshiriki mwenye ushirika mwema na kanisa lake atakubaliwa na Kanisa hilo kama mshiriki. Kwa sababu hiyo, wanaamini ya kwamba huyo anaweza kushiriki katika meza ya Bwana pamoja nao. Ubatizo wa kibiblia na amri ya kanisa la mahali ni muhimu kwa desturi hii. Hata hivyo, kanisa huweka mkazo mkuu wa imani kwa Wabatisti wenzao.

c. Ushirika ulio wazi "Open communion." Ushirika huu huwapa Wakristo wote uhuru kushiriki katika meza ya Bwana pamoja nao. Imani hii haifanyi ubatizo wa kibiblia kuonyesha matokeo yake hasa. Wale wanaofanya njia hii kuwa ya kawaida huamini ya kwamba maagizo ni ya Kikristo badala ya kuwa ya kikanisa. Kama agizo hili ni la Kikristo, basi hudai ya kwamba kanisa halina amri juu ya mtu ye yote anayepokea meza ya Bwana.

3) Kanisa linapaswa kuweka mpango wa kila mara kuhusu matendo ya meza ya Bwana.

Kanisa lahitaji kuwa na mpango wa kila wakati kuhusu kuwa na meza ya Bwana. Wengine huwa na meza ya Bwana kila baada ya miezi mitatu. Biblia haisemi kuhusu kufanywa mara ngapi. Kwa hivyo, ni afadhali kanisa kukata shauri wawe na meza ya Bwana mara ngapi na lini.

6. Tumejifunza nini kuhusu maagizo ya kanisa?

1. Maagizo ni ushuhuda wa baraka zilizopokelewa.
2. Maagizo ni kwa waamini pekee.
3. Ubatizo wa uzamisho huonyesha kujitolea kwa mtu na umoja wa kifo, mazishi na ufufuo wa Yesu Kristo.
4. Meza ya Bwana hutuonyesha na kutukumbusha toleo ambalo Yesu alitufanyia pale msalabani.
5. Amri ya maagizo hayo imo ndani ya Yesu Kristo na ni chini ya mamlaka ya kanisa.

## MUHTASARI
## SOMO LA SITA

1. Nani Anayestahili kuwa Mshiriki wa Kanisa la Kibatisti?
   A. Kuzaliwa mara ya pili ni jambo la kwanza linalohitajika.
   B. Kubatizwa kwa njia ya uzamisho ni jambo kuu la pili.
   C. Kuna kanuni za misingi ya kibiblia kuhusu imani hii?

2. Ni misingi gani ya kibiblia muhimu inayohusu washiriki wa kanisa kufanya kazi pamoja.
   A. Usawa wa ushirika ni fundisho la Agano Jipya.
   B. Udugu wa washiriki ni fundisho la Kibiblia.

3. Kama mshiriki wa kanisa una wajibu wo wote?
   A. Una wajibu wa vipawa vyako vya kiroho?
   B. Una wajibu wa kusaidia Kanisa lako.
      1) Kwa njia ya maombi yako.
      2) Kwa njia ya Fungu lako la kumi na matoleo.
      3) Kwa njia ya mahudhurio yako ya uaminifu.
      4) Kwa njia ya kuwatia wengine moyo.
      5) Kwa njia ya mashauri yako ya maombi.
   C. Una wajibu wa uinjilisti na kuwafundisha wengine.

4. Ushirika uliokomaa wa kanisa una matokeo gani?
   A. Tokeo ni ushirika.
   B. Tokeo ni kukua kiroho.
   C. Tokeo ni nguvu ya kiroho.

5. Tumejifunza nini kuhusu ushirika wa Kanisa?

# SURA YA SITA
# USHIRIKA WA KANISA

Ni nani ambaye angekuwa mshiriki wa Kanisa la Kibatisti? Ni kanuni gani za kibiblia muhimu zinazohusu ushiriki wa Kanisa? Kuna nafasi na wajibu gani? Tunataka kuyajibu maswali haya katika sura hii.

## 1. Nani Anayestahili kuwa Mshiriki wa Kanisa la Kibatisti?

Ushirika wa kanisa ni kwa wale waliookolewa na kubatizwa pekee. Mwamini aliyebatizwa hutimiza mambo mawili makuu ya imani.

### A. Kuzaliwa mara ya pili ni jambo la kwanza linalohitajika.

Ushirika wa kanisa ni muhimu. Ingawa hivyo, ushirika si muhimu sana kama kuzaliwa mara ya pili na kuwa mkristo. Mtu anayeomba kuwa mshiriki wa kanisa anapaswa kuwa mtu ambaye ameokolewa tayari. Kuzaliwa upya kwaletwa na Mungu. Roho Mtakatifu huja ndani ya maisha ya mtu na kuonyesha mtu dhambi zake. Mtu huyo huzitubu dhambi zake na kwa imani huyaweka maisha yake kwa Bwana Yesu Kristo. Afanyapo hivyo, huwa mtu mpya. Badiliko hilo la kimaisha huitwa kuzaliwa upya. Mtu ye yote ambaye amezaliwa upya anaweza kuwa mshiriki wa Kanisa. Si mtu ye yote tu anayestahili hatua hii isipokuwa awe amezaliwa upya kwa imani. Kanisa ni ushirika wa waamini, na waamini tu ndio wanaostahili kujiunga katika ushirika huu. Mtu ambaye hajaokolewa hawezi kuwa mwenyeji katika ufalme wa Mungu.

### B. Kubatizwa kwa njia ya uzamisho ni jambo kuu la pili.

Ubatizo wa uzamisho ni jambo lingine la umuhimu. Baada ya mtu kuzaliwa mara ya pili hutaka kuwaambia wengine habari za maisha yake mapya ndani ya Kristo. Njia moja ya kufanya hivyo ni kwa ubatizo. Waamini wanaamrishwa kubatizwa. Wale ambao ni watii wa amri ya Yesu watabatizwa. Maana ya ubatizo ni "kuchovya" au "kuzamisha." Katika ubatizo wa kuchovya mwamini huonyesha picha ya ufahamu wake wa wokovu. Huonyesha kifo chake kwa dhambi, mazishi yake na ufufuo wake katika maisha mapya. Ni wale waliookolewa tu wanaostahili kubatizwa.

Ubatizo hauokoi mtu, wala ushirika. Maana yake ni kusema mtu akibatizwa tu na kuwa mshiriki wa Kanisa bila kumwamini Kristo hawezi kuokolewa. Ingawaje ni hivyo, mtu akitaka kuwa mshiriki wa Kanisa inampasa kubatizwa. Jambo hili lina ukweli gani ikiwa ubatizo haumwokoi mtu? Ubatizo huonyesha kujitolea kwa mtu kwa Yesu Kristo. Kanisa linawataka washiriki wenye nia ya

kutoa ushuhuda wao.

C. Kuna kanuni za misingi ya Kibiblia kuhusu imani hii?

Misingi ya kibiblia kuhusu imani hii hupatikana katika Matendo 2:41. "Nao waliolipokea neno lake...." maana yake ni, wale waliotubu dhambi na kumwamini Yesu. Walifanya kama Petro alivyowaambia kufanya. "....Wakabatizwa" maana yake ni wale ambao walikuwa wameokolewa wakabatizwa kwa uzamisho ndani ya maji. Huu ulikuwa ushuhuda ya kwamba Kristo amebadilisha maisha yao. "....Na siku ile wakaongezeka..." huonyesha ya kwamba ushirika wa Kanisa hufuata kuamini na kubatizwa. "...Watu wapata elfu tatu...." hutuonyesha ya kwamba kulikuwa na watu elfu tatu waamini waliobatizwa.

Katika Matendo 2:42-47, asili ya ushirika wa kanisa inaweza kuonekana. Kanisa lilikuwa na ushirika na uhuru ndani ya Yesu Kristo. Walijifunza pamoja na kukubali kushika wajibu wao. Wakawa mashahidi. Katika hayo yote Yesu akawa Bwana.

2. Ni misingi gani ya kibiblia muhimu inayohusu washiriki wa kanisa kufanya kazi pamoja?

Washiriki wa kanisa wanahitaji kufikiriana wenyewe kama ndugu na dada. Wanahitaji kuwakubali wengine kama vile wanavyokubaliwa. Yesu akasema, "...mtu ye yote atakayefanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu" (Marko 3:35). Mtume Paulo hutuambia hivi, "Hapana Myahudi wala Myunani. Hapa mtumwa wala mtu huru. Hapana mtu mume wala mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:28).

A. Usawa wa ushirika ni fundisho la Agano Jipya.

Mtu ye yote ambaye amezaliwa mara ya pili ana uwezo wa kujikatia shauri kuhusu mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Ikiwa waamini wana uwezo wa kufanya hivyo basi wana usawa. Hakuna migawanyiko katika mwili wa kiroho. Watu fulani au mtu fulani hawezi kuwa bora kuliko wengine. Wakristo wote ni wenye dhambi waliookolewa kwa neema ya Mungu. Wamesamehewa na wana uhuru katika Kristo. Huu ni msingi na utawala wa Kanisa la Kibatisti. Utawala wao ni wa washiriki wenyewe. Washiriki wa kila kundi hukata shauri kwamba wafanye nini. Wanaweza kuwa na kamati ya kufikiria mambo fulani na kufanya mapendekezo. Halafu washiriki wakate shauri kwamba wafanye nini. Huu ndio msingi wa kanisa wanalotaka la Kibatisti. Wakati mwingine kuna washiriki wanaotaka kutawala kanisa. Watu hawa mara nyingi huzungumza juu ya usawa. Ingawa hivyo, kwa kweli huwa hawataki usawa.

Huwa wanataka kulitawala kanisa. Wanatumia neno usawa kwa kusudi la kupata wanachotaka. Kanisa linahitaji kutetea usawa wa washiriki wake wote. Washiriki wasiwaruhusu watu wachache kulitawala kanisa.

B. Udugu wa washiriki ni fundisho la Kibiblia.

Kufuata mapenzi ya Mungu pamoja huleta udugu. Washiriki wana moyo wa udugu kwa sababu huyaona mengi pamoja. Wanapofanya kazi pamoja, kushiriki pamoja na kuomba pamoja, huwa na urafiki wa karibu. Urafiki huo wa karibu huwa udugu. Kanisa linapaswa kuwa kama jamaa iliyo wazi. Jamaa katika Kristo hushiriki katika usawa na upendo. Jamaa kama hiyo si ya kimwili bali ni ya kiroho.

3. Kama mshiriki wa kanisa una wajibu wo wote?

Kama mshiriki wa Kanisa una nafasi na wajibu. Mambo haya mawili hayawezi kutenganishwa. Wengi hutaka kupata nafasi bila kukubali wajibu. Uhuru huleta wajibu au madaraka kwa kila mwananchi. Mwenyeji aliye na wajibu hupenda kutetea uhuru kwa kusaidia serikali yake na kupinga uharibifu. Wajibu wa kuwa mshiriki mwema wa kanisa hutokana na uhuru katika Kristo. Kama mshiriki wa kanisa unapaswa kutumia vipawa vyako vya kiroho kulisaidia Kanisa lako. Unahitaji kuwa na bidii katika kuwaongoza wengine kwa Yesu, ukiwasaidia kukua katika imani. Kama Mkristo, una wajibu mbele ya Mungu. Atakusaidia kuendelea katika uwakili wa wajibu wako.

A. Una wajibu kwa vipawa vyako vya kiroho?

Kila mkristo amepewa kipawa fulani cha kiroho. Una wajibu kukitumia kipawa chako cha kiroho kwa kuwasaidia wengine.

Kuna vipawa vingi vya kiroho. Kila kimoja ni muhimu. Mtume Paulo anazungumza juu ya vipawa hivi katika 1 Wakorintho 12. Hapo anatumia mwili kama mfano wa umuhimu wa kila kipawa katika kanisa la mahali fulani. Kanisa ni mwili wa Kristo. Kila kipawa ni kwa ajili ya wema na uzuri wa kanisa (1 Wakorintho 12:7). Paulo anaorodhesha vipawa fulani vya kiroho katika 1 Wakorintho 12:8-10. Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" (I Wakorintho 12:11).

Vipawa vya kuhubiri, kufundisha na kuponya ni vipawa ambavyo watu wengi hufikiri ya kwamba ni vya maana sana. Kuwa na uwezo wa kutafsiri na kulihubiri Neno la Mungu ni kipawa kizuri. Kuwa na uwezo wa kufundisha ni kipawa kizuri. Kuwa

tabibu na kuweza kuwaponya watu, Bwana aweza kumtumia mtu wa aina hiyo. Ingawa vipawa hivi ni muhimu, si kwamba ni bora kuliko vipawa vingine. Kuna vipawa vingine muhimu sana ambavyo watu hawawezi kuviona kwa urahisi. Kuwa na uwezo wa kumsikiliza rafiki ni kipawa ambacho watu wengi hawaoni. Kuwa na uwezo wa kumsaidia mwingine akate shauri ni kipawa ambacho wengi hawaoni. Vipawa hivi ni muhimu sana katika mwili wa Kristo.

Mambo mengi yamesemwa sana kuhusu kipawa cha kunena kwa lugha. Yawezekana kipawa hiki kimetumiwa na kueleweka vibaya kuliko vipawa vingine vyote vya roho. Wengine wangependa kuwa na kipawa hiki ili wajione kuwa bora zaidi. Wengine hufikiri ya kwamba mtu hawi Mkristo wa kiroho kama hana kipawa hiki cha kunena kwa lugha. Tunda la Roho (Wagalatia 5:22-23) huonyesha utu mkamilifu wa Mkristo, yaani, Mkristo aliyekua kiroho. Vipawa vya Roho huwaweka Wakristo tayari katika huduma yao. Kipawa cha kunena kwa lugha ni kipawa cha chini kuliko vyote kama wengi wanavyotafsiri siku hizi. Hakitimizi makusudi mengi ya kanisa. Uinjilisti na kuwafundisha wengine ni kusudi la kanisa. Baada ya siku ile ya Pentekoste katika Matendo 2, maandiko husema juu ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Kila mara utaona ya kwamba kila aliyejazwa roho hutoa ushuhuda wake kwa bidii kuhusu Yesu. Waamini wanaamriwa kujazwa Roho Mtakatifu (Waefeso 5:18). Ukisoma vifungu 15-21 utaona ya kwamba Wakristo wanapaswa kuendelea kama watu wenye hekima. Wanahitaji kuwatia moyo wengine katika nyimbo za kiroho. Watoe shukrani kwa kila kitu. Huku ndiko kuelimisha au kutiana nguvu. Nguvu katika uinjilisti na uthabiti katika kuelimisha ni onyesho ama alama ya ujazo wa Roho Mtakatifu. Kunena katika lugha, si thibitisho la wokovu wala ujazo wa Roho Mtakatifu.

Kipawa cha Roho Mtakatifu hakifanyi mtu kuwa muhimu mbele za Mungu. Mkristo si mtu muhimu eti kwa sababu anaweza kufanya mambo makuu; lakini waamini ni watu muhimu kwa sababu Kristo alikufa kwa dhambi zao. Ni lazima kuwa waaminifu katika kufanya yale ambayo Yesu anawapa kufanya. Wewe kama mwamini unahitaji kugundua kipawa chako. Jambo la pili, chunguza maisha yako na uwezo wako. Yaweza kuwa ya kwamba kitu kile unachopenda kufanya ndicho kipawa chako kutoka kwa Mungu. Jambo la tatu, waulize Wakristo wema unaowajua wakwambie wanafikiri kipawa chako ni kipi. Jambo la nne, jaribu kutumia kile wanachofikiri kuwa ni kipawa chako. Ikiwa unakifurahia na Mungu anakibariki basi yaweza kuwa hicho ndicho kipawa chako kwa huduma zaidi. Unahitaji kukikuza kipawa hicho chako kwa huduma zaidi. Unaweza kukuza kipawa chako kwa kukitumia. Unahitaji kukiweka

wakfu kipawa chako kwa matumizi ya utukufu wa Mungu.

B. Una wajibu wa kusaidia Kanisa lako.

1) Kwa njia ya maombi yako (Wafilipi 1:1-19).

Mungu amekufanya uwe na wajibu kwa Kanisa lake. Unahitaji kukumbuka kazi ya Mungu katika sala zako. Na pia uombee washiriki wa Kanisa lako na viongozi wote kwa jumla.

2) Kwa njia ya Fungu lako la kumi na matoleo (1 Wakorintho 16:2; Matendo 2:45).

Mungu amekupa wajibu wa kutoa fungu lako la kumi na matoleo mengine. Mungu hutegemeza kanisa lake na kazi yake kwa njia hii. Kanisa hutegemea washiriki wake kwa pesa ya kila kazi. Wabatisti huamini ya kwamba uwakili wa Kibiblia ni muhimu. Mungu atalibariki kanisa ambalo washiriki wake watalisaidia kkwa kutoa fungu la kumi na matoleo. Uwakili wa kibiblia katika kanisa huleta moyo wa kujitegemea. Sio fundisho la Biblia kumwuliza mtu mwingine kutegemeza kazi ambayo wewe mwenyewe hutaweza kuiendesha. Kanisa lako linahitaji msaada wako. Unahitaji kutoa zaidi ya kiasi kidogo unachoweza kutoa. Kutoa kidogo tu maana yake ni kwamba unataka nafasi bila kushiriki.

3) Kwa njia ya mahudhurio yako ya uaminifu (Waebrania 10:25).

Mungu ameendelea kukusaidia wewe katika wajibu wa kuhudhuria ibada za Kanisa lako. Unapaswa kuwa katika mikutano yote iwezekanavyo. Unapokosa kuhudhuria mikutano ya ibada huwezi kukua katika imani. Kutohudhuria kwako kunawashusha moyo wengine na hata kulidhoofisha kanisa lako.

4) Kwa njia ya kuwatia wengine moyo (Waebrania 10:24)

Mungu amekufanya wewe uwe na madaraka ya kutiana moyo pamoja na wengine. Kama unavyowatia wengine moyo, unajenga kanisa. Ukizungumza na wengine katika wema na upendo huwa unawasaidia. Ukizungumza kwa njia mbaya kwa Wakristo unaumiza na kuzuia kukua kwao kiroho.

5) Kwa njia ya mashauri yako ya maombi (Matendo 15:1-29)

Mungu amekupa madaraka ya kusaidia kanisa lako kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu yalivyo. Unapaswa kusaidia kwa maombi na kutafuta mapenzi ya Mungu kwa Kanisa lako. Una uhuru huo ambao umepewa na Mungu. Kama Mkristo unapaswa kuwa mshiriki wa kanisa aliyekomaa. Mshiriki wa kanisa aliyekomaa husali juu ya mashauri yake.

Katika Matendo 15 washiriki wa Yerusalemu walikuwa washiriki wa kanisa wenye wajibu. Shauri lilikatwa kuhusu wokovu na watu wa mataifa kulingana na mapenzi ya Mungu. Watu wachache waliojua sana juu ya jambo hili walikutanika na kujadili juu yake. Viongozi hawa wakafanya mapendekezo. Kátika Matendo 15:22a twasoma haya, "Basi ikawapendeza midtume wazee na kanisa lote..." Kanisa lote likafanya shauri kuhusu mapenzi ya Mungu yalivyokuwa. Washiriki hawa wa kanisa wakawa waaminifu katika madaraka yao katika kanisa lao. Wewe uwebarikiwa kwa sababu ya uaminifu wako. Ukiwa mwaminifu katika kuyatenda mapenzi ya Mungu basi wengine watabarikiwa.

C. Una wajibu wa uinjilisti na kuwafundisha wengine.

Kusudi la kanisa ni lile la uinjilisti na kuelimisha wengine. Uinjilisti na kuwaongoza wengine kumpokea Yesu kama Bwana na mwokozi. NI LAZIMA UWE MWINJILISTI. Kila mshiriki ana wajibu huo. Kanisa haliwezi kuwalipa watu wa kutosha kufanya kazi hiyo yao ya uinjilisti. Uinjilisti ni pamoja na kuwaombea wapotevu na kuwashirikisha katika ushuhuda wako. Unahitaji kuomba na kuwaambia wengine yale Yesu alikutendea maishani mwako. Kuelimisha ni kuwajenga wale ambao wameokoka. Una wajibu wa kuwasaidia wengine kukua kiroho. Unaweza kuwasaidia wengine kwa mahudhurio yako ya kila mara kanisani. Unaweza kuwasaidia katika kuwa mfano mwema kwa njia ya kutoa sadaka zako. Unaweza kusaidia kwa njia ya kuwashuhudia wengine. Unaweza kusaidia kwa njia ya kufundisha darasa la masomo ya Biblia au kwa kuhubiri. Unaweza kusaidia katika njia hizi zote. Una wajibu mbele ya Mungu kuwasaidia wengine kukua kiroho katika njia yo yote ile unayoweza.

4. Ushirika uliokomaa wa kanisa una matokeo gani?

Wengi hawavuni baraka kamili za kuwa mshiriki wa kanisa. Kwa kufanya mambo hayo yote yaliyotajwa hapo juu, waweza kupata baraka. Ushirika wa kujitolea wa kanisa unaweza kuufanya ushirika kukua, na kuwa wenye nguvu.

A. Tokeo ni ushirika.

Baada ya kuongoka, mwamini hutamani ushirika pamoja na waamini wengine. Ushirika huu ni muhimu. Ni baraka kwa washiriki wa kanisa waliojitolea. Paulo alikuwa njiani kuelekea Dameski kuwafunga na kuwatesa Wakristo. Baada ya kukutana na Yesu njiani, Paulo akatafuta ushirika wa Wakristo. Mtume Yohana alisema, "Hilo tuliloliona na kulisikia twawahubiria na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi na ushirika wetu ni pamoja na

Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo" (1 Yohana 1:3). Wakristo wanapaswa kutafuta ushirika wa Wakristo. Wanastahili kujiunga na Kanisa ambalo linaamini kama wao katika mafunzo ya Biblia. Wabatisti wanakubali haki ya ushirika wa kujisomea na kuielewa Biblia mwenyewe. Kila Mkristo ana haki ya kutafsiri mapenzi ya Mungu katika maisha yake. Imani ya mshiriki inapaswa kukubaliana na ya washiriki wenzake katika Kanisa. Kama sivyo basi, na atafute kanisa analokubaliana nalo.

B. Tokeo ni kukua kiroho

Washiriki wa kanisa waliojitolea kwa kawaida watakua kiroho. Washiriki hukua wanapoomba, kujifunza Biblia na kusikia Neno likihubiriwa. Hukua kwa kushirikiana katika imani na wengine kanisani. Wanapokua kiroho huwa Wakristo wazima na washiriki wema wa kanisa. Watu wengi hufurahia kuona watoto wakikua na kujifunza. Kanisa nalo hufurahia kuona Mkristo mpya akikua na kukomaa. Paulo hutuambia hivi, "....Na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo" (Waefeso 4:15-16).

C. Tokeo ni nguvu ya kiroho.

Nguvu za watu wengi zinaweza kubeba mzigo mzito. Ndivyo ilivyo na kanisa. Wakristo wengi waweza kufanya kazi kubwa pamoja kuliko kazi ya mtu mmoja peke yake. Wakristo wanapofanya kazi pamoja, utumishi wao huongezeka. Ushuhuda wao unatiwa nguvu.

Utumishi wa Mkristo kwa Bwana huongezeka wengine wanapofanya kazi pamoja naye. Mungu humpa kila Mkristo kipawa fulani. Mkristo basi hufanya kazi ndani ya mwili wa Kristo, yaani, kanisa. Vipawa vya washiriki wengine husaidia katika utumishi wake kwa Kristo.

Ushuhuda wa Mkristo hufanywa imara. Wakristo kama kundi wanaweza kumtuma mwinjilisti kuhubiri katika sehemu nyingine mpya. Kundi la Wakristo katika jamii wanaweza kufanya mambo makubwa. Kadiri walivyo wengi kanisani, ndivyo wawezavyo kufanya mambo mengi kwa Kristo Bwana.

5. Tumejifunza nini kuhusu ushirika wa Kanisa?

1. Ubatizo wa mwamini ndio msingi wa ushirika wa kanisa.

2. Ushirika wa kanisa humpa mkristo njia ya ushirika wa kikristo na kukua kiroho.

3. Ushirika wa kanisa umetegemezwa juu ya usawa na udugu wa waamini.

4. Kila mshiriki ana wajibu wa kutumia vipawa vyake kwa maendeleo ya kanisa.

5. Kila mshiriki ana madaraka ya kulitegemeza kanisa lake, kuwaongoza wengine wampokee Yesu, na kuwasaidia wakue katika maisha ya kiroho.

## MUHTASARI
## SOMO LA SABA

1. Viongozi wa kanisa waliitwaje katika Agano Jipya?
   A. Mitume ni wale waliokuwa pamoja na Yesu.
   B. Manabii walisema ujumbe waliopewa na Mungu.
   C. Wainjilisti walihubiri injili katika eneo Jipya.
   D. Mchungaji au mwalimu aliongoza na kufundisha kanisa la mahali fulani.
   E. Mashemasi walitumika katika kanisa la mahali fulani.

2. Ni mtu wa aina gani ambaye kanisa lingemchagua kuwa mchungaji au shemasi?
   A. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu wa kiroho.
   B. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu wa hekima.
   C. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu anayeheshimiwa.

3. Kiongozi wa kanisa awe mtu wa aina gani kulingana na Agano Jipya?
   A. Kiongozi wa kanisa ni mtumishi.
   B. Kiongozi wa kanisa ni kuhani miongoni mwa makuhani.
   C. Kiongozi wa kanisa huitwa na Kristo.

4. Kanisa linawezaje kuwachagua viongozi wake?
   A. Uchaguzi umeelezwa na maneno ya Agano Jipya.
      1) "Kuitwa" (Matendo 13:2)
      2) "Chagua" (Matendo 6:3)
      3) "Kuweka kando" (Matendo 14:23)
   B. Uchaguzi hufanywa na kanisa likiongozwa na Roho Mtakatifu.
   C. Uchaguzi ufanywe kulingana na hitaji la kanisa.
   D. Uchaguzi ufanywe kulingana na uwezo wa Kibiblia.

5. Je, mchungaji alipwe mshahara?
   A. Mchungaji anahitaji kulipwa kwa sababu zifuatazo:
      1) Ni mafundisho ya Biblia.
      2) Ndivyo ilivyo.
   B. Mchungaji alipwe na kanisa analotumikia.
   C. Mchungaji alipwe kila mara na kwa uzuri.

6. Wabatisti wanaamini nini kuhusu kuwaweka viongozi wakfu?
   A. Maana ya wakfu ni nini?
   B. Kuna mifano gani ya Kibiblia kuhusu wakfu?
   C. Wakfu una maana gani katika kanisa la Kibatisti?
7. Tumejifunza nini kuhusu uongozi wa Kanisa?

## SURA YA SABA

## UONGOZI WA KANISA

Viongozi wa kanisa waliitwaje katika Agano Jipya? Walifanya nini? Kiongozi wa kanisa aweje? Wabatisti wanaamini nini kuhusu wakfu? Hebu tuanze kuyajibu maswali haya.

Uongozi wa kanisa ni muhimu. Kanisa likiwa na viongozi wazuri laweza kuwa na nguvu. Mchungaji aliyefaulu kiroho huwa anakua katika imani. Hutafuta kujua mapenzi ya Mungu. Kiongozi wa kanisa ni mtumishi chini ya Yesu Kristo. Yeye anahusika na mambo ya kiroho ya kanisa. Kanisa linahitaji wwatu ambao wameitwa, wenye vipawa na waliokomaa kiroho.

1. Viongozi wa kanisa waliitwaje katika Agano Jipya?

Kulikuwa na viongozi wa aina nne waliotajwa katika kitabu cha Waefeso 4:1. "Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu." Katika Matendo 6 pana uchaguzi wa watumishi wa kanisa (mashemasi).

A. Mitume ni wale waliokuwa pamoja na Yesu.

Mtume maana yake ni kusema "yule ambaye ametengwa kuwa mwakilishi wa mtu mwingine." Katika Matendo 1:20-22 walimchagua mwingine awe mahali pa Yuda. Kwa kustahili cheo hicho, ilimpasa yule achaguliwaye awe alikuwa nao "...tangu utabizo wa Yohana, hata siku ile alipochukuliwa kwetu kwenda juu...." (Matendo 1:22a). Tena lazima awe "....shahidi wa kufufuka kwake pamoja nasi..." (Matendo 1:22b). Hali hii humzuia mtu ye yote siku hizi kujiita mtume. Kuna watu ambao ni mashahidi, na kuwa watu ambao wametumwa. Hata hivyo, hakuna mtu ambaye amestahili cheo kilichotajwa katika Matendo 1:22. Mafundisho ya mitume yalikuwa kuhusu maisha, kazi na mafundisho ya Yesu. Mafundisho yao yameandikwa katika Agano Jipya.

B. Manabii walisema ujumbe waliopewa na Mungu.

Nabii maana yake ni "mtu anayesema kwa niaba ya mwingine." Nabii wa Mungu alisema ujumbe aliopewa na Mungu. Alisema bila kuogopa. Kuna tofauti baina ya umuhimu wa nabii katika Agano la Kale na katika Agano Jipya. Hii ilikuwa hivyo kwa sababu mbili muhimu. Kwanza, ilikuwa kwa sababu ya kuja kwa Yesu. Pili, ilikuwa kwa sababu ya kuja kwa Roho Mtakatifu kwa waamini wote. Katika Agano la Kale Roho Mtakatifu aliwajia watu wachache kwa kazi maalum. Katika Agano Jipya Roho amekuja

kumpa kila mwamini nguvu. Roho atafanya hivyo kwa wale watakaompa nafasi maishani mwao kuwaongoza na kutawala.

C. Wainjilisti walihubiri injili katika eneo Jipya.

Mwinjilisti ni "mtu anayetangaza au anayeleta "habari njema." Neno hili limetumiwa mara tatu katika Agano Jipya. Filipo anaitwa mwinjilisti. "...Tukaingia nyumbani mwa Filipo, mhubiri wa Injili, aliyekuwa mmoja wa wale saba (mashemasi)..." (Matendo 21:8). Katika Waefeso 4:11 mwinjilisti ni mtu aliye na kipawa cha kazi yake. Paulo alimwambia Timotheo "...fanya kazi ya mhubiri...." (2 Timotheo 4:5). Timotheo alimsaidia Paulo katika kazi ya umisheni. Paulo akamwambia Timotheo kuhubiri na kufundisha. Mwinjilisti ni yule ambaye anawahubiria na kuwafundisha injili wale ambao hawajaisikia.

Siku hizi neno hili linatumiwa vibaya. Mwinjilisti ni zaidi ya msaidizi wa mchungaji. Yeye ni zaidi ya mhubiri ambaye hajasomea kazi yake ya kuhubiri. Ni zaidi ya mhubiri wa jitihada. Mwinjilisti huleta habari njema.

D. Mchungaji au mwalimu aliongoza na kufundisha kanisa la mahali fulani.

Walimu wa Biblia husema ya kwamba "....Wachungaji na waalimu...." Katika Waefeso 4:11 ni kazi moja. Utumishi huu ni kuwa mchungaji na mwalimu wa kanisa. Agano Jipya hutumia maneno matatu ya kueleza maana ya kiongozi wa kanisa. "Pastor" maana yake ni "mchungaji." "Bishop" au askofu maana yake ni mwangalizi. "Elder" au mzee maana yake ni kiongozi anayeheshimiwa. Luka anatumia maneno hayo yote matatu kueleza viongozi hao wakiwa na cheo kimoja tu. "....Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa Kanisa" (Matendo 20:17). "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake..." (Matendo 20:28). Wabatisti wanatumia neno, pastor au mchungaji. Wanaamini ya kwamba neno, mchungaji, linaeleza maana ya kiroho ya kazi ya kiongozi wa kanisa.

Maana ya mchungaji na askofu imetumiwa vibaya na watu wengi. Katika madhehebu fulani kuna wachungaji ambao wanasimamia wachungaji wengine na makanisa. Jina mchungaji kwa wengine lina maana ya mchungaji aliyesoma, na kuwekwa wakfu, na anawasimamia viongozi kadha wa makanisa na wainjilisti, mwangalizi au mzee. Mtu huyu alikuwa kiongozi na mwalimu wa kanisa la mahali fulani. Kwa hivyo, Wabatisti hawaamini katika jamaa ya ukasisi. Tena hawaweki vizuizi kwa cheo cha uchungaji

kuwa kwa wale tu waliosoma thiologia.

E. Mashemasi walitumika katika kanisa la mahali fulani.

Maana ya neno shemasi ni utumishi. Katika Yerusalemu Kanisa lilikua kwa haraka sana. Huduma ya kuwasaidia wajane na maskini ikawa nzito kwa mitume. Ilikuwa ikitumia wakati wao wote. Hawakuwa na wakati wa kujifunza, kuomba na kuhubiri. Mgawanyiko ukaanza kanisani. Mitume wakaliomba kanisa "....chagueni watu saba miongoni mwenu....ili tuwawekee mikono juu ya jambo hili" (Matendo 6:3). Kanisa likafanya hivyo. Wale waliochaguliwa wakafanya kazi nzuri, na shida haikusikika tena. Stefano na Filipo pia wakawa wahubiri wazuri. Kazi yao imeandikwa katika Matendo 6, 7 na 8. Kanisa likawachagua watu waliokomaa kiroho kuwa watumishi kama mashemasi.

Kanisa huwategemea mashemasi wake. Hulisaidia Kanisa kufanya kazi yake. Humsaidia mchungaji. Husaidia katika maagizo ya Kanisa, ubatizo na meza ya Bwana. Mashemasi husaidia katika kuwatembelea wagonjwa na watu wengine wenye mahitaji. Mashemasi wema ni baraka kwa kanisa na mchungaji.

2. Ni mtu wa aina gani ambaye kanisa lingemchagua kuwa mchungaji au shemasi?

Kanisa lingemchagua mchungaji au shemasi ambaye tabia yake ni sawa na ya mwingine. Paulo alitupa misaada ya tabia ya mchungaji katika I Timotheo 3:1-7 na kwa mashemasi katika I Timotheo 3:8-13. Mitume walitoa muhtasari mzuri unaompasa mtu wa kanisa kuwa ni mtumishi. "Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima...." (Matendo 6:3).

A. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu wa kiroho.

"...Wenye kujawa na Roho...." maana yake ni mtu anayeongozwa na Roho Mtakatifu. Kujawa inapotumika kwa watu ina maana ya aina ya maisha ambayo mtu huyo anaishi. Kiongozi wa kiroho wa kanisa lazima awe mtu ambaye anaongozwa na Roho wa Mungu. Huo ni uwezekano wa kwanza ambao kanisa linahitaji kufikiria. Ikiwa mtu si wa kiroho basi hahitajiwi aongoze kanisa.

B. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu wa hekima.

"....Wenye kujawa na....hekima...." maana yake mwenye busara. Katika bara la Afrika, kiongozi aliyekomaa na mwenye busara huheshimiwa. Kanisa linamhitaji mtu mwenye busara anayeweza kutoa mashauri mazuri. Ajuaye hali ya maisha, ulimwengu, watu na njia ya Mungu. Hekima siyo elimu ya shuleni. Mtu mwenye

hekima ana zaidi ya ufahamu. Yeye ana hekima na maarifa.

C. Kiongozi wa kanisa lazima awe mtu anayeheshimiwa.

"....Watu....walioshuhudiwa kuwa wema...." ni watu ambao wana heshima nzuri. Mtu mwenye ushuhuda mwema anayeheshimiwa. Kanisa lazima limchague mtu ambaye anaheshimiwa. Lazima aheshimiwe kanisani na katika jamii pia. Awe kielelezo kwa mwamini. Wasioamini wengi wanaangalia maisha na matendo yake. Wataliheshimu kanisa ikiwa kiongozi wao anaheshimiwa.

3. Kiongozi wa kanisa awe mtu wa aina gani kulingana na Agano Jipya?

A. Kiongozi wa kanisa ni mtumishi.

Mitume walikuwa na shida hii ya kuwa mtumishi. Wengi siku hizi wanayo shida hii pia. Mitume wakawa wakitaka kuwaambia wengine jambo la kufanya lakini Yesu akasahihisha fikira zao. Akasema:

> ....Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa
> kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa
> nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha.

Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote. Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Marko 10:42-45).

Ulimwengu haufikiri ya kwamba kiongozi lazima awe mtu wa aina hii. Mchungaji awe mtu wa aina hii. Mchungaji hutafuta kuwasaidia watu; lakini, asiwatumie kwa faida yake.

B. Kiongozi wa kanisa ni kuhani miongoni mwa makuhani.

Kuhani ni mtumishi. Mchungaji ni mtumishi. Wote ni watumishi wa Mungu. Wabatisti wanawaita viongozi wao wachungaji badala ya kuhani. Kanuni ya imani kuhusu ukuhani wa waamini hufundisha ya kwamba kila mwamini ni kuhani na mtumishi. Kwa sababu ya kanuni hii, Wabatisti hufundisha ya kwamba watumishi wote ni sawa mbele ya Mungu. Mchungaji ni kiongozi wa kanisa, lakini si mtumishi peke yake.

C. Kiongozi wa kanisa huitwa na Kristo.

Mungu humwita kila mtu kupokea uzima mpya katika Yesu. Wamwaminio Kristo hufanyika kuwa watumishi wake.

Kanisa lilianzishwa na Kristo. Mungu akatumia kanisa la kila mahali katika uinjilisti na kufundisha. Kanisa ni washiriki ambao ni watumishi wa Mungu. Wao kama wainjilisti wanawaongoza wengine kumpokea Yesu kama Bwana. Wao kama waalimu wanawafundisha waamini wapya katika imani. Katika watumishi hawa Mungu huwaita viongozi wa Kanisa. Viongozi wa kanisa huwatayarisha watumishi ambao ni washiriki wa kanisa. Hawa watumishi hufanya kazi ya uinjilisti na kufundisha. Hii ndiyo kazi ya kuwavuta na kuwaelimisha wale wasio na Kristo.

Kanisa lazima kumpima kila mtu anayesema ya kwamba ameitwa na Mungu kuwa kiongozi. Watu fulani hutaka kuwa wachungaji kwa makusudi mabaya. Wengine hujitakia faida zao, kazi au fahari. Kiongozi wa Kanisa inampasa kutumika kwa sababu ya kujitoa kwake kwa Yesu. Yesu akajitoa mwenyewe kwa wenye dhambi. Wakristo wanapaswa kujitoa wenyewe kwa kazi yake. Kujitolea kwa Yesu maana yake ni mtu anayetaka kuyafuata mapenzi ya Bwana. Utumishi unaopatikana kwa kujitoa kwa Bwana huleta utakatifu na sifa kwake. Uongozi wa kanisa unaweza kuwa mgumu, usiopendeza, usiotambuliwa au usio na mapato. Ingawa ni hivyo, kiongozi anayemtumikia Kristo atabaki kuwa mwaminifu.

4. Kanisa linawezaje kuwachagua viongozi wake?
   A. Uchaguzi umeelezwa na maneno ya Agano Jipya.
      1. "Kuitwa" (Matendo 13:2)

Huu ulikuwa uchaguzi wa Roho Mtakatifu. Hii ni hatua ya kwanza. Wote wanaitwa na Roho katika wokovu. Wote wanaitwa na Roho kukua katika imani. Wengine wameitwa katika huduma maalum. Mwito huu lazima uthibitishwe na kanisa. Walifanya hivyo kwa Paulo na Barnaba.

2. "Chagua" (Matendo 6:3)

Uchaguzi huu ni wa kanisa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Mungu hakemei uhuru ambao amewapa waamini. Hii hufuatana na uwezo ulioonekana katika maisha yake na haja za kanisa. Kumchagua kiongozi wa kanisa usiwe sawa na uchaguzi wa viongozi wa serikali. Mtu asigombanie kazi hiyo.

3. "Kuweka kando" (Matendo 14:23)

Wengine hufikiri ya kwamba Paulo na Barnaba waliwachagua na kuwaweka viongozi katika kanisa. Bila shaka waliwasaidia makanisa kuwatambua watu wema. Hata hivyo neno kutenga lilitumika kuwa na maana ya "kuchagua kupiga kura ya kuinua mikono." Wazo la kuchagua kwa kura ni sawa kulingana na kifungu hiki. Paulo na Barnaba walikuwa na busara. Walijua ya kwamba kanisa lingefuata kiongozi ambaye limechagua.

B. Uchaguzi hufanywa na kanisa likiongozwa na Roho Mtakatifu.

Wabátisti wanaamini kwa nguvu ya kwamba kanisa lina uwezo wa kuamua mapenzi ya Mungu kuhusu kumchagua mchungaji wake. Kanisa lifanye hivi linapotaka mchungaji. Kanisa lichague kamati. Kamati ijulishwe na kanisa ya kwamba wanataka kiongozi wa aina gani. Kamati imtafute kiongozi wa kupendekezwa kwa kanisa. Wampendekeze tu yule wanayefikiri ya kwamba ni mtu wa Mungu na mshiriki wa kanisa. Kanisa lizungumze naye kuhusu wokovu wake, mwito wake na maono yake kwa kanisa. Washiriki waombe ili wajue mapenzi ya Mungu. Baada ya hayo yote, washiriki wapige kura kama wanavyoamini ya kwamba Mungu anawataka kufanya.

C. Uchaguzi ufanywe kulingana na hitaji la kanisa.

Kanisa limchague kiongozi kulingana na hitaji. Haja inaweza kuwa ya kwamba wanahitaji mchungaji ambaye ni mwalimu mzuri. Wakati mwingine hitaji linaweza kuwa la mchungaji ambaye ni mwinjilisti mzuri. Kanisa lizungumze juu ya haja yake. Baada ya haja kukubaliwa, basi kamati ichaguliwe. Wamtafute kiongozi wa aina ile.

D. Uchaguzi ufanywe kulingana na uwezo wa Kibiblia.

Kanisa kila mara limchague kiongozi aliye na uwezo kulingana na mpango wa Biblia. Hiyo ni faida ya kanisa. Kanisa litakuwa na shida ikiwa litaangalia tu uwezo wa aina moja litakapokua likimchagua kiongozi. Inawezekana kumchagua mtu anayependwa na watu wote. Hata hivyo ikiwa si kiongozi wa kiroho anaweza kuwa kiongozi wa bure na asiye na maana. Ikiwa kanisa lingemchagua mtu aliye na wanawake wengi, wasishangae Mungu akikosa kuwabariki. Mchungaji ambaye hahitimu Kibiblia ataleta shida nyingi kwa kanisa. Kukataa kumkubali kiongozi wa namna hii ni rahisi kuliko kusuluhisha matatizo atakayoleta. Kuchagua elimu kuliko vipawa, kujulikana kuliko kiroho au kuonekana kimwili nje kuliko kuonekana kwa uwezo wa ndani huleta shida nyingi.

5. Je, mchungaji alipwe mshahara?

Mchungaji alipwe. Wachungaji wengi katika Afrika ni wakulima. Wengine wana kazi mbalimbali zinazowapa pesa za kuwasaidia kimaisha. Kwa sababu hiyo, washiriki hufikiri ya kwamba wachungaji wasilipwe kwa kuwa wana mapato. Wengine hufikiri ya kwamba kwa vile mchungaji anamfanyia Mungu kazi, basi na apate msaada (mshahara) kutoka kwa Mungu. Mchungaji kama washiriki wote hupata baraka kutoka kwa Mungu. Wakristo

wote humtumikia Mungu.

A. Mchungaji anahitaji kulipwa kwa sababu zifuatazo:

1) Ni mafundisho ya Biblia.

Yesu alisema "...maana mtenda kazi astahili posho lake" (Mathayo 10:10). Paulo akaandika "na Bwana vivyo hivyo ameamuru ya kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili" (I Wakorintho 9:14). Akaandika tena "mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote" (Wagalatia 6:6).

2) Ndivyo ilivyo.

Mtu ye yote ambaye ameajiriwa na mtu lazima alipwe kwa kazi yake. Inakubalika ya kwamba kampuni imlipe mwajiriwa wake. Kanisa hupokea faida ya kazi ya mchungaji. Wamemwomba awafanyie kazi. Inawapasa kumlipa mchungaji.

B. Mchungaji alipwe na kanisa analotumikia.

Kanisa hutaka mchungaji wake kuwatembelea wagonjwa, wapotevu na washiriki. Wanamtaka ahubiri na kufanya mipango ya Kanisa. Inampasa kufanyiza ama kufunganisha ndoa, kuongoza mazishi na mikutano mingine maalum. Inampasa atoe nafasi yake na kutumikia kanisa. Kwa vile kanisa linatazamia vitu hivi vyote linapaswa kumlipa na kumtegemeza mchungaji. Paulo alifundisha ya kwamba wale wanaopata faida ya mchungaji ni sharti wamlipe. Kuna shida iwapo mtu mwingine atamlipa mchungaji. Kuna sababu mbili. Sababu ya kwanza ni mfanya kazi hutaka kumpendeza mwajiri wake amlipaye. Ikiwa misheni, jumuiya au chama ndiyo humlipa mchungaji, inawezekana asione wajibu wake kwa kanisa. Ikiwa kundi lingine linamlipa mchungaji, kanisa hufikiri ya kwamba hawana wajibu wa kumlipa mchungaji wao. Makanisa fulani ya Kibatisti yamefuata mtindo wa madhehebu mengine kwa kuwalipa wachungaji wao. Makanisa mengine ya Kibatisti hutoa pesa zao kwa jumuiya au chama nao humlipa mchungaji. Jambo hilo humweka mchungaji katika matatizo. Kwa vile kanisa hufikiri ya kwamba mchungaji analipwa na jumuiya au chama, basi hawana wajibu wa kutoa. Na kanisa likikosa kutoa, basi jumuiya au chama hukosa pesa za kumlipa mchungaji. Fundisho hili la mtu mwingine kumlipa mchungaji wa kanisa si la Biblia. Hii ni shida hasa.

C. Mchungaji alipwe kila mara na kwa uzuri.

Kila kanisa likate shauri kuhusu mshahara wa mchungaji wake. Makanisa mengine humlipa mchungaji kulingana na asilimia ya mapato ya matoleo yao. Wengine hulipa kiasi cha kutosha kila juma au kila mwezi. Wengi wa wachungaji wa Kibatisti katika Afrika hutumika nusu kwa kanisa na nusu kwa kazi nyingine.

Mchungaji anaweza kuwa mkulima, mwalimu au mfanyi kazi katika serikali. Hupata mahitaji yake hasa kutoka kazi hizo. Kwa kufuata kanuni, inafaa mshahara wa mchungaji uwe karibu sawa na mapato ya watu wengine wa kawaida au washiriki.

Kanisa lianze kumlipa mchungaji mara tu anapoanza kazi yake. Kanisa limlipe kila juma au mwezi. Walipe kulingana na saa za kazi, uwezo wao wa kutoa na mahitaji yake. Zamani sana washiriki walikuwa wakimlipa mchungaji chakula kwa sababu ya uhaba wa fedha. Mchungaji ana matumizi ya fedha kama safari akiitumikia kanisa. Kanisa lilipe kwa matumizi haya. Kanisa lisiamini ya kwamba hiyo ni sehemu ya mshahara wa mchungaji. Mchungaji anapaswa kutoa fungu lake la kumi kwa kanisa.

6. Wabatisti wanaamini nini kuhusu kuwaweka viongozi wakfu?

Wakfu ni desturi ya kanisa ambayo inaweza kuleta matatizo. Desturi zingine ni tofauti kabisa na mafundisho ya Biblia.

A. Maana ya wakfu ni nini?

Neno, wakfu, halipatikani katika Agano Jipya. Neno ambalo limetafsiriwa kuwa wakfu lina maana ya kutenga au kuweka kando au kuchagua. Siku hizi maana ya neno hili ni kumtenga mtu kwa ajili ya kazi ambayo Mungu amemwitia kufanya. Wabatisti wanaamini ya kwamba kumweka mchungaji wakfu hakuna maana ya kumtenga kutoka kwa washiriki wake. Ni utambuzi wa mwito wake wa kiroho katika huduma yake. Hutambua vipawa vya kiroho ambavyo vimeonekana maishani mwake. Huonyesha ufahamu wake katika mambo ya kiroho na ya Kibiblia. Wakfu si tendo la kumpa mtu uwezo fulani au neema maalum. Ni utambuzi wa uwezo wa Mungu aliopewa. Wakfu si tendo la kanisa lenyewe. Wakfu si tendo la kumtenga mchungaji kutoka kwa washiriki wake. Ni tendo la kumweka mchungaji kando kwa ajili ya utumishi alioitiwa na Mungu.

B. Kuna mifano gani ya Kibiblia kuhusu wakfu?

Mathiya (Matendo 1:26) alitengwa kando kwa ajili ya kuwa mtume. Watu saba walitengwa kwa ajili ya kazi ya ushemasi (Matendo 6:1-7). Katika Matendo 13:3, Paulo na Barnaba walitengwa kwa ajili ya kaiz ya umisheni. Paulo akamkumbusha Timotheo kuhusu kuwekwa wakfu kwake na kazi yake (I Timotheo 4:14). Wazee katika Kanisa la Galatia (Matendo 14:23) Paulo, na Barnaba na makanisa waliwatenga.

C. Wakfu una maana gani katika kanisa la Kibatisti?

Wabatisti wanatambua umuhimu wa kuweka mtu wakfu kwa

ajili ya utumishi maalum. Wale tu walioonyesha ya kwamba wameitwa na Mungu na wawekwe wakfu. Wale walioitwa na Mungu watapewa vipawa na Roho Mtakatifu na watajua mambo ya kiroho. Wakfu ni katika uwezo wa uongozi wa Kanisa lenyewe la mahali fulani.

Katika wakfu wa mchungaji, wachungaji wengine wanaweza kualikwa wawe kamati ya kumpima huyu mchungaji. Wamwulize maswali. Wabatisti hawaamini ya kwamba wakfu ni kwa wachungaji pekee. Washiriki wa kanisa wawemo ndani ya kamati hii. Kamati iwe na hekima ya kutosha kumpima yule ambaye anawekwa wakfu. Baada ya maswali, kamati itaweka mapendekezo kwa kanisa. Nalo Kanisa litakata shauri la mwisho. Ikiwa kanisa limekata shauri kumweka wakfu mtu huyo, basi, kamati, itasaidia katika ibada na mkutano huo wa kumtenga mtumishi wa kanisa.

Wakfu huandamana pamoja na maombi kwa uongozi wa Mungu, baraka kwa mchungaji na kazi yake. Mashauri ya Kibiblia yenye kumhimiza atapewa na kamati pamoja na Kanisa lake. Atahitaji kusema habari za uongofu wake na mwito wake. Aulizwe maswali kuonyesha kukua kwake kiroho, vipawa vyake, mwito wake na ufahamu wake wa Ki4iblia. Kumwekea mikono ni thibitisho la huduma ya mwito wake aliopewa na Mungu.

Makanisa mengine, jumuiya na chama waambiwe jinsi kanisa lilivyofanya. Inawezekana anahitaji kuandikishwa katika serikali. Ikiwa hiyo itatakiwa, basi, itakipasa chama au jumuiya kuthibitisha jambo hilo kwa serikali.

7. Tumejifunza nini kuhusu uongozi wa Kanisa?

1. Kibiblia, wachungaji na mashemasi ni viongozi wa kanisa la mahali fulani.

2. Viongozi wa kanisa wawe wa kiroho, wenye busara na hekima na wenye kuheshimiwa.

3. Yawapasa viongozi wa Kanisa wawe watumishi waliojitolea kwa Kristo. Wawekwe wakfu kwa kazi, na wasitenganishe kutoka kwa Kanisa au washiriki.

4. Viongozi wachaguliwe na kanisa lenyewe chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, kulingana na haja ya kanisa na uwezo wao.

MUHTASARI
SOMO LA NANE

1. Utawala wa kanisa uwe wa kanisa lenyewe au uwe wa Afisi Kuu?
   A. Swali la utawala wa kanisa limekuwa swali kubwa la kihistoria.
   B. Utawala wa kanisa lenyewe la mahali ni wa washiriki wote.
   C. Utawala wa afisi kuu ni ule uongozi wa watu wachache walio ndani au nje ya kanisa wanaloliongoza.
   D. Wabatisti wanaanimi katika utawala wa kanisa wa washiriki.

2. Kanuni gani za Biblia ambazo zinaweza kufuatwa kwa kuchagua aina ya utawala wa kanisa?
   A. Udugu wa waamini ni fundisho la Agano Jipya.
   B. Mpango wa Mungu ni uhuru wa kiroho wa mwamini.

3. Je, kuna misaada yo yote ya kibiblia ya kusimamia dai hili la Kanisa kujitawala lenyewe?
   A. Kuna mifano ya Biblia ya washiriki wakikata mashauri.
   B. Jinsi neno, kanisa, lilivyotumiwa kwanza husaidia kueleza utawala wa kanisa kwa njia ya washiriki.

4. Je, kuna kanuni gani muhimu za utawala wa Kanisa la Kibatisti?
   A. Ushirika ni kwa hiari.
   B. Washiriki wote wako sawa mbele ya Mungu.
   C. Kanisa linahitai kuwa huru kutokana na nguvu na ulazimisho wa nje.

5. Kuna shida gani zinazotokea katika utawala wa Kanisa la Kibatisti?
   A. Mshiriki anaweza kutaka kulitawala kanisa.
   B. Wakati kila mmoja anapofanya kama apendavyo, basi hakuna utawala.
   C. Washiriki wanaweza kutaka wengine kuwatawalia kanisa lao.

6. Kuna kanuni muhimu kwa utawala wema wa kanisa ndani ya Kanisa la Kibatisti.
   A. Matumizi ya kamati mbalimbali ni busara.
   B. Kila mshiriki awemo katika majadiliano kabla ya shauri kukatwa.
   C. Kila mshiriki asaidie kanisa.

7. Tumejifunza nini kuhusu utawala wa Kanisa?

## SURA YA NANE
## UTAWALA WA KANISA

Ni utawala wa aina gani wa kanisa unaopatikana siku hizi? Kwa nini Wabatisti wamechagua kufuata utawala wa washiriki wa kanisa wenyewe? Kuna kanuni gani za Kibiblia na misaada tofauti inayohusu kanisa na utawala wake wa washiriki wenyewe? Hebu na tuyaangalie maswali haya.

Makundi yote, jamaa, shule, biashara, kanisa lazima wawe na utawala wa aina fulani. Kila kundi hutaka kufuata utawala unaolingana na jinsi wanavyoamini na wanavyotaka katika makusudi yao. Wabatisti huamini ya kwamba utawala wa kanisa lazima upate mafundisho ya Agano Jipya. Washiriki fulani wa kanisa la Kibatisti huweza kubadilisha aina ya utawala wao. Hao huwa bado hawajasoma vizuri kanuni za Biblia au historia ya Wabatisti. Yawezekana kuwa wanataka kufuata mifano ya madhehebu mengine. Kama vile imani ya Wabatisti ni muhimu, basi utawala wa kanisa lao ungekuwa mfano kwao.

1. Utawala wa kanisa uwe wa kanisa lenyewe au uwe wa Afisi Kuu?

Kuna mifano miwili ya aina ya utawala wa kanisa lenyewe au afisi kuu. Utawala wa washiriki wenyewe wa kanisa ni utawala wa kanisa lenyewe. Utawala wa watu wachache ndani au nje ya kanisa lenyewe ni utawala unaoongozwa na afisi kuu.

A. Swali la utawala wa kanisa limekuwa swali kubwa la kihistoria.

Katika Agano Jipya kila kanisa liliongozwa na washiriki wa kanisa hilo. Hapakuwa na uongozi wa afisi kuu uliotawala makanisa. Serikali ya Rumi ilikuwa ya utawala wa mambo yote kufanyiwa katika afisi moja kuu. Kwa kufuata matokeo hayo, hii ndiyo sababu iliyofanya makanisa kuiga utawala wa aina hiyo. Uongozi huo wa afisi kuu ukawa na nguvu zaidi kwa muda wa miaka mingi. Hata kukatokea wakati mmoja katika historia, kuwe na dhehebu moja kwa Wakristo wote ulimwenguni. Mnamo mwaka wa 1054, dhehebu hilo likagawanyika na kuwa madhehebu mawili yaani, dhehebu la Kikatoliki na la Kiorthodox (Roman Catholic and Greek Orthodox). Mojawapo ya sababu ya mgawanyiko ilikuwa inahusu utawala wa kanisa. Katika wakati wa matengenezo ya kanisa, hakuna kanisa lolote lililojiongoza lenyewe. Mafundisho ya Agano Jipya yalisahauliwa.

B. Utawala wa kanisa lenyewe la mahali ni wa washiriki wote.

1) Mafundisho ya Kibiblia husaidia kueleza utawala wa kanisa la mahali.

Makanisa ya Agano Jipya yalikuwa huru, washiriki walibatizwa baada ya kuamini kwao, na wakaongoza katika ushirika wao. Kila kanisa lilikuwa huru kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu kwa kanisa hilo. Viongozi hawakutenganishwa na washiriki. Kiongozi akawa mfano kwa mwamini au waamini. Waamini wote walikuwa sawa mbele ya Mungu. Makanisa yakafuata mafundisho ya mitume ambayo yamo katika Agano Jipya sasa. Wakategemea uongozi wa Roho Mtakatifu. Makanisa yakasaidiana na kufanya kazi pamoja. Walikuwa na umoja wa kiroho katika Kristo. Kwa hivyo, walichotaka tu ni utawala wa Kanisa la mahali.

2) Nguvu za utawala wa kanisa la mahali ni:

(a) Utawala wa kibiblia. Makanisa ya Agano Jipya yakajitawala.

(b) Kanisa kuwa zaidi chini ya uongozi wa Kristo. Huo basi ni "utawala wa Mungu." Neno la kiingereza "Theocracy" lina maana ya utawala wa Mungu. Roho Mtakatifu huliongoza kanisa katika ukweli uliopatikana katika maandiko matakatifu.

(c) Hufuata mafundisho fulani muhimu ya Agano Jipya. Umoja wa waamini, usawa mbele ya Mungu, na uhuru wa kiroho ndani ya Kristo huheshimiwa katika utawala wa kanisa la mahali.

(d) Huwaheshimu waamini. Utawala wa kanisa la mahali maana yake ni kila Mkristo anaweza kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu. Heshima hii ya mwamini hufuata kanuni au imani ya ukuhani wa mwamini.

(e) Hulipa kanisa uhuru wa kufuata mapenzi ya Mungu. Maana yake ni kwamba kanisa liko huru kufuata na kukata shauri kwamba mapenzi ya Mungu ni nini. Kanisa lina wajibu wa kufuata mapenzi yake pekee.

3) Udhaifu wa utawala wa kanisa la mahali ni:

(a) Kunaweza kuwako na ukosefu wa ushirika na makanisa mengine. Wakristo wanahitaji ushirika vivyo hivyo.

(b) Kunaweza kuwako ukosefu wa umoja na makanisa mengine. Kuna nguvu katika umoja. Makanisa yana umoja katika Kristo. Kwa hivyo kuna hamu kubwa kwa waamini wengine na makanisa vile vile.

C. Utawala wa afisi kuu ni ule uongozi wa watu wachache walio ndani au nje ya kanisa wanaloliongoza.

1) Utawala wa afisi kuu ulitokea baada ya kuandikwa kwa Agano Jipya.

Uongozi huu wa kufuata mfano wa utawala wa serikali

ya Kirumi ulijitokeza katika karne ya pili. Kama tulivyoona kwamba utawala huo wa afisi kuu ulipata kuwa wa naguvu sana. Viongozi wakawa mbali na washiriki. Viongozi wakatawala uongozi wa kanisa. Washiriki wa kanisa hawakuruhusiwa kujiingiza katika utawala wa kanisa. Uongozi ulikuwa tu kwa wale walioelimishwa.

2) Nguvu za uongozi wa makanisa wa afisi kuu ni:

(a) Kuna nia ya umoja na ushirikiano. Uongozi huu ukiwa ni wa kundi la wenyeji, huwako na nia ya umoja na ushirikiano.

(b) Uongozi wa aina hii huwapa nafasi viongozi waliosoma kujitolea kwa saa zao zote kufanya kazi hiyo.

3. Udhaifu wa uongozi wa makanisa wa ofisi kuu ni:

a. Uongozi huu hauna msingi wa nguvu katika mafundisho ya Kibiblia.

b. Uongozi huu unaweza kukosa mahitaji na matakwa ya kanisa la mahali.

c. Wale walio katika uongozi wanaweza kuwazuia wengine wasiwe viongozi.

d. Huweza kuzuia maendeleo ya upesi ya Kanisa.

e. Huweza kuwa utaratibu au ushirika zaidi kuliko kuwa mwili wa kiroho.

4. Ifuatayo ni mifano mitatu ya uongozi au utawala wa afisi kuu.

Madhehebu yafuatayo matatu ni mfano wa yale yanayotumia mwongozo wa kufuata afisi kuu. Madhehebu mengine yana mpango wa uongozi ulio sawa na huu. Mengine baadhi yao yameanza kuwapa washiriki uhuru wao.

a. Kanisa la Kikatoliki mwongozo wao ni ule wa afisi kuu kukata mashauri. Baba Mtakatifu hufikiriwa kuwa mwakilishi wa Kristo hapa duniani. Hushirikiana na maaskofu katika uongozi wake. Hata hivyo, kulingana na imani yao, Baba Mtakatifu anaweza kusema kwa ajili ya Kristo. Na makundi ya makanisa hutawaliwa na maaskofu wake. Kanisa lina uhuru fulani mahali pao. Na ijapokuwa lina uhuru, haliwezi kupinga matakwa ya askofu wake. Kwa kawaida huwa na maaskofu wachache tu wa kuongoza makanisa mengi nchini. Mtu akisha chaguliwa kuwa askofu, huendelea kuwa askofu mpaka atakapofikia umri wa kupumzishwa, kifo au kuondolewa katika cheo hicho.

b. Kanisa la Uingereza pia linafuata mwongozo huu wa askofu sawasawa na kanisa la Kikatoliki la Roma. Mahali pao pakuu pa utawala wa kanisa ni Uingereza na mkuu wao huishi pale. Mtu huyu

hutoa mamlaka kwa kanisa kwa njia ya maaskofu. Makundi yao yana uhuru zaidi kuliko Wakatoliki.

c. Kanisa la Scotland au Kanisa la Presbyteria linaongozwa pia katika njia ya utawala wa afisi kuu. Wana kundi la wazee katika makundi ya makanisa ambao huongoza mambo mengi Kanisani. Huwako basi na Kusanyiko Kuu ambapo wazee huja kutoka makundi mbalimbali ya makanisa kukata mashauri ya dhehebu lote kwa jumla. Utawala wao ni wa wajumbe wateule. Washiriki huwapa wajumbe wao ujumbe wao kwa utawala wa kanisa kupeleka katika baraza kuu.

d. Wabatisti wanaamini katika utawala wa kanisa wa washiriki. Wabatisti hufundisha hitaji la kufuata mafundisho ya Agano Jipya. Mafundisho haya hutegemea utawala wa Kanisa kwa njia ya washiriki wenyewe. Wabatisti hupinga usimamizi wa nguvu kwa kanisa. Hata hivyo, Wabatisti hujaribu kuondoa tatizo hili kwa kufanya kazi pamoja katika jumuiya ya sehemu na ya nchi nzima. Makundi au vyama hivi vya Kibatisti hupewa uhuru wa ushirika, umoja na nguvu katika uinjilisti. Vyama hivi havina mamlaka juu ya Kanisa la mahali fulani. Makanisa hutiwa moyo badala ya kutawaliwa. Wanaweza kuuliza au kuomba lakini hawawezi kuwaambia kanisa jambo la kufanya. Kanisa la mahali fulani hujitawala lenyewe. Utawala huu mara nyingine huitwa demokrasia.

Demokrasia maana yake ni "utawala wa watu wenyewe." Katika utawala huu wa kanisa, kundi lenyewe hujitawala. Maana yake ni, kila mwanachama hushiriki katika kukata mashauri. Kama iwezekanavyo, kila mshiriki huwa sehemu ya utawala wa Kanisa. Kanisa hutawaliwa na washiriki wenyewe wakiongozwa na roho wa Kristo.

Kanisa la Kibatisti litapokea maoni kutoka kwa jumuiya ndogo ya eneo au ya nchi nzima. Hivyo basi, kanisa hukataa kutotoa uhuru na wajibu wao wa kujitawala wenyewe. Katika utawala wa aina hii, makanisa yana wajibu wa kuunda dhehebu. Na kwa njia hii, makanisa huwa na uhuru wa kutotawaliwa na dhehebu ila utawala ule mwingine ambao tumekwisha zungumza hapo mbeleni.

Kuna makanisa mengi ya Kibatisti. Hakuna kanisa moja tu la Kibatisti linalokusudiwa kuwa la nchi nzima. Nchi huwa na jumuiya au ushirika wa Kibatisti. Kanisa la Kibatisti ni kanisa la mahali fulani.

Katika nchi ambazo kazi huwa ni mpya, baadhi ya Wabatisti hutamani utawala wa afisi kuu ya kanisa. Hii ni kwa sababu wengi hawajaona utawala wa kanisa la mahali fulani. Wanaishi katika nchi ambayo ina utawala wa nguvu wa afisi kuu ya serikali. Wanajua madhehebu mengine yaliyo na utawala wa nguvu wa afisi kuu. Wengine wana mipango ya jumuiya au chama kikuu kuwalipa wachungaji mishahara. Wengine hufikiri ya kwamba kamati ya utendaji (E.C.) ya jumuiya ndogo au jumuiya kuu ina mamlaka juu ya kanisa. Makanisa fulani huruhusu kamati ya kanisa kukata mashauri yote ya kanisa. Mifano hii husahau mafundisho makuu ya Biblia. Kanisa la Agano Jipya - ni lile ambalo linafuata kanuni za mafundisho ya Agano Jipya. Utawala wa kanisa la Kibatisti wanapaswa kuwa mfano na kielelezo cha imani na matendo ya Wabatisti.

2. Kanuni gani za Biblia ambazo zinaweza kufuatwa kwa kuchagua aina ya utawala wa kanisa?

Agano Jipya haitoi mfano hasa wa kufuatwa katika utawala wa kanisa. Hii yaweza kuwa ndiyo sababu ya kuweko kwa utawala mbalimbali makanisani siku hizi. Wabatisti huamini ya kwamba utawala wa kanisa likiongozwa na washiriki wenyewe ni wa Biblia, na husaidiwa na mafundisho ya Agano Jipya.

A. Udugu wa waamini ni fundisho la Agano Jipya.

Kanisa ni ushirika wa washiriki waliozaliwa mara ya pili. Ni washiriki wa jamaa ya kiroho. Wao wakiwa jamaa moja, wana usawa mbele ya Mungu Baba katika nafasi na wajibu wao. "Mungu haonyeshi upendeleo" (Warumi 2:11). Agano Jipya hufundisha ya kwamba washiriki wa jamaa hii wana vipawa tofauti vya kiroho.

Vipawa hivi ni kwa kumtumikia Mungu. Vipawa havionyeshi ukuu wa mtu katika kanisa. Wakristo hutegemeana. Yesu alifundisha ya kwamba waamini ni watumishi na wala si mabwana.

B. Mpango wa Mungu ni uhuru wa kiroho wa mwamini.

Mungu katika mpango wake alimpatia kila mwamini uhuru wa kiroho. Aliwaheshimu watu kwa kuwa na njia ya uhuru na kuchagua. Kanisa lisitumie utawala wa kanisa ambao ni kinyume cha mpango wa Mungu. Hii haina maana ya kwamba Mkristo asifanye apendavyo. Kila mtu ana wajibu kwa Mungu katika uhuru huo. Kanisa laweza kumchagua kiongozi aliyeelimika. Hata hivyo, elimu haiwezi kumpa mtu haki ya kuwatawala wengine. Kila mshiriki ana uhuru wa haki ya kukata shauri kuhusu mapenzi ya Mungu kwa maisha yake. Usawa na uhuru ni msingi wa demokrasia.

3. Je, kuna misaada yo yote ya kibiblia ya kusimamia dai hili la Kanisa kujitawala lenyewe?

A. Kuna mifano ya Biblia ya washiriki wakikata mashauri.

Katika Matendo ya Mitume 6, Kanisa la Yerusalemu likakata shauri kuwachagua watu saba wafanye kazi ya ushemasi. Mitume waliomba msaada kwa kanisa kufanya hivyo. Waliomba kanisa kuwachagua watu wema wasaidie katika utumishi wa kanisa. Kanisa katika Antiokia (Matendo 13) waliwatuma Paulo na Barnaba nje katika kazi ya umisheni wakiwa wamisheni. Paulo na Barnaba wakarudi katika kanisa hili kutoa taarifa au ripoti ya kazi yao. Kanisa katika Yerusalemu lilikutana kuzungumzia juu ya hali ya wokovu wa watu wa mataifa. Katika Matendo 15:22a twasoma "....ilionekana kuwa nzuri kwa mitume na wazee pamoja na kanisa lote...."

B. Jinsi neno, kanisa, lilivyotumiwa kwanza husaidia kueleza utawala wa kanisa kwa njia ya washiriki.

Neno kanisa hapo kwanza, lilitumiwa kwa kusema utawala wa kusanyiko la Waathene. Washiriki kwa kusanyiko walikuwa wakaazi wa mji wa Athene walio huru. Wananchi hawa huru wakafanya mashauri ya mji wao na usawa wa uhuru wenye madaraka ukawa ndio msingi wa demokrasia yao. Wayunani walianza utawala wa raia mapema kabla ya Kristo kuja. Warumi walikuwa na serikali ya utawala wa afisi kuu ambayo mfalme au mtawala alikuwa na uwezo mkuu. Serikali hii ya Kirumi ilianza kuvutia serikali ya Kanisa kufuata mpango huo wao mnamo miaka mia moja baada ya Kristo. Tangu matengenezo ya Kanisa, makanisa yakaanza kufuata tawala mbali mbali za Kanisa. Wabatisti huamini ya kwamba utawala wa kanisa lazima ufuate mafundisho ya Agano Jipya. Usawa na uhuru wa wajibu ni mafundisho muhimu.

4. Je, kuna kanuni gani muhimu za utawala wa Kanisa la Kibatisti?

A. Ushirika ni kwa hiari.

Ushirika kwa kawaida ni jambo la hiari ya mtu. Mtu huwa na ushirika tu akiomba kushiriki. Ikiwa ameokoka na kubatizwa Kibiblia, basi anaweza kuwa mshiriki akiomba. Mtu anapaswa kutubu dhambi zake, amwamini Kristo, halafu achague kubatizwa na kuwa mshiriki wa kanisa. Wabatisti hawaamini ya kwamba ni vyema kubatiza watoto wachanga. Wanapinga imani ya kumlazimisha mtu afanye kitu ambacho kwa hiari yake mwenyewe hajataka kufanya. Mshiriki halazimishwi kujiunga na Kanisa la Kibatisti. Yu mshiriki kwa sababu ya pendo la uchaguzi wake wa hiari.

B. Washiriki wote wako sawa mbele ya Mungu.

Hakuna sheria katika Kanisa la Kidemokrasia. Washiriki wote wako sawa mbele ya Mungu. Wana nafasi na wajibu. Wana wajibu kwa Mungu kutumia vipawa vyao katika kazi ya kulisaidia kanisa. Wote, yaani viongozi na washiriki ni sawa mbele ya Mungu. Wanapaswa kuwa waaminifu katika kazi ambayo Mungu amewataka kufanya. Viongozi wamewapa washiriki madaraka katika kanisa. Kiongozi aliye mwaminifu kwa Mungu ataaminiwa na washiriki. Kiongozi asiye mwaminifu hataaminiwa na washiriki. Washiriki wote ni watumishi ambao ni lazima wawe waaminifu kwa Mungu. Kila mshiriki atumiaye maneno ya utu uzima, na vitendo vya uzima, hupewa heshima na washiriki wengine. Kama ilivyoandikwa Kibiblia katika Yakobo 2:1-13, washiriki wana makosa wakionyesha migawanyiko na upendeleo.

C. Kanisa linahitaji kuwa huru kutokana na nguvu na ulazimisho wa nje.

Kanisa la Kibatisti ni ushirika unaojitawala. Kanisa la Kibatisti hujiongoza lenyewe. Wabatisti hupinga kabisa utawala utokao nje ya kanisa lenyewe. Kanisa litafanya kazi pamoja na makanisa mengine. Ingawa hivyo, halitalazimishwa. Halitawekwa katika hali ya lazima kufanya kitu ambacho halijakata shauri la hiari kufanya. Wabatisti waliwahi kufungwa jela kwa sababu ya kutotaka kulazimishwa. Walikataa kufanya yale ambayo walijua kuwa si mapenzi ya Mungu. Kristo ni nguvu na amri ya pekee kwa kanisa. Kamati, jumuiya ya eneo au ya nchi au chama havina amri juu ya kanisa. Biblia ni kiongozi wa imani, matendo, na hali zote za Wakristo na makanisa. Kanisa hufanya kazi pamoja na makanisa mengine katika jumuiya ya eneo. Hufanya kazi pamoja na makanisa mengine katika nchi nzima kwa njia ya jumuiya au chama cha nchi. Hivi vyama havina utawala juu ya kanisa la mahali. Wao hupendekeza mashauri, mipango na matendo. Ni juu ya kanisa kukata shauri kama mapendekezo hayo ni kufuatana na mapenzi ya Mungu. Katika roho wa uhuru, udugu wa Kikristo na umoja wa Roho, Wabatisti wanajulikana kwa kufanya kazi pamoja. Kutumia uhuru wetu wa kufanya kazi pamoja huonyesha Ukristo wetu zaidi kuliko kupigana wenyewe kwa wenyewe.

5. Kuna shida gani zinazotokea katika utawala wa Kanisa la Kibatisti?

A. Mshiriki anaweza kutaka kulitawala kanisa.

Utawala wa Kanisa la Kibatisti ni kwa washiriki wote. Katika uhuru wa namna hii hutokea mara kwa mara mtu anayetaka kutawala kanisa. Hii hufanyika wakati kuna mtu mwenye nguvu na uwezo na washiriki huogopa kumpinga. Kwa kuzuia shida hii, ni lazima Kanisa likubali kushika wajibu wa uhuru wao usiharibiwe.

Kumwambia mtu kama huyo kwamba si vizuri kutawala Kanisa si jambo rahisi. Yesu hakusema ya kwamba mambo ya muhimu yatakuwa rahisi.

B. Wakati kila mmoja anapofanya kama apendavyo, basi hakuna utawala.

Ingawa hivyo watu wengine hufikiri ya kwamba demokrasia ni sawa na Waamuzi 21:25 "siku hizo hapakuwa na mema machoni pake mwenyewe." Demokrasia ya Kanisa la Kibatisti si kwamba kila mshiriki afanye apendavyo mwenyewe. Je, utumwa hufanya apendavyo? Hapana. Paulo alijiita mtumwa wa Kristo. Je, maana yake ni kwamba Paulo alifanya alivyotaka au alifanya kama Kristo alivyomtaka afanye? Ukweli ni kwamba Paulo alifanya kama Kristo alivyotaka afanye. Waamini siku hizi ni lazima wafanye mapenzi ya aliyewaokoa. Ikiwa Kristo anaongoza ushirika, je, kutawako kutoelewana? Hakutakuwako ikiwa Kristo hasa anaongoza.

C. Washiriki wanaweza kutaka wengine kuwatawalia kanisa lao.

Kuna washiriki ambao wanaona furaha watu wengine kuwakatia mashauri. Uhuru maana yake ni kazi. Wengi hukataa kupokea madaraka. Mambo haya hufanyika katika makanisa fulani ya Kibatisti. Washiriki wanaweza kuachia kamati kukata mashauri na kuyatekeleza. Wanaweza pia kuwaachia kamati ya utendaji ya jumuiya ya eneo au ya nchi au chama kukata mashauri ya Kanisa lao. Wakati ambapo Kanisa hukataa madaraka yao basi hupoteza uhuru wao pia.

6. Kuna kanuni muhimu kwa utawala wema wa kanisa ndani ya Kanisa la Kibatisti.

A. Matumizi ya kamati mbalimbali ni busara.

Kanisa la Kibatisti hutumia kamati mbalimbali katika kutenda kazi. Kanisa bado litakuwa likijitawala hata wakati wa kuchagua kamati hizo. Kanisa huipa kamati mamlaka ya kazi zinazotakiwa kufanywa. Kamati yaweza kulisaidia kanisa kwa kushika wajibu wake juu ya mambo yatakiwayo. Kwa mfano kanisa linaweza kuhitaji kamati ya ujenzi au kamati ya fedha. Kamati huleta mapendekezo yake yote kwa kanisa ili shauri likatwe. Kamati isikatae mamlaka ambayo imepewa. Ikiwa itakataa basi kanisa lisimamishe shughuli hiyo au liwachague wanakamati wengine kuchukua mahali pao.

B. Kila mshiriki awemo katika majadiliano kabla ya shauri kukatwa.

Katika Afrika, mashauri mengi hukatwa katika mapatano ya

kawaida. Wakati ambapo kanisa linakataa shauri, washiriki wote waombwe kushiriki katika mashauri hayo. Kama vile kila mshiriki apatavyo nafasi ya kushiriki kwa kuona mapenzi ya Mungu yalivyo, basi kanisa lote likate shauri jinsi ya kufanya. Kila mshiriki ahudhurie mkutano wa aina hiyo. Kiongozi ajaribu awezavyo kumpa kila mshiriki nafasi ya kusema maoni yake, haidhuru umri na hali ya mshiriki huyo. Kundi liwakataze watu wachache kutawala mazungumzo. Mkutano kama huo mara nyingi hutumia muda mwingi, lakini hiyo ndiyo njia bora ya kukata shauri.

C. Kila mshiriki asaidie kanisa.

Mungu hutazamia mshiriki kuja kufanya kazi. Roho wake humpa kila mwamini kipawa cha kiroho kwa manufaa ya Kanisa (I Petro 4:10). Kila mshiriki na awemo katika maendeleo ya kazi ya kanisa ambayo ni kazi ya Bwana. Kila mshiriki awe akitafuta mapenzi ya Mwana wa Mungu. Kanisa liwatazamie washiriki wake kukua kiroho na kuwa wanafunzi. Kanisa litazamie kutoka kwa washiriki wake mambo yale ambayo Mungu anawatazamia.

7. Tumejifunza nini kuhusu utawala wa Kanisa?

1. Utawala wa kanisa lenyewe la mahali fulani na wa washiriki wenyewe unakubaliana na kanuni za Kibiblia.

2. Wabatisti wanaamini katika usawa, uhuru, na madaraka au wajibu katika utawala wa kanisa.

3. Kuna kanuni tatu ambazo Wabatisti wanatumia katika utawala wa kanisa. Kanuni hizo ni ushirika wa hiari, ushirika wa usawa wa nafasi na wajibu mbele za Mungu, na uhuru kutokana na lazimisho lo lote.

4. Watu huleta shida kwa utawala wa Kanisa la Kibatisti. Wengine hutaka wenyewe kulitawala kanisa. Wengine hutaka kufanya wapendavyo wenyewe. Na wengine hutaka watu wengine wawatawalie na kuwaongozea kanisa.

5. Utawala wa kanisa kwa njia ya ushiriki utumie kamati mbalimbali. Kila mshiriki aruhusiwe kutoa mashauri yake kabla ya kukata shauri, na kila mshiriki atazamiwe kusaidia kanisa.

## MUHTASARI
## SOMO LA TISA

1. Kanisa la Kibatisti hufanya kazi na makanisa mengine?
   A. Je, kuna mifano yo yote ya Biblia ya kufuata?
   B. Jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni nini?
      1) "...Muungano wa makanisa..."
      2) "...Walio na Imani na matendo yanayofanana..."
      3) "...Waliojiunga pamoja kwa hiari..."
      4) "...Kwa ushirika na utumishi..."
      5) "...Kwa utukufu wa Mungu..."
   C. Je, ni kanuni zipi ambazo huhimiza makanisa kufanya kazi pamoja?
      1) Kutegemea na kujitegemea ni muhimu.
      2) Kufanya kazi pamoja ni kuleta uhai kwa madhehebu.
      3) Uchaguzi wa hiari wa kufanya pamoja unafaa.
      4) Haki ya wengine ni lazima itambuliwe.
   D. Kusudi la jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni nini?
   E. Ni nani wanaoweza kuwa washiriki wa jumuiya ya eneo au ya nchi au chama?
   F. Unaweza kuchora namna gani picha ya jumuiya ya eneo?
      1) Picha ya makanisa yaliyo huru, yakitegemea na kutegemeana.
      2) Picha ya wazo kosefu la jumuiya.
   G. Jumuiya ya eneo au jumuiya ya nchi hufanya kazi kwa njia gani?
      1) Kazi ya viongozi ni nini?
      2) Kazi ya kamati ya utendaji ni nini?
   H. Je, jumuiya ya eneo na jumuiya ya nchi ni vyama tofauti vinavyojitegemea?

2. Je, Wabatisti wafanya kazi na madhehebu mengine?
   A. Muungano unaolisaidia kanisa kutimiza kusudi lake ni mzuri.
   B. Muungano una matokeo ya kusahihishwa.
   C. Muungano unaweza kuwa ushuhuda mwema kwa wasio Wakristo katika jamii.

3. Kanisa liwe na uhusiano gani na serikali ya taifa?
   A. Wazo la kanuni kamili ni:
      1) Kanisa huru.
      2) Taifa huru.
      3) Utengano baina ya kanisa na serikali ya taifa.
   B. Mambo yanayohusu kanisa na serikali pamoja ni:
      1) Utulivu katika nchi.
      2) Mambo yanayohusu hali ya watu.
      3) Uaminifu na uadilifu katika wafanya kazi wa serikali.
   C. Wakristo wana wajibu kwa serikali yao.

4. Tumejifunza nini kuhusu uhusiano wa kanisa?

## SURA YA TISA
## UHUSIANO WA KANISA

Ikiwa kanisa lina uhuru, basi, kwa nini lihusiane na makanisa mengine? Jumuiya ya eneo na jumuiya ya nchi na chama ni nini? Kanuni za makanisa kufanya kazi pamoja ni zipi? Je, Wabatisti wafanye kazi pamoja na madhehebu mengine? Uhusiano wa kanisa na serikali ya nchi uwe namna gani? Hebu na tuyaangalie maswali haya.

Mshiriki Mbatisti na kanisa nzima ni huru tena si huru. Kuwa huru maana yake ni, Wabatisti wana uhuru na wajibu mbele ya Kristo. Hawana uhuru maana yake ni, Wabatisti wanategemeana. Wakristo na makanisa hawako huru kwa sababu hawajitoshelezi wenyewe kikamilifu. Paulo anatumia mfano wa mwili kwa kufundisha kanuni hii (I Wakorintho 12:14-26; Waefeso 4:15-16). Mkristo au kanisa liko sawa kabisa kujiunga na wengine kumtumikia Mungu. Kanisa lina wajibu wa kuwaongoza wengine kwa Yesu na kumjenga mwamini katika imani yake.

1. Kanisa la Kibatisti hufanya kazi na makanisa mengine?

Kwa kawaida makanisa ya Kibatisti hufanya kazi pamoja katika jumuiya ya eneo, jumuiya ya nchi na katika mwungano/chama. Hebu na tuchunguze wazo hilo kwa makini.

A. Je, kuna mifano yo yote ya Biblia ya kufuata?

Hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo tunaweza kupata maneno haya - jumuiya ya eneo, jumuiya ya nchi na ya muungano. Katika Agano Jipya kanisa lilikuwa bado halijaanzisha mojawapo ya majina haya. Hakuna utawala kamili hasa wa kanisa katika Agano Jipya ambao unaweza kutumiwa kama kielelezo. Hivyo basi hatuwezi kupata njia kamili ya kuweza kufanya kazi pamoja na makanisa mengine. Kuna maandiko fulani ambayo yanaonyesha vile kanisa lilivyosaidia kanisa lingine. Matendo ya mitume 15, Kanisa la Antiokia likataka mashauri ya Kanisa la Yerusalemu. Paulo katika Wagalatia 2:1-10 akataka kuchunguza ujumbe wake na wa wengine. Antiokia wakasaidia Yuda na shida ya njaa iliyowapata (Matendo 11:27-30). Hili likawa jibu la Kanisa moja kwa lingine. Katika I Wakorintho 16:1-4; 2 Wakorintho 9:1-5, makanisa ya mataifa yakatoa msaada kuwasaidia Wakristo wa Yerusalemu.

B. Jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni nini?

Elezo moja laweza kutumiwa kuyaeleza majina hayo yote. Tofauti iliyoko kati ya jumuiya ya eneo na jumuiya ya nchi na ya muungano ni kuhusu ukubwa wa sehemu ya kazi yenyewe. Jumuiya

ndogo ni ya eneo fulani tu, kama wilaya. Jumuiya kuu ni ya nchi nzima, ya muungano wa makanisa yote nchini. Hii ni sawasawa na chama. Kwa hivyo, jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni muungano wa makanisa yaliyo na imani moja, matendo yaliyo sawa, na wamekuja au kuungana pamoja kumtumikia na kumtukuza Mungu. Hebu tuichunguze kanuni hiyo ili tuweze kuielewa vizuri:

1)"...Muungano wa makanisa...."

Jumuiya ya makanisa ni tofauti na kundi la chama cha wafanya kazi kilichoundwa na watu binafsi. Vikundi kama hivyo huundwa na kuendelezwa kwa makusudi ya kuleta faida kwa kila mtu aliye mwanachama. Jumuiya ya eneo la Wabatisti ni makanisa. Jumuiya huundwa kwa makusudi ya kusaidia wengine wala si kuwapa watu kazi na kwa faida ya watu. Jumuiya ya eneo la makanisa ya Kibatisti yana makusudi ya kiroho.

2)"...Walio na Imani na matendo yanayofanana..."

Jumuiya ni ya makanisa ya Kibatisti. Siyo jumuiya ya madhehebu yote. Ni jumuiya ya watu walio na imani sawa, matendo sawa na desturi sawa. Kwa kawaida jumuiya ya eneo huwapokea tu wale wenye imani, desturi na matendo yaliyo sawa na yao wenyewe. Makanisa ya Wabatisti huamini Biblia kuwa ndiyo yenye mamlaka ya mwisho kwa mambo ya imani. Wanaamini katika ubwana wa Kristo, wokovu kwa neema katika njia ya imani na huamini pia katika ukuhani wa waamini. Wanawabatiza tu waamini kwa njia ya uzamisho, ushirika wa usawa na uhuru kwa hiari, uhuru na madaraka au wajibu na uinjilisti.

3)"...Waliojiunga pamoja kwa hiari..."

Jumuiya ya eneo huanza wakati ule makanisa yanapokata shauri kwa hiari kujiunga pamoja. Kila kanisa hukata shauri kujiunga na makanisa mengine. Wakristo na makanisa wasilazimishwe kujiunga. Kujiunga kuwe tendo la hiari. Kanisa lisilazimishwe kujiunga na jumuiya au chama cho chote.

4)"...Kwa ushirika na utumishi..."

Jumuiya ya eneo hutekeleza wajibu wa ushirikiano kati ya makanisa. Ushirika huu huongeza nguvu katika kazi ya Mungu. Jumuiya huyasaidia makanisa kukua. Katika ushirikiano pamoja na makanisa mengine, kanisa laweza kukua kwa njia ya uinjilisti na umisheni. Kwaweza kupatikana ujuzi wa makanisa kwa wingi wa idadi. Shule ya Biblia ya pamoja yaweza kuyasaidia makanisa kukua katika kazi ya Mungu. Katika ushirikiano, jumuiya hufanyika kuwa chombo cha kuyakuza makanisa katika huduma yao kwa wenzao.

5)"...Kwa utukufu wa Mungu...."

Wakristo wote wangekuwa na nia ya kuleta utukufu kwa Mungu. Makanisa, jumuiya za eneo, jumuiya za nchi, na vyama vinapaswa kuwako kumtukuza Mungu. Zote huwapo kwa ajili ya utukufu wa Mungu wala si kwa faida yao. Hii ndiyo sababu jumuiya ya Wabatisti ni tofauti na zile za ulimwengu. Jumuiya ya ulimwengu huanza na faida na sababu za watu wenyewe. Jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni lazima kuonyesha upendo wa Mungu.

C. Je, ni kanuni zipi ambazo huhimiza makanisa kufanya kazi pamoja?

1) Kutegemea na kujitegemea ni muhimu.

Kutegemewa na kuwategemea wengine sharti kuwepo. Kwa hivyo ni kutegemeana. Kujitegemea ni kufanya mapenzi ya Mungu kama unavyoona unaongozwa kufanya katika uhuru wako. Kujitegemea au uhuru uletao migawanyiko si wa kibiblia. Wakristo wako huru lakini wanaambiwa kujitoa kila mtu kwa mwenzake. Hii ni kweli kwa makanisa na kwa Wakristo vile vile. Uwezo wa kila Mkristo huwasaidia wengine kulingana na vipawa vyake. Kila kanisa husaidiana na makanisa mengine.

2) Kufanya kazi pamoja ni kuleta uhai kwa madhehebu.

Makanisa hufanya kazi pamoja kwa kueneza injili na kufanya hivyo ni kuwa katika roho wa Kristo. Makanisa yanapofanya hivyo pamoja husaidiana katika kusudi la kukuza ufalme wa Mungu. Kufanya pamoja kunategemea uhuru wa kila kundi katika ushirika.

3) Uchaguzi wa hiari wa kufanya pamoja unafaa.

Imani ya Mkristo ni lazima iwe huru mbali na kulazimishwa (yaani, "coercion"). Neno hili maana yake ni kumlazimisha mtu afanye jambo ambalo hakulichagua kufanya kwa hiari yake. Neno hili linatukana uhuru aliopewa mtu na Mungu. Yesu aliwakataza wanafunzi wake kumlazimisha mtu ambaye alikataa kufuatana nao (Luka 9:49-50). Katika historia ya Kikristo watu fulani waliwalazimisha watu wengine kuamini kama walivyoamini. Wabatisti wanaamini ya kwamba ushirika wa kanisa ni wa hiari. Ushirika wo wote katika kanisa, jumuiya au chama lazima uwe wa hiari.

4) Haki ya wengine ni lazima itambuliwe.

Haki ya wengine lazima itambuliwe. Haki isipolindwa, wale wachache wenye nguvu hulazimisha wengine wasio na nguvu kufuata mashauri yao. Si rahisi kufikiri ya kwamba wachache sio sawa au wamekosa. Wabatisti huheshimu haki ya wengine. Kanisa

lo lote au jumuiya au chama wanaweza kuondoa uanachama wao katika kundi. Hii hufanyika wakati ambapo kundi fulani hukataa mafundisho ya Biblia na desturi ya Wabatisti. Kwa vyo vyote watu fulani wachache wasiwalazimishe wengine.

D. Kusudi la jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ni nini?

Wabatisti huamini ya kwamba makanisa ya jumuiya au chama na jumuiya ya eneo ndiyo dhehebu. Madhehebu huwako kwa kusudi la kuyasaidia makanisa kutimiza makusudi yao. Makanisa nayo husaidia kazi ya jumuiya au chama au jumuiya ya eneo katika kufanya kazi ya kueneza injili. Jumuiya nazo kutafuta njia za kuyatimiza mahitaji haya ya makanisa. Makanisa yanahitaji ushirika, kanuni ya kuwatambulisha, umisheni wa kuwaendea watu nje, elimu na maendeleo ya Kanisa.


E. Ni nani wanaoweza kuwa washiriki wa jumuiya ya eneo au ya nchi au chama?

Washiriki wa jumuiya au chama ni makanisa. Makanisa haya kwa kupenda kwao na kwa hiari .yao hukata shauri la kufanya kazi pamoja na makanisa mengine ya Kibatisti katika muungano wa jumuiya. Kanisa linaweza kushiriki katika jumuiya ya eneo, ya nchi na katika chama pia. Jumuiya ya eneo na ya nchi ni makundi mawili tofauti. Wanahusika na kila moja kwa sababu makanisa hayo ni washiriki wake. Jumuiya ya eneo hutumika na kuyaunganisha makanisa ya eneo pamoja. Jumuiya ya nchi hufanya kazi na kuunganisha makanisa ya nchi nzima pamoja au katika sehemu kubwa fulani nchini. Haya yote yanafanywa na makanisa ya Kibatisti wakifanya kazi pamoja. Kanisa laweza kushiriki katika yote mawili au mojawapo yaani jumuiya ya eneo au ya nchi.

F. Unaweza kuchora namna gani picha ya jumuiya ya eneo?


1) Picha ya makanisa yaliyo huru, yakitegemea na kutegemeana.

Picha hii inaonyesha ya kwamba kila kanisa linajitegemea. Wana uhuru wa kufanya kama mapenzi ya Mungu yalivyo kwa upande wao. Wanategemea wengine kwa vile wanategema makanisa mengine. Jumuiya ni makanisa yanayofanya kazi pamoja yakisai- diana na kuwafikia wapotevu kwa ajili ya Kristo.




2) Picha ya wazo kosefu la jumuiya.

Picha hii huonyesha wazo kosefu ya kwamba jumuiya ya eneo au ya nchi au chama ina mamlaka juu ya makanisa. Hii huonyesha ya kwamba mashauri yote ya makanisa hutengenezwa katika chama na kupelekwa kwa makanisa. Katika utaratibu wa aina hii, makanisa hayana uhuru, hayajitegemei, hayana hiari. Hawawezi kuwa na haki ya kujikatia mashauri. Oni hili linapinga kanuni ya Kibatisti kuhusu utawala wa kanisa kwa njia ya washiriki wenyewe.



G. Jumuiya ya eneo au jumuiya ya nchi hufanya kazi kwa njia gani?

Makanisa wanachama huwatuma wajumbe wao katika mkutano wa mwaka wa jumuiya au chama. Mkutano huwa na wakati wa kuhubiri, kuimba, kutoa ushuhuda, n.k. Nambari au idadi ya wajumbe hutegemea makanisa yale ambayo ni wanachama. Mkutano hufikiri kuhusu kazi inayotakiwa kufanywa na kuweka makisio yake. Wajumbe hupokea taarifa ya kazi. Wajumbe wote hawawezi kukutana nyakati zote kukata mashauri. Kwa hivyo huchagua kamati na viongozi wa chama. Kamati ya utendaji (E.C.) huwakilisha katika mambo yote ya mikutano kabla ya mkutano wa mwaka.

1) Kazi ya viongozi ni nini?

Kwa kawaida viongozi wanaochaguliwa ni mwenye-kiti na mdogo wake, mwandishi na mdogo wake, na mwaka hazina. Hawa wanachaguliwa kulingana na katiba ya chama. Wanapaswa kuwa watu wazima katika imani, waliohakikishwa kuwa viongozi na ambao hali yao ya kiroho haina mashaka au maswali. Wanaofaa. Kazi ya kila kiongozi iwe katika mwongozo wa kazi zinazomhusu kiongozi; anaweza tu kusema kwa niaba ya chama kuhusu mambo yale ambayo yamepitishwa na kukubaliana na chama. Kundi au kamati ya wawakilishi wa chama kuhusu mambo yanayotangulia mkutano wa mwaka wana mamlaka hayo. Kamati ya utendaji inapaswa kuangalia mambo hayo na kusaidia inavyowezekana. Ingawa hivyo, viongozi hao wanapaswa kuangalia mamlaka yao na uwezo wao kwa chama. Kwa mfano kamati hushindwa kufanya kazi zake kwa sababu mbalimbali. Kwa kiongozi kufanya kazi iendelee, anaweza kutoa mapendekezo kwa kamati. Afanyapo hivyo, aweza kushtakiwa eti anatawala kazi.

2) Kazi ya kamati ya utendaji ni nini?

Wajumbe wa makanisa hukutana mara moja tu kila mwaka. Wajumbe hao hukata mashauri kuhusu mapenzi ya Mungu ya kutimi- zwa kwa kusudi lake Bwana. Katika mkutano wa mwaka, kusanyiko huchagua kamati ya utendaji. Wachaguliwao katika kamati hii watoke katika kila sehemu ya kazi nzima. Kamati ya utendaji hukutani kila mara katikati ya mwaka kulingana na mipango ya kazi. Mipango ya mikutano hufuata utaratibu. Wao hupata ripoti au taarifa, hufanya kazi kulingana na mambo yanayotakiwa, halafu hufanya mapendekezo na kuyapatia makanisa.

Kamati haiwezi kuyafanya makanisa yakubali kufuata mashauri ambayo wao wenyewe (makanisa) hawajakata shauri. Kwa kawaida makanisa hukubali mapendekezo yaliyofanywa na kamati ya utendaji. Lakini kanisa pia lina haki ya kukataa.

Idadi ya makanisa itategemewa kwa kujua idadi ya kamati ya utendaji ya jumuiya ya eneo. Wanaochaguliwa katika kamati ya utendaji ya jumuiya ya nchi wanatakiwa kuwa wachache. Kamati hii ya utendaji huchaguliwa kulingana na wajumbe wa makanisa ya jumuiya ya eneo. Na ikumbukwe ya kwamba makanisa ndiyo yaliyo wanachama wa jumuiya, siyo jumuiya ndogo za eneo.

H. Je, jumuiya ya eneo na jumuiya ya nchi ni vyama tofauti vinavyojitegemea?

Ndiyo, kila kundi, makanisa, jumuiya ya eneo, jumuiya ya nchi, chama, ni makundi mbalimbali yanayojiendesha yenyewe. Kanisa ni msingi wa makundi yote ya Kibatisti. Jumuiya zote huwako kwa kusudi la kuyasaidia makanisa. Makanisa huvipa vyama hivi wajibu fulani kutimiza. Vyama hivi hufuata mapenzi ya Mungu kwa kuwaomba wajumbe wa makanisa kupiga kura. Hufanywa hivyo katika mkutano wa mwaka. Jumuiya zote zina sehemu ya maneno haya katika katiba zao: "Huku tukiwa huru na kujitegemea katika eneo letu la kazi, jumuiya yote au chama haitadai na haitajaribu kutawala kundi lingine la Kibatisti." Kundi lililo na maneno hayo katika katiba yake halitadharau uhuru wa kanisa. Kila kundi hufuata mapenzi ya Mungu kama walivyokata shauri kulingana na wingi wa washiriki wake. Wabatisti hawalazimishi kanisa kufanya kitu cho chote kinyume cha mapenzi yake.

2. Je, Wabatisti wafanya kazi na madhehebu mengine?

Kuna madhehebu mengi ya Kikristo. Mengine yana imani na matendo sawa na ya Kibatisti. Yesu aliwakemea wanafunzi wake kwa kukataza mahubiri ya wengine ambao hawakuwa katika kundi lao. Yesu akasema, "...msimkataze, kwa kuwa yeye ambaye si kinyume chenu yu upande wenu" (Luka 9:50). Ingawa wengine hawakubaliani na Wabatisti, wanahitaji kupendwa kwa sababu wanampenda Yesu pia. Wabatisti wasitake kupata washiriki kutoka makanisa mengine. Kukiwako na shida, viongozi wakae pamoja na kusuluhisha shida hiyo katika upendo. Shida hiyo ikiachwa iendelee italeta ushuhuda mbaya katika jamii. Makanisa yatafute washiriki wapotevu sio kutoka makanisa mengine. Hapa kuna mashauri au kanuni zinazohusu kufanya kazi pamoja na madhehebu mengine.

A. Muungano unaolisaidia kanisa kutimiza kusudi lake ni mzuri. Muungano ni kufanya kazi pamoja. Umoja unaolisaidia kanisa

kutimiza shabaha yake ni sawa. Kanisa linahitaji kufikiri na kukata shauri juu ya kila hatua. Hii maana yake ni kusema ya kwamba kanisa linahitaji kupanga shabaha na lengo kwa kufanya kazi zake. Basi hivyo kanisa hujua ikiwa muungano utalisaidia kutimiza shabaha yake na lengo lake au la.

B. Muungano una matokeo ya kusahihishwa.

Katika kufanya kazi pamoja na madhehebu mengine, Wabatisti wanaweza kujifunza ya kwamba pia na wao wanamtafuta Yesu na kumtumikia. Wabatisti wanaweza kujifunza kitu juu ya imani yao. Nao pia waweza kujifunza kitu kuhusu imani ya Wabatisti. Kujifunza kutoka wenzi wao ni kwa kuchunguza imani na matendo yao. Hii huwafanya Wabatisti kusoma sana Biblia. Kama vile mafundisho ya Biblia hufuatwa na kutekelezwa, hii huwafanya Wabatisti kukua zaidi katika nia na mwongozo wa maandiko matakatifu.

C. Muungano unaweza kuwa ushuhuda mwema kwa wasio Wakristo katika jamii.

Wasio Wakristo wwamesumbuka sana na tofauti iliyopo katikati ya madhehebu tofauti. Wanafikiri ya kwamba Wakristo hawawezi kushirikiana pamoja. Ikiwa makanisa katika sehemu yanagombana, basi hapo kuna ushuhuda mbaya. Makanisa yaliyo katika jamii ni yafanye kazi pamoja kwa kuonyesha umoja wao katika Kristo.

3. Kanisa liwe na uhusiano gani na serikali ya taifa?

A. Wazo la kanuni kamili ni:

1) Kanisa huru.

Kanisa huru ni kanisa linaloongozwa na kutawaliwa na washiriki wake. Kweli kuna sheria za nchi ambazo ni lazima kanisa kutii. Sheria hizi ni zile ambazo huwapa wakaazi masharti. Hata hivyo, serikali isiingilie mambo ya kiroho. Kwa mfano, katika historia ni serikali tu huwapa watu wa madhehebu kuabudu katika dhehebu moja. Wabatisti wamepinga sana wazo hilo la kuwa na dhehebu la serikali ya nchi. Wabatisti hutaka uhuru wa watu kuabudu katika njia ambayo inatosheleza haja zao za kiroho.

2) Taifa huru.

Taifa huru ni lile ambalo linaoongozwa na kutawaliwa na wananchi wenyewe. Wabatisti wanaamini ya kwamba wananchi wakiongozwa na Mungu wana uwezo wa kuliongoza taifa lao wenyewe. Katika historia ya Ukristo, kuna mifano mibaya ya kanisa kuingoza serikali. Wabatisti hupinga njia hiyo. Kusudi la Kanis aliko katika mambo ya kiroho na usafi wa tabia ya maisha ndani ya

watu, sio katika uwezo wa kisiasa.

3) Utengano baina ya kanisa na serikali ya taifa.

Kanisa huru katika nchi huru maana yake ni kwamba zote zina uhuru. Kuna utengano katikati yao. Serikali ya nchi haitawali kanisa katika mambo ya kiroho, wala kanisa halitawali serikali katika mambo ya kisiasa. Kanisa ni lazima lifuate mambo ya serikali na hasa sheria zile ambazo wanapewa raia kuzifuata. Kanisa lifuate sheria ya umilikaji wa mashamba na sheria za ujenzi wa nchi. Serikali ya nchi iwe na tabia nzuri na ifuate haki. Inahusika na maisha ya watu. Inaheshimu haki ya walio wengi na wachache pia. Kuwe na utengano baina ya serikali na kanisa.

B. Mambo yanayohusu kanisa na serikali pamoja ni:

1) Utulivu katika nchi.

Kanisa na serikali huhusika na utulivu wa nchi. Katika taifa fulani ambalo halina utulivu wa siasa, watu huteseka. Utulivu ni muhimu katika maendeleo.

2) Mambo yanayohusu hali ya watu.

Serikali zote zinahusika na mambo ya elimu, matibabu na matakwa ya kimaendeleo. Makanisa pia yanahusika na mambo hayo. Makanisa mengi yana shule, kazi ya matibabu, maendeleo na mambo ya mipango ya kuinua hali ya maisha ya watu. Hali ya maisha ya watu ni hitaji la kanisa na la serikali pia.

3) Uaminifu na uadilifu katika wafanya kazi wa serikali.

Maisha ya Yesu ni mfano mwema wa uaminifu na uadilifu. Kanisa liwe mfano wa Kikristo. Kanisa hutafuta wokovu wa wengine kuwa kama Kristo. Serikali yo yote ichukue hatua ya kupinga machafuko. Serikali ya machafuko huendelea kutawala kwa nguvu. Watu wa taifa hupata taabu wakati serikali na kanisa hawafikirii kuhusu maisha ya raia katika uaminifu na uadilifu.

C. Wakristo wana wajibu kwa serikali yao.

Katika Agano Jipya, serikali haikuwa jambo la maana. Warumi waliwatawala watu wengi hata wale wasiokuwa Warumi. Wengi wa watu hawa wakakemewa na kufanywa watumwa wa Warumi. Na ajabu ni kwamba Yesu hutuambia kumpa Kaisari vitu vya Kaisari (Matendo 22:21). Tunaambiwa katika nyaraka kutii, kuheshimu, kulipa kodi, kutenda haki, na tusitumie uhuru wetu vibaya kwa kutenda mabaya katika wajibu wetu kama raia (Warumi 13:1-7; Tito 3:1-3; I Petro 2:13-17). Ni rahisi kufanya vitu hivi katika taifa huru. Katika taifa lo lote, liwe si huru, Mkristo anapaswa kuishi kulingana na mafundisho ya Biblia.

4. Tumejifunza nini kuhusu uhusiano wa kanisa?

1. Hakuna kielelezo cha Biblia tulichopewa kufuata katika muungano wetu na madhehebu. Kwa hivyo, kanisa na mpango wa kimadhehebu wafuate Biblia.

2. Makanisa yanayojitegemea. Huyategemea makanisa mengine, hufanya kazi pamoja kwa uhuru, huviheshimu vipawa vya kila mmoja, hutumia kanuni za Biblia.

3. Jumuiya ya eneo na jumuiya ya nchi au chama huwako kwa kusudi la kuyasaidia makanisa kufikia lengo lake. Makundi hayo yote ni huru yakijiongoza yenyewe. Hawawezi kuyalazimisha makanisa kufuata mapenzi yao.

4. Muungano wa kimadhehebu wapaswa kuwa mfano wa udugu wa Kikristo.

5. Kanisa huru katika nchi huru ni jambo la maana na la kibiblia.

## MUHTASARI
## SOMO LA KUMI

1. Kanisa liwe na mapatano ya Namna gani?
   A. Agano la Kanisa.
   B. Fungu la Imani.
   C. Katiba ya Kanisa.

2. Kanisa Liweke Taarifa Gani?
   A. Kitabu cha taarifa ya kanisa.
   B. Taarifa ya hazina ya kanisa.

3. Je, kanisa laweza kuwa na vikundi maalum vidogo vidogo ndani yake?
   A. Kundi la kujifunza Biblia (madarasa ya shule ya Jumapili).
   B. Kwaya au Uimbaji.
   C. Makundi ya vijana.
   D. Makundi ya wanawake na wanaume.

4. Tumejifunza nini kuhusu mapatano ya kanisa, taarifa au matengenezo au mipango yake?

## SURA YA KUMI
## MAPATANO YA KANISA
## TAARIFA NA TARATIBU ZA MIPANGO

Je, washiriki wa kanisa wawe na mpango fulani wa mapatano? Ni mapatano ya aina gani ambayo wanaweza kuwa nayo? Je, kanisa laweza kuweka utaratibu wa taarifa ya mpango? Taarifa gani ambazo zinaweza kuwekwa? Na ni zipi? Je, Kanisa liwe na mgawanyiko wa vikundi mbalimbali katika ushirika? Vikundi gani ambavyo vinapaswa kuwamo kanisani, na kwa nini? Katika sura hii tutakuwa tukiangalia juu ya mapatano, mipango na vikundi katika kanisa. Kila kanisa na litumie mipango hii.

1. Kanisa liwe na mapatano ya Namna gani?

Kanisa na lifanye mapatano yake mara tu linapoundwa. Agano la kanisa, fungu la maneno ya imani na katiba ya kanisa ni mambo muhimu. Hayo hufanywa ili kuwahusisha washiriki katika kuhusiana wao kwa wao. Mapatano hayo huweka kwa utaratibu wajibu au madaraka ya kila mshiriki na wajibu kwa kanisa pia. Husaidia katika kuzuia shida, kusuluhisha matatizo na kutumika kama mwongozo.

A. Agano la Kanisa.

1) Kusudi la Agano la Kanisa.

Agano la Kanisa ni mapatano ya washiriki yanayowahusu wao kwa wao. Ikiwa washiriki wa kanisa hawana mapatano ya msingi, basi watajuaje madaraka yao, wao kwa wao? Agano hasa ni neno la kibiblia. Mungu alianzisha maagano na watu wake. Kama kanisa, tunapaswa kuonyesha agano. Kila kanisa liandike agano lake. Hapa kuna mfano wa agano la kanisa.

2) Mfano wa agano la Kanisa.

Agano la Kanisa letu

Tunaamini ya kwamba tumeongozwa na Mungu kumpokea Yesu Kristo kama Bwana wetu. Na baada ya kukiri kwa imani, tumebatizwa katika jina la Baba na la Mwana na la Roho mtakatifu. Sasa mbele ya Mungu tunawekewa agano hili kama mwili mmoja ndani ya Kristo.

Kwa maendeleo ya Kanisa hili

Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, tutatembea pamoja katika upendo wa Kikristo. Tutafanya kazi pamoja katika upendo wa Kikristo. Tutafanya kazi pamoja kwa maendeleo ya kanisa hili, katika elimu, utakatifu, na nguvu. Tutalitegemeza kimaendeleo na

kiroho. Tutatunza ibada zake, maagizo yake, tabia na imani.

Uwakili wa Mkristo

Tutatoa pesa zetu kwa mpango na upendo kumsaidia mchungaji. Tutalipa gharama za kanisa. Tutawasaidia maskini. Tutasaidia umisheni ili tueneze injili katika nchi au mataifa yote.

Pekee Nyumbani

Tutatumia wakati wa kutosha katika kujifunza Biblia na kuomba. Tutawafundisha watoto wetu njia za Mungu. Tutatafuta njia za kuwaongoza watu wa jamaa zetu na rafiki zetu kumpokea Yesu kama Bwana.

Mbele ya Ulimwengu

Tutatembea kwa uangalifu mbele ya watu wengine. Tutakuwa watu wa haki katika mambo yetu, na wakamilifu katika ahadi zetu, tutakuwa mfano wa matendo yetu. Tutazuia kueneza fitina na maneno mabaya juu ya watu wengine na tutajizuia kuwa na hasira. Kwa furaha yetu, tutamtegemea Bwana Yesu, siyo katika unywaji wa pombe, dawa za kulevya au katika vitu vya ulimwengu. Tutafanya kazi kwa bidii tuwezavyo ili ufalme wa Mungu uweze kukua.

Sisi kwa sisi

Tutasaidiana katika upendo wa kidugu. Tutakumbukana katika maombi. Tutasaidiana katika ugonjwa na shida au taabu. Tutaonyeshana upendo wetu katika maneno na vitendo. Tutajitahidi kutoumizwa kwa haraka na wengine na kuwa tayari siku zote kutengeneza mambo yaliyoharibika tukifuata mfano wa mafundisho ya Bwana wetu.

Tunapohama

Tukihama, tutajiunga na kanisa lingine ambapo tutaongozwa na Neno la Mungu. Tutaendelea kuishi katika agano la Mungu na watu wake katika sehemu hiyo tuliyohamia.

B. Fungu la Imani.

1) Kusudi la fungu la imani.

Fungu la imani au maandishi fulani ya imani lazima yatengenezwe. Kusudi la sehemu hii ni kufanya ufupisho wa yale yanayoaminiwa na kanisa. Watu wengi wamekuwa Wabatisti nao wametoka katika madhehebu tofauti. Wakati mwingine watu hao huleta katika Kanisa la Kibatisti mafundisho ya madhehebu waliyotoka. Kanisa liwe na kauli iliyo wazi kuhusu imani yao. Ni jambo la muhimu kuwa na kauli hiyo katika maandishi wakati

kanisa linapoanzishwa. Mtu anapokuwa mshiriki, ajue kanuni za imani ya kanisa. Kauli hiyo inaweza kuwa fupi au ndefu kulingana na hitaji la kanisa. Mfano wa kauli ndefu ni kama hivi: Imani ya Wabatisti na Ujumbe. Hapa pana mfano wa kauli fupi ya imani. Lazima kanisa liandike kauli yake lenyewe. Linaweza kutumia mambo hayo kama mfano wa kufuata.

2) Mfano wa kauli fupi ya imani.

Imani Fulani Tuipendayo.

1. Tunaamini Biblia ni neno la Mungu kwa watu. Ni amri ya pekee kutegemewa kwa imani ya kila Mkristo na matendo yake.

2. Tunaamini ya kwamba washiriki wa kanisa lazima wawe watu waliozaliwa mara ya pili. Wokovu uwe wa kwanza kabla ya kuwa washiriki wa kanisa.

3. Tunaamini ya kwamba Agano Jipya hufundisha tu ubatizo wa waamini kwa njia ya kuchovya. Ubatizo unaonyesha mfano wa ujumbe wa injili - kwamba ni kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

4. Tunaamini ya kwamba waamini wa Agano Jipya walibatizwa kwanza kabla ya kuweza kushiriki katika meza ya Bwana.

5. Tunaamini katika haki ya kila mshiriki wa kanisa kushiriki katika utawala wa kanisa, mipango na tabia. Utawala wa kanisa la Kibatisti ni wa washiriki wenyewe bila kulazimishwa au kutawaliwa na watu walio nje ya kanisa.

6. Tunaamini ya kwamba mtu ana uhuru wa kukata shauri lake mwenyewe kuhusu dini bila kulazimishwa na watu wengine.

7. Tunaamini ya kwamba kanisa litaweza kujitawala lenyewe na kufanya kazi pamoja na makanisa mengine kulingana na vile wanavyooona na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

8. Tunaamini katika uhuru kamili baina ya serikali na kanisa kwa kuiongoza.

C. Katiba ya Kanisa.

1) Kusudi la katiba ya kanisa.

Agano la Kanisa huongoza mambo ya uhusiano wa kiroho wa kanisa. Shabaha ya katiba ya kanisa ni kuongoza shughuli za kanisa. Kanisa kama kundi la watu, linapaswa kutoa mawazo kuhusu jinsi litakavyofanya shughuli zake. Katiba yake iwemo na maelezo ya kauli ilioandikwa hapo mbele.

2) Mfano wa katiba ya Kanisa.

i. Kauli ya kwanza au sehemu ya kwanza. JINA

ii. Kauli ya pili. IMANI.

(Makanisa fulani hupenda kuweka katika kauli hii ufupisho wa imani. Wengine hutaka kauli au sehemu kamili).

iii. Kauli ya tatu. AGANO LA KANISA.

iv. Kauli ya nne. TABIA AU MATENDO.

Sehemu ya kwanza - mwongozo (mfano wa uongozi wa kanisa).

Sehemu ya pili - Imani au kanuni.

MASHARTI (BY-LAWS)

Kauli ya kwanza (1) - UANACHAMA

| | |
|---|---|
| Sehemu ya kwanza | 1. Tabia au uwezo. |
| Sehemu ya pili | 2. Wajibu. |
| Sehemu ya tatu | 3. Haki. |
| Sehemu ya nne | 4. Walio wengi (hesabu ya walio wengi). |
| Sehemu ya tano | 5. Kikomo au mwisho wake. |
| Sehemu ya sita | 6. Matengenezo (kurudi kutengeneza tena). |

Kauli ya pili (2) - VIONGOZI WA KANISA

| | |
|---|---|
| Sehemu ya kwanza | 1. Mchungaji (hii itahusika jinsi ya kumwita, kumsimamisha kazi, na kazi zake). |
| Sehemu ya pili | 2. Mashemasi (hii ihusike na nambari ya mashemasi, uchaguzi, muda na kazi zao). |
| Sehemu ya tatu | 3. Mwenyekiti (hii inatwambia mtu mwenyewe, wajibu wake wa kuchunga, mchungaji, mashemasi au wengine, na wajibu wake). |
| Sehemu ya nne | 4. Mwandishi (hii inahusu tabia ya uchaguzi, kazi na muda wa kufanya kazi hiyo ya |

uandishi).

Sehemu ya tano — 5. Mweka hazina (hii inahusu tabia ya uchaguzi, kazi yake na anayehusika ni nani. Au taarifa yake ya pesa inamhusu nani).

Nafasi nyingine ambazo kanisa linazo kulingana na mahitaji ziandikwe katika sehemu hiyo.

Kauli ya tatu (3) - KAMATI ZA KANISA

Kamati za kawaida za kila mara ziandikwe. Hii itaonyesha jinsi wanavyoweza kuchaguliwa, watu wangapi, kazi zao, na mambo mengine yanayotakiwa.

Kauli ya nne (4) - HAZINA YA KANISA

Kanisa liweze kueleza waziwazi mambo yanayohusu hali ya pesa zake. Mambo ya matumizi ya pesa, mapato, hesabu, taarifa pamoja na yote mengine yanayohusu pesa za kanisa yawe wazi kwa kila mshiriki.

Kauli ya tano (5) - MIKUTANO

Sehemu ya kwanza 1. Ibada
Sehemu ya pili 2. Shughuli

Kauli ya sita (6) - TABIA

Kauli ya saba (7) - KAMATI YA UTENDAJI YA KANISA

Kanisa linaweza kuchagua kamati ya utendaji ya watu waliochaguliwa kutoka vikundi mbalimbali vya kanisa. Wana madaraka ya kupanga, kushirikisha na kuongoza mpango wa kanisa.

Kauli ya nane (8) - MAREKEBISHO

Hii hueleza jinsi katiba na masharti yatakayoweza kufanyiwa marekebisho. Kuna mifano mingine ya katiba za kanisa. Lingekuwa jambo la busara kwa kanisa kupata nakala mbalimbali ili waone mifano ya kuwafaa wakitengeneza katiba yao.

3) Kanuni zinazohusu katiba ya kanisa.

a. Usawa wa washiriki ulindwe sawasawa.
b. Haki ya washiriki ihakikishwe.
c. Utengenezaji tena wa hali ya juu ya ushirika wa kanisa utunzwe.
d. Jinsi Kanisa litakavyofanya kazi zake lazima kuandikwa waziwazi.

2. Kanisa Liweke Taarifa Gani?

A. Kitabu cha taarifa ya kanisa.

1) Kusudi la kitabu cha taarifa ya kanisa.

Kila kanisa lazima liweke vizuri taarifa zote za mashauri yaliyokatwa na taarifa ya washiriki. Katika kitabu hicho kuwemo na taarifa ya washiriki iliyokatwa na Kanisa. Kuwemo pia na idadi ya washiriki wa kanisa. Kionyeshe jinsi kila mtu alivyopata kuwa mshiriki na jinsi anavyotoka katika ushirika wa kanisa. Kitabu hiki ni cha manufaa sana. Washiriki wa kanisa ni wale tu ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha kanisa. Ni hao tu wanaokubaliwa kushiriki katika mashauri ya kanisa. Mara nyingi sisi husahau mashauri yaliyokatwa katika mikuano. Kanisa likiwa na taarifa nzuri, litakumbuka mashauri yote yaliyopitishwa.

2) Kanuni zinazohusu kitabu cha taarifa ya kanisa.

a. Kanisa liweke taarifa tangu mwanzo wake.

Ni jambo la manufaa kwamba kanisa liweke taarifa yake tangu mwanzo. Taarifa hii husaidia kanisa. Baadaye watajua ni nani aliyeanzisha kanisa na jinsi gani alivyoanzisha pamoja na mashauri

b. Kanisa lichague karani kutunza taarifa.

Karani wa kanisa hutunza taarifa zote za mikutano na shughuli za kanisa. Ana wajibu wa kuwaandikisha washiriki. Huandika majina, tarehe na njia ambayo mtu alipata kuwa mshiriki wa kanisa. Anapaswa pia kuandika jinsi mtu anavyohama kutoka kwa kanisa. Mwandishi au karani aweze kuandika barua ya uhamisho au mapendekezo kuhusu mshiriki aliyejiunga na kanisa lingine ikiwa kanisa linatafuta kujua habari zake. Habari hii ifanywe katika mkutano wa shughuli za kanisa. Kwa hivyo, karani awe mwaminifu katika kuhudhuria mikutano ya kanisa.

c. Taarifa iwekwe mahali pa usalama.

Ikiwa hakuna mahali pa usalama, basi taarifa inakiliwe katika karatasi nyingine. Kanisa lihakikishe ya kwamba karani anapewa kitabu cha taarifa.

d. Karani ajifunze jinsi ya kuweka taarifa za kanisa.

Karani huyo mpya afundishwe sawasawa jinsi ya kuweka taarifa hiyo ya kanisa. Mchungaji akague kuona ikiwa washirikil wapya wameandikishwa vyema.

B. Taarifa ya hazina ya kanisa.

1) Kusudi la taarifa ya hazina ya kanisa.

Taarifa ya hazina ya kanisa ni muhimu sana. Washiriki

hutoa fungu la kumi na matoleo. Wamefanyia kazi pesa hizo wanazotoa kanisani. Kanisa basi liweke taarifa nzuri ya vipawa hivyo. Kanisa ambalo haliweki taarifa nzuri ya matoleo yao, litaingia katika matatizo mara moja. Washiriki hukataa kutoa ikiwa hawajui pesa zao zinafanya nini.

2) Kanuni zinazohusu taarifa ya hazina ya kanisa.

(a) Jumla ya pesa zilizopatikana lazima iandikwe.

Kanisa hupata pesa kwa njia nyingi. Kwa hivyo taarifa ziwekwe sawasawa jinsi pesa zilivyoingia na kwa makusudi gani. Hii huipa kanisa nafasi ya kutumia pesa zake kulingana na makusudi ya pesa hizo.

(b) Stakabadhi zihifadhiwe.

Kwa kusudi la kumlinda mweka hazina, lazima stakabadhi iandikwe kila wakati anapolipa pesa kununua kitu cho chote. Stakabadhi ni muhimu kueleza jinsi pesa zilivyotumiwa.

(c) Taarifa ya kila mwezi itolewe mbele ya kanisa.

Kwa njia hii washiriki watajua jinsi taarifa ya hazina ya kanisa ilivyo wazi kwa maswali ya uaminifu. Mweka hazina atoe ripoti yake kwa kanisa kila mwezi. Kukiwako na maswali yasiyojibika, basi mara tu mashaka huanza, kutoaminiana na uvumi wa kutokuwa na ukweli.

(d) Pesa zitumiwe tu kulingana na makisio ya kanisa.

Pesa ni za kanisa. Kwa kufanya makisio, kanisa hutayarisha mpango wa matumizi ya pesa hizo. Mweka hazina asiulizwe kutoa pesa kwa kitu ambacho hakiko katika mpango wa makisio. Kuna haja au mahitaji ambayo hayamo katika makisio. Kamati ya kanisa na ifanye mapendekezo kuhusu mahitaji hayo.

(e) Pesa ziwekwe kando kwa umisheni kwanza.

Wakristo wanapaswa kutoa kwa Mungu vilivyo vya Mungu kwanza. Kanisa litoe kwa kazi ya umisheni kwanza. Kanisa lisilofanya hivi ni sawa na mshiriki ambaye hatoi kwa Mungu kwanza. Mtu kama huyo je, atatazamia kubarikiwa na Mungu? Je, kanisa kama hilo laweza kutazamia baraka kutoka kwa Mungu?

(f) Mchungaji asiwe mweka hazina.

Makanisa mengine yana shida kuhusu pesa. Kwa hivyo ni bora mchungaji asishughulike na pesa. Pesa zitunzwe na kushughulikiwa sawasawa na kanisa. Ikiwa kanisa litafanya hivyo, basi mchungaji atakuwa mbali na mashtaka ya kutotunza pesa za kanisa vizuri.

(g) Kamati ihesabu pesa na kiasi kilichopokelewa na mweka hazina, na kiandikwe katika mapokeo.

Ikiwa mweka hazina ndiye atakayehesabu pesa, shida zinaweza kutokea. Ni bora kwa kundi kupokea na kuhesabu pesa. Mweka hazina awape risiti au stakabadhi.

3. Je, kanisa laweza kuwa na vikundi maalum vidogo vidogo ndani yake?

Kanisa ambalo limekuwa linaweza kuwa na vikundi maalum vikutane kwa mahitaji maalum. Vikundi hivi sio tofauti na kanisa. Havifanyi mambo yao wenyewe tofauti na kanisa. Kwa vile wamo kanisani, basi wako chini ya uongozi wa kanisa. Kila kundi katika kanisa lina uhuru wa kufanya mambo mengi. Ingawa hivyo, kwa vile wanawakilisha kanisa, basi lazima wawe chini ya mashauri na uongozi wa kanisa. Kanisa liwe na vikundi hivi vyote au baadhi yake.

A. Kundi la kujifunza Biblia (madarasa ya shule ya Jumapili).

1) Vikundi vya kujifunza Biblia vina makusudi mawili. Kusudi lao la kwanza ni kuwafundisha watu Biblia. Kusudi la pili ni kuwafundisha washiriki jinsi ya kuwaambia wengine habari za Yesu. Washiriki wanaojifunza Biblia na kuwaambia watu habari za Yesu hukua katika imani.

2) Maandiko yanafunzwa kwa sababu Biblia ndicho kitabu cha amri ya mwisho kwetu.

3) Kanisa liwafundishe waalimu wa kufundisha vikundi hivyo vya kusoma Biblia. Wafundishwe jinsi ya kuliongoza darasa kuwashuhudia watu wengine habari za Yesu. Kuweko na madarasa ya Biblia kwa makundi yote ya kila umri kanisani.

4) Kila kundi la kujifunza Biblia liweke taarifa yake vizuri. Taarifa nzuri husaidia kundi kuwatembelea wengine.

B. Kwaya au Uimbaji.

1) Kusudi la kwaya ni kusaidia kanisa katika uimbaji wake (muziki).

2) Kwaya inaweza kusaidia kanisa katika elimu ya kibiblia, kwa hivyo ni vizuri kutumia nyimbo ambazo zinafundisha ukweli wa Biblia.

3) Kwaya ni njia bora ya kuwaleta watu kwa Yesu Kristo.

4) Kiongozi wa kwaya awe mtu anayejua imani yake na tena awe mtu anayefahamu muziki. Anahitaji kuwa munyenyekevu na wa kutegemewa.

C. Makundi ya vijana.
1) Huwapa vijana nafasi za kukua kiroho.
2) Huwapa vijana nafasi ya ushirika wa kikristo.
3) Huweza kukuza vijana katika Ukristo. Hii ni muhimu kwa kanisa la siku zijazo.

D. Makundi ya wanawake na wanaume.
1) Huweza kuliwezesha kanisa kukua katika ufahamu wa Biblia.
2) Huweza kusaidia katika umisheni wa uinjilisti.
3) Huwapa nafasi ya masomo maalum ya kusaidia mahitaji yao.
4) Wachunge na kulinda kwamba kundi hilo lisiwe la watu fulani tu. Wanapaswa kuwakaribisha washiriki wapya na kuwafanya wajisikie kwamba wao nao ni sehemu ya kundi.

4. Tumejifunza nini kuhusu mapatano ya kanisa, taarifa au matengenezo au mipango yake?
1. Kila kanisa liandike maagano yake na kanuni ya imani. Katiba ya kanisa ni jambo muhimu sana.

2. Taarifa njema, kama vile kitabu cha taarifa ya kanisa, kitabu cha taarifa ya hazina, vyaweza kuzuia shida nyingi.

3.- Vikundi au makundi maalum katika kanisa, kama vile kwaya, vijana, wanawake na wanaume, vinaweza kulifanya kanisa kukua katika kumjua Mungu na Neno lake na kuwavuta wengine kwa Kristo.

4. Viongozi wote, maafisa na makundi yote ya kanisa yawe chini ya mamlaka ya kanisa.

## MASWALI NA MAJIBU
## SURA YA KWANZA

Unaweza kusoma katika sura ya kwanza kuhusu Wabatisti katika historia ya Ukristo.

1. Kwa nini Wabatisti huamini kwamba wao ni washiriki wa Kanisa la Agano Jipya?
   Kanisa la Agano Jipya hufuata mafundisho ya Agano Jipya. Wabatisti na makanisa yao hufanya hivyo.

2. Kwa nini Wabatisti huamini kwamba ubwana wa Yesu ni jambo muhimu zaidi hata kuliko ubatizo?
   Fundisho hili Yesu yu Bwana ni fundisho muhimu katika Biblia. Hakuna faida ya kumbatiza mtu ambaye hajamkubali Yesu kuwa Bwana.

3. Kulikuwako na mafundisho gani na desturi zipi muhimu za makanisa ya Agano Jipya?
   Haya ni: Yesu ni Bwana, wokovu hupatikana kwa kuamini tu, ubatizo ni kwa walioamini kwa njia ya kuchovya ndani ya maji. Washiriki wa kanisa wawe watu wazima.

4. Mafundisho gani makosefu yaliyotokea na yakaacha mafundisho ya Agano Jipya?
   Mengine yalikuwa: Kuwa mshiriki wa kanisa ilikuwa sawa na kuwa katika ufalme wa Mungu. Kubatizwa kulikuwa sawa na kuwa Mkristo, kuwa mchungaji au kuhani kulikuwa sawa na kuwa juu ya washiriki, kufuata mashauri ya kamati kuu ya kanisa kulikuwa sawa na kuyafuata mafundisho ya Agano Jipya.

5. Ni lini neno Batisti lilitumiwa kuonyesha maana ya kanisa?
   Matumizi ya kwanza ya neno Batisti likiwa na maana ya kanisa ilikuwa katika mwaka wa 1609. Misingi ya imani 30 inapatikana katika Agano Jipya.

6. Kuna Wabatisti wangapi katika ulimwengu?
   Kulingana na jumla iliyopeanwa na Wabatisti wa ulimwengu wote (B.W.A) katika mwaka wa 1980, kuna Wabatisti zaidi ya milioni 30.

## SURA YA PILI

Unaweza kusoma zaidi kuhusu kanisa la Agano Jipya katika sura ya pili.

7. Kanisa ni nini?
Kanisa ni kundi la watu wa mahali fulani, waliomwamini Yesu na kubatizwa, waliokusanyika pamoja kwa maagano ya imani, na kwa ushirika wa injili.

8. Nani ambaye ni msingi wa kanisa?
Yesu pekee ndiye msingi wa kanisa (I Wakorintho 3:11).

9. Misemo gani ionyeshayo utatu wa Mungu katika kanisa?
Mitatu kati ya misemo hiyo ni: watu wa Mungu, mwili wa Kristo, na ushirika wa Roho Mtakatifu.

10. Je, kwani ni lazima kuweko na kanisa moja tu la mahali kwa makusanyiko yote?
La, maandiko hayataliunga mkono fundisho hili. Zaidi ya mara tisini kwa mia (90%) neno Kanisa limetumiwa katika Agano Jipya, maana yake ni kanisa la mahali. Makanisa hayo kwa kawaida yakutana katika nyumba za watu.

## SURA YA TATU

Unaweza kusoma zaidi kuhusu kusudi la kanisa katika sura ya tatu.

11. Kusudi la kanisa ni nini?
Kanisa ni ushirika wa waamini waliobatizwa na walioamriwa kuwafanya watu kuwa wanafunzi.

12. Ni mambo gani ambayo yamo katika kuwafanya watu kuwa wanafunzi?
Uinjilisti na kufundisha. Uinjilisti ni kuwaambia wengine habari za Kristo. Kuelimisha ni kuwafundisha waamini wapya njia ya Mungu.

13. Jamii inahitaji kanisa la aina gani?
Kila jamii inahitaji kanisa ambalo lina washiriki waliozaliwa mara ya pili. Inahitaji kanisa ambalo lina utumishi ulio sawa na ule wa Yesu na lililo na nguvu za kiroho.

14. Je, kanisa laweza kujihoji (kujichunguza lenyewe)?
Ndiyo, kanisa lijiulize lenyewe maswali kama haya: Je,

tunawavuta watu kwa Yesu? Na tunawasaidia kukua katika imani yao?

## SURA YA NNE

Unaweza kusoma zaidi kuhusu imani ya Wabatisti katika sura ya nne.

15. Ni imani gani zinazowafanya Wakristo kuwa tofauti na watu wasio Wakristo?
Wakristo wanaamini katika utu wa Yesu, yaani, alikuwa Mungu katika mwili, na katika toleo lake kuwa dhabihu ambayo ni nguvu ya Yesu inayookoa. Mambo haya mawili makuu humpa mtu kuokolewa kwa imani akimpokea Yesu Kristo.

16. Ni imani gani zinazowafanya Wabatisti na wengine kuwa tofauti na kanisa la Kikatoliki la Kirumi?
Tofauti hizi ni: Maandiko tu yanayotegemewa kwa imani na desturi, wokovu ni kwa imani pekee, kila mwamini ni kuhani.

17. Je, imani na desturi fulani za umuhimu kwa Wabatisti ni zipi?
Hizi ni pamoja na: Yesu ni Bwana, maandiko ni amri ya mwisho ya waamini, wokovu ni kwa mtu binafsi. Kwa njia ya imani ndani ya Yesu, ushirika wa Kanisa uwe tu kwa wale waliokwishazaliwa mara ya pili, Wakristo wana uhuru wa madaraka kufanya mapenzi ya Bwana, kila mshiriki ni mwinjilisti.

## SURA YA TANO

Unaweza kusoma zaidi kuhusu maagizo ya kanisa katika sura ya tano.

18. Maagizo ya Yesu kwa kanisa ni nini?
Ni ubatizo na meza ya Bwana.

19. Je, ubatizo unaweza kumwokoa mtu?
Hapana, ubatizo ni kwa waamini pekee. Ni thibitisho la baraka za Mungu ambazo zimekwisha pokelewa tayari.

20. Je, wale wapokeao meza ya Bwana hupata neema maalum?
Hapana, meza ya Bwana ni mfano wa chakula kwa wale ambao tayari wamepokea neema ya Bwana.

21. Je, kuwekwa wakfu ni kuwa na uwezo zaidi juu ya maagizo ya kanisa?

Hapana, maagizo ni lazima yawe chini ya mamlaka ya kanisa.

22. Je, mtu ye yote anaweza kushiriki katika maagizo hayo?
Hapana, maagizo ni kwa Wakristo tu.

## SURA YA SITA

Unaweza kusoma zaidi kuhusu ushirika wa kanisa katika sura ya sita.

23. Ni nani anayeweza kuwa mshiriki wa kanisa la Kibatisti?
Ushirika ni kwa watu waliozaliwa mara ya pili na kubatizwa kwa uzamisho.

24. Ni kanuni gani za Biblia zinazoweza kuongoza uhusiano wa washiriki wa kanisa?
Usawa (Wagalatia 3:28) na udugu (Marko 3:35).

25. Una madaraka yo yote kama mshiriki wa kanisa?
Ndiyo, una wajibu wa kutumia vipawa vyako vya kiroho kwa manufaa ya kanisa. Unapaswa kulisaidia kanisa lako. Una madaraka ya kuwashuhudia wengine na kuwafundisha habari za Yesu.

26. Unaweza kulisaidia kanisa lako?
Unaweza kulisaidia kanisa lako katika maombi, katika fungu lako la kumi, katika sadaka na matoleo, katika uaminifu wa kuhudhuria, katika kuwahimiza wengine, na katika wajibu wa mashauri yako.

27. Kuna matokeo gani ya kanisa lililokua kiushirika?
Hayo ni ushirika mwema, kukua kwa kiroho na nguvu.

## SURA YA SABA

Unaweza kusoma zaidi kuhusu uongozi wa kanisa katika sura ya saba.

28. Kwa nini Wabatisti hutumia neno "mchungaji" badala ya "Askofu" au "mzee" au "kasisi?"
Wabatisti hutumia jina "mchungaji" kwa sababu hueleza vizuri zaidi kuhusu kazi yake. Anaweza kuwa "mzee" ambaye ni mwenye kuheshimiwa. Ni "kasisi" kwa sababu anatazama na kutunza kukua kiroho kwa washiriki.

29. Kiongozi wa kanisa awe mtu wa aina gani?

Awe mtu wa kiroho, mwenye hekima na wa kuheshimiwa (Matendo 6:3).

30. Agano Jipya hufundisha nini kuhusu tabia ya kiongozi wa kanisa?
Ni mtumishi, kasisi ndani ya kundi la makasisi, na amejitolea kwa Kristo.

31. Je, kiongozi achaguliewe na mtu mwingine tu badala ya washiriki wenyewe?
Hapana, kiongozi wa kanisa achaguliwe tu na washiriki wenyewe. Hufanywa hivyo tu katika uongozi wa kanisa, kulingana na mahitaji ya kanisa kwa kufuatia uwezo wa kiongozi.

32. Uwakfu ni nini?
Uwakfu ni utambuzi wa mwito wa mtu kwa Mungu, vipawa vyake vya kiroho, na kuelewa kwake katika mambo ya kiroho na ya Kibiblia.

33. Je, uwakfu humpa mchungaji uwezo fulani maalum, madaraka au nafasi ya uwezo?
Hapana, Wabatisti huamini kwamba ni Mungu tu anayemwita mtu na kumpa vipawa vinavyotakiwa kutimiza huo mwito. Uwakfu ni mfano wa kitendo, haupitishi nguvu maalum, nafasi au uwezo au mamlaka.

34. Kwa nini wahubiri wa Kibatisti hawavai kola au kanzu?
Mavazi ya aina hii hutumiwa kuonyesha tofauti iliyoko kati ya washiriki na mchungaji. Wabatisti huamini kwa dhati kwamba kusiweko tofauti kati ya washiriki na mchungaji.

35. Wachungaji ni watu wa kiroho zaidi kuliko washiriki?
Mchungaji awe mfano wa mwamini. Ingawa hivyo, Wakristo wote ni makuhani kwa hivyo wanapaswa kuwa mfano vile vile.

36. Wachungaji walipwe mishahara?
Ndiyo, Biblia hufundisha ya kwamba Kanisa limsaidie mchungaji wake.

37. Nani amlipe mchungaji?
Kanisa lina wajibu wa kumlipa mchungaji.

38. Alipwe kiasi gani?
Apate karibu sawa na mapato ya kawaida ya washiriki wanavyopata.

39. Alipwe mara ngapi?
Wengine hulipwa kila juma na wengine kila mwezi.

40. Je, jumuiya ya eneo au ya nchi au chama kimlipe mchungaji?
Hapana, mchungaji wa kanisa la mahali alipwe na kanisa hilo lake.

## SURA YA NANE

Unaweza kusoma zaidi kuhusu utawala au uongozi wa kanisa katika sura ya nane.

41. Mpango gani wa utawala wa kanisa ambao unafuatwa na kanisa la Kibatisti?
Wabatisti huamini katika utawala na kanisa la mahali kwa njia ya washiriki wenyewe. Uongozi wao unategemea usawa wao, uhuru wa, na udugu.

42. Je, Agano Jipya hufundisha mfano kamili wa aina ya utawala wa kanisa?
Hapana. Katika Agano Jipya uchaguzi wa viongozi waliofaa ulipendelewa zaidi kuliko aina fulani ya utawala wa kanisa.

43. Tunajuaje aina fulani ya utawala wa kanisa ambayo tunaweza kutumia?
Agano Jipya haitupi mfano kamili wa kufuata. Kwa hivyo, tunapaswa kuwa na utawala wa Kanisa ambao unafuatana na mafundisho ya Agano Jipya. Utawala wa Kanisa usiweze kuaibisha roho wa undugu baina ya waamini wala uhuru wao wa kiroho.

44. Je, kunayo mifano ya Kibiblia kuhusu washiriki wakijitengenezea mashauri?
Ndiyo, tazama Matendo 6, 13 na 15.

45. Je, kuna kanuni gani za maana za utawala wa Kanisa la Kibatisti?
Tatu kati ya hizo ni: Ushirika ni kwa uchaguzi wa hiari, washiriki wote ni sawa mbele za Mungu, makanisa yana uhuru wa kujikatia mashauri yao wenyewe.

46. Kuna matatizo gani ambayo yanatokea katika utawala wa Kanisa la Kibatisti?
Ni haya: Mshiriki akitaka kutawala kanisa, washiriki wakitaka kufanya kama wanavyokata, wakitaka watu wengine kuwaongozea

kanisa lao.

47. Je, uhuru ni nafasi ya kujifanyia cho chote kama tutakavyo?
Hapana, huo si uhuru. Ikiwa kila mtu angefanya anavyochagua kufanya, kungeleta michafuko.

48. Je, kuna mambo gani mazuri ya maana kuhusu utawala wa kanisa yaliyomo ndani ya Kanisa la Kibatisti?
Kanisa litumie kamati kadiri wanavyotaka. Kila mshiriki aweze kushiriki katika kutoa maoni yake kabla ya shauri kukatwa. Kila mshiriki afanye kazi kwa manufaa ya kanisa.

## SURA YA TISA

Unaweza kusoma zaidi kuhusu uhusiano wa kanisa katika sura ya tisa.

49. Kanisa la Kibatisti hufanyaje kazi pamoja na makanisa mengine ya Kibatisti?
Kanisa la Kibatisti hufanya kazi pamoja na makanisa mengine ya Kibatisti kwa njia ya jumuiya mbalimbali na vyama.

50. Jumuiya ya eneo, jumuiya ya nchi na chama ni nini?
Jumuiya ya eneo au jumuiya ya nchi au chama ni kundi la makanisa yaliyo na usawa katika mambo ya imani na desturi ambayo yameungana pamoja katika ushirika na utumishi kwa utukufu wa Mungu.

51. Uanachama katika jumuiya au chama, je, ni kwa uchaguzi wa hiari?
Ndiyo, huo ndio msingi wa imani ya Kibatisti.

52. Kuna kanuni gani za nguvu zinazotakiwa ili kujenga jumuiya yenye nguvu?
Kutegemea bila kudharau uhuru wa kila kundi ni muhimu sana. Madhehebu hupata uhai kwa kufanya kazi pamoja. Uanachama na ushirika ni jambo la hiari. Haki ya kila mmoja lazima kutunzwa na kuheshimiwa.

53. Mahitaji gani waliyo nayo makanisa ambayo yanahitaji kufanya kazi pamoja?
Makanisa yanahitaji ushirika, usawa wa kanuni za imani, nguvu katika kazi, elimu na maendeleo. Kufanya pamoja katika jumuiya na vijana husaidia kutimiza lengo hiyo.

54. Je, watu binafsi wanaweza kuwa washiriki wa jumuiya na chama?
Hapana, makanisa ya Kibatisti tu ndiyo yanayoweza kuwa wanachama.

55. Je, jumuiya au chama kinaweza kuliamrisha kanisa na kuliambia jinsi ya kufanya?
Hapana, Wabatisti huamini ya kwamba kanisa linaongozwa na washiriki wenyewe. Kwa hivyo, kundi lingine linaweza tu kuomba kanisa kufanya kama wanavyotaka kufanya. Hawawezi kuwaamrisha.

56. Basi, jumuiya na chama vinaweza kukutanaje ili waweze kukata mashauri yanayotakiwa?
Wajumbe wa mkutano wa mwaka huwachagua viongozi wa kamati kuu. Hawa huangalia kwamba maazimio yale yaliyopitishwa na wajumbe kwa kupiga kura ni lazima yafanywe na kuchunga kazi. Huchunga pia matatizo mapya na mahitaji mapya ambayo yametokea katikati kabla ya mkutano mkuu wa mwaka.

57. Je, kiongozi au kamati yaweza kusema kwa ajili ya kundi lote?
Kiongozi ye yote husema tu kwa ajili yake na vile vile kwa ajili ya kamati. Wanaweza pia kusema yale ambayo kundi au kamati imewaambia kusema.

58. Je, jumuiya zote au vyama ni vikundi vinavyojitegemea peke yao?
Ndiyo, maana yake ni kwamba wanajiongoza wenyewe. Hakuna kundi ambalo linalitawala au kuliongoza lingine. Yaani, jumuiya ya eneo inajiongoza yenyewe. Vile vile jumuiya ya nchi au chama hujiongoza wenyewe. Wako huru kufanya mapenzi ya Mungu wakiongozwa na Roho wa Mungu.

59. Kanuni gani ingeongoza kufanya kazi pamoja na madhehebu mengine?
Hizi ni: ushirikiano au muungano uweze kutimiza shabaha ya kanisa. Muungano unaweza kusaidia katika kuielea Biblia, muungano unaweza kutoa ushuhuda kwa watu wasio Wakristo.

60. Kunapasa kuwepo uhusiano gani kati ya makanisa na serikali ya taifa?
Kanuni ya kukubalika ni hii kwamba kuwe na kanisa huru katika taifa huru. Wanafikiriana lakini hawatawaliani.

61. Kuna usawa gani wa mafikira ya kanisa na serikali?

Wote hufikiri juu ya utulivu wa nchi, ustawi na hali ya watu, uaminifu na udhaifu wa wale wanaotumikia serikali.

62. Je, Wakristo wana wajibu kwa serikali yao?
Ndiyo, wanapaswa kuwa raia wema. Wanapaswa kuwaombea viongozi wao na kuwa mfano wa Yesu katika vitu vyao.

## SURA YA KUMI

Unaweza kusoma zaidi kuhusu mapatano, taarifa na makundi ya kanisa katika sura ya kumi.

63. Je, kanisa liwe na mapatano?
Ndiyo, kanisa lenye busara liandike mapatano yake, katiba na kauli za msingi wa imani yake.

64. Je, kanisa laweza kujiandikia mapatano yake lenyewe?
Ndiyo, kanisa liwe na mapatano yake lenyewe katika maandishi. Washiriki wahakikishe kwamba mapatano hayo yameandikwa kueleza nia, imani na desturi ya kanisa hilo.

65. Je, kanisa liweke taarifa?
Ndiyo, kitabu cha taarifa ya kanisa na cha taarifa ya hazina lazima viweko na kuandikwa sawasawa.

66. Kuwe na nini katika kitabu cha taarifa ya kanisa?
Karani wa kanisa aandike taarifa zote za mashauri ya kanisa. Kuwemo pia na orodha ya washiriki wa kanisa ikionyesha jinsi kila mmoja alivyojiunga na kanisa na alivyotoka katika kanisa. Vyote viwekwe pamoja.

67. Kwani kuna haja ya kuwa na taarifa sawasawa ya hazina?
Ndiyo, taarifa nzuri huzuia shida nyini zisizo za lazima.

68. Je, kanisa liwe na vikundi ambavyo vinatumika kwa mahitaji ya washiriki?
Ndiyo, vikundi vya kujifunza Biblia, kwaya, vijana, wanawake na wanaume. Vikundi vinaweza kulisaidia kanisa kukua.